**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 17 Aprili, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mhe. Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI.**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa Mwaka 2006 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Education Authority for the year* 2006).

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Mwaka 2006.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE:**
Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje kwa Mwaka 2006.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 67

**Upimaji wa Sifa za Watendaji wa Serikali**

**MHE. MUSSA A. ZUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, mipango mingi mizuri ya Serikali huwa inashindwa kutekelezwa ama kutokana na sababu kuwa baadhi ya Watendaji wake hawana sifa wanazodai kuwa nazo:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupima upya sifa za Watendaji wake na taaluma zao ili mipango yake iwafikie wananchi kwa haraka na kwa ufanisi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mbunge wa Ilala, ninapenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Serikali huajiriwa na kuendelea kudumu katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia sifa za kielimu, kitaaluma, uwezo na uzoefu kama ilivyoanishwa katika Miundo ya Utumishi *(Schemes of Services)* ya kada mbalimbali Serikalini. Aidha, mchakato mzima wa kuajiri hufanya kwa umakini mkubwa ikiwa ni pamoja na uhakiki sifa ambazo zinahitajika kwa nafasi husika.

Mheshimiwa Spika, Miundo ya Utumishi Serikalini hupitiwa kila baada ya muda usiopungua miaka mitano (5) na kuhuishwa ili kukidhi sifa na mahitaji ya kazi kwa wakati husika. Aidha, kila mwaka watumishi wa Serikali hupimwa utendaji kazi kwa kuzingatia sifa zao na malengo waliojiwekea. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Sera ya Menejimenti na Ajira ya mwaka 1998, ilikwishaona umuhimu wa kupima sifa za watendaji wake na taaluma zao, ili mipango yake iwafikie wananchi kwa haraka na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kutokutekelezwa kwa baadhi ya mipango ya Serikali halitokani na Watendaji kutokuwa na sifa bali kukosekana kwa uwajibikaji na usimamizi mzuri katika baadhi ya Ofisi za Umma. Hata hivyo, endapo Mheshimiwa Mbunge anao ushahidi wa watendaji ambao waliidanganya kwa kuonyesha sifa ambazo hawana ningeshauri awasiliane na vyombo husika ili watendaji hao waweze kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuvuliwa madaraka waliyopewa.

Na. 68

**Kuyeyuka kwa Barafu Katika Mlima Kilimanjaro**

**MHE. SUSAN LYIMO** aliuliza:-

Kwa kuwa, hali ya hewa inaizid kuwa mbaya kila siku, mito na mifereji imekauka na mingine kutoweka kabisa hii ikiwa ni pamoja na kupunguza kwa kiasi kikubwa cha barafu katika kilele cha Mlima Kilimanjaro:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuunusuru Mlima Kilimanjaro?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barafu iliyo katika kilele cha Mlima Kilimanjaro imepungua kwa kiasi kikubwa. Kupungua kwa barafu hiyo kumethibitishwa na tafiti mbalimbali zilizofanywa na wataalam wa ndani na nje ya nchi.

Utafifiti wa kisayansi kuhusu hali ya barafu ya Mlima Kilimanjaro umefanywa kwa muda mrefu kuanzia mwaka 1887. Maandiko yanayotokana na utafiti huo ya mwaka 1891 ya Hans Meyer mpaka yale ya mwaka 2004 ya Kasser, Hardy, Hyera na wengineo yamehusu kupungua kwa barafu ya mlima huo.

Mtafiti Lonnie Thompson wa Chuo Kikuu cha Ohio, nchini Marekani akishirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ameonyesha kwamba:-

- Mlima Kilimanjaro kihistoria ulikuwa na maeneo sita yenye barafu (*ice fields*)
- Sasa ni maeneo matatu tu yaliyobaki ikiwa ni pamoja na lile eneo kubwa la ukanda wa Kaskazini wa theluji lijulikanalo kama (*North Ice Field*) ambalo urefu wake ni kati ya mita 49 na 51.

Mtafiti Jacques Blot wa Chuo Kikuu cha Bordeaux, Ufaransa anaripoti kwamba tangu mwaka 1912 mpaka sasa theluji ya Mlima Kilimanjaro imepungua kwa zaidi ya asilimia 80. Ripoti za tafiti mbalimbali zinaonyesha kwamba theluji ya Kilimanjaro sio tu inapungua kina bali hata kwa mapana yake.

Wanasayansi wamebaini kwamba kupungua kwa barafu katika Mlima Kilimanjaro kunatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya joto (*air temperature*), kupungua kwa unyevunyevu katika hewa (*air humidity*), kupungua kwa mawingu, kupungua kwa mvua na kuongezeka kwa nguvu za mionzi ya masafa mafupi (*shortwave radiation*), katika kipindi cha miaka mia moja na ishirini (120) iliyopita. Hivi karibuni wanasayansi wamebaini sababu nyingine kubwa ya kupungua kwa barafu hiyo ni mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na ongezeko la joto duniani kwa kiasi cha wastani nyuzi joto 0.6 *centigrade* katika kipindi cha miaka 100 iliyopita.

Kuyeyuka kwa barafu kumeripotiwa pia dunia kote, mathalani milima yenye barafu ya Kenya na Rwenzoni, Afrika ya Mashariki na Andes, Amerika ya Kusini na Evarest na huko Tibet Asia.

Miaka ya 1800 mlima Kenya ulikuwa na maeneo 18 yenye barafu ambapo sasa yamebaki maeneo 11. Inakisiwa kwamba barafu yote itatoweka katika miaka 20 ijayo. Mwaka 1966 mlima Ruwenzori huko Uganda ulikuwa na vilima 6 vyenye barafu, lakini sasa barafu imebakia kwenye vilima 3 tu.

Barafu ya mlima Evarest imepungua kwa zaidi ya kilomita 5 tokea mwaka 1953. Inakadiriwa kuwa barafu hiyo hupungua kati ya mita 10 na mita 15 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi ni ya ulimwengu wote, tunachoweza kufanya kama nchi ni kuendelea kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (*United Nations Framework Convention on Climate Change)* na Itifaki yake, ya Kyoto yaani *Kyoto Protocol.* Tunaungana na nchi yote zinazoendelea kuzitaka nchi zilizoendelea kupunguza kwa kasi kubwa zaidi utoaji wa gesi zinazoleta ongezeko la joto, ongezeko linaloleta mabadiliko ya tabianchi. Lakini barafu ya juu ya mlima Kilimanjaro ni sehemu tu ya ikolojia ya Kilimanjaro yote. Hivyo basi tunachoweza kufanya pia ni kuboresha mazingira ya mlima na eneo lote linalozunguka mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kwa niaba ya wananchi wa Rungwe Mashariki kuwapongeza kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wabunge wawili walioingia Bunge hivi Karibuni, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mbeya, na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura Mbunge wa Tunduru. Nachukua nafasi hii vilevile kuwapa pole wananchi wa Kilosa na familia ya Marehemu Haron Chiduo, Mwenyezi Mungu aiweke mahala pema roho ya marehemu peponi.

**MHE. SUSAN LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ambayo nadhani kwa kiasi kikubwa yametuelimisha, wengi, lakini pamoja na majibu hayo na maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Waziri amekiri kwamba, kuyeyuka kwa theluji kwa mlima Kilimanjaro kunatokana na hali mbaya ya joto duniani ulimwenguni kote, na kwa kuwa Tanzania tumeridhia na kusaini mkataba wa Kyoto. Je, Waziri anatuambia nini? kuhakikisha kwamba nchi kubwa kama Marekani ambayo inatoa utoaji wa gesi inayoleta joto duniani nao wanasaini au wana-*ratify* mkataba ule wa Kyoto.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nilikuwa naomba kumwomba Waziri atueleze kwa kuwa hali hii mbaya ya joto imesababisha pia *level* ya usawa wa bahari kupanda, na kwa kuwa tunajua maeneo mengi ya Dar es Salaam yalizungukwa na bahari. Je, kuna mkakati gani pia wa kusaidia tatizo hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)]:** Mheshimiwa Spika, nchi zilizoendelea zinatakiwa kutokana na mkataba wa Kyoto, kupunguza gesi wanayotoa hewani kwa kiasi cha asilimia 5.2 gesi ya waliyotoa mwaka 1990 ifikapo mwaka 2012. Nchi zote zinazoendelea isipokuwa Marekani, Canada na Australia ndizo ambazo zimeridhia mkataba wa Kyoto. Kwa hiyo, juhudi kubwa sasa inayoendelea ni kuweza kuzishawishi nchi hizi hasa hasa Marekani kwa kuwa wanatoa kiasi cha gesi cha asilimia 25 ya gesi yote inayotolewa duniani ziweze kusaini mkataba wa Kyoto. Lakini juhudi kubwa zinatokana na wananchi wa Marekani wenyewe kwa mfano jimbo la Califonia lenyewe limeshajiwekea viwango na majimbo mengine katika

nchi ya Marekani wanaendelea kufanya hivyo. Kuna shinikizo kubwa sana kwa utawala hasa wa sasa wa George Bush kuweza kukubaliana na kusaini mkataba wa Kyoto. Lakini juhudi hizi bado mpaka sasa hazijazaa matunda zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, moja ya matokeo ya joto ni kuongezeka kwa kina cha bahari, kwa maana ya ujazo wa maji ya bahari na athari zake ni mmonyoko wa fukwe nyingi za bahari nyingi duniani ikiwa ni pamoja na zile za Tanzania kwa sababu sisi tuna bahari kiasi cha urefu wa kilomita 800. Tunachoweza kufanya sasa kwa kweli, moja ni kutojenga karibu na bahari, kwa maana hiyo kuzingatia sheria zetu sisi wenyewe kwamba kuna kiasi fulani cha mita ambacho huruhusiwi kujenga kisheria. Kwa hiy, sisi wenyewe tumeshajiwekea hiyo sheria inabidi tuifuate. Lakini vilevile miundombinu isiende karibu sana na bahari, kama mtakavyojua kwamba hata visiwa vingine vimesha zama hapa hapa Tanzania kama vile kisiwa cha Maziwe sehemu za Pangani

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Nakushukuru kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika swali la msingi Mheshimiwa aliyeuliza alikuwa hakuzungumzia mlima Kilimanjaro, lakini juu ya kukauka kwa mito, mifereji na kadhalika na hasa hata mkoa wa Pwani kule kwangu Kisarawe, mabwawa yamekauka, hali ambayo inatishia maisha ya watu. Na kwa kuwa tafiti alizozitaja Mheshimiwa Waziri zimegusia kwamba sababu kubwa ziko zile zinazosababishwa na hali ya *nature* na harakati za binadamu. Sasa majibu yake yamelenga katika kuzuia hali ya *nature* lakini hayajazungumzia juu ya harakati za binadamu. Je Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba uchomaji wa misitu, kilimo cha holela na mambo mengine ambayo yanafanywa na binadamu vinazingatiwa na kudhibitiwa ili kuweza kuzuia hali hii ya ukame ambao unaenea kila mahali?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, amenisaidia kwa sababu ameshaorodhesha mambo ambayo inabidi tusiyafanye, kama vile tusikate miti hovyo, tusichome mioto hovyo yaani mioto ile michanga na shughuli nyingine za binadamu ambazo zinaathiri mazingira. Yote haya yako katika mkakati wa Serikali ambao Mheshimiwa Makamu wa Rais ametangaza tarehe 1 Aprili, 2006 unaohusu hifadhi ya ardhi na vyanzo vya maji. Lakini vilevile kuna sheria ya mazingira sheria Na. 20 ya Mwaka 2004 ambayo vilevile inatusaidia katika hifadhi ya mazingira nchi. Lakini kama ninavyosema jambo kubwa kwa kweli ni elimu kwa umma, sisi sote hata tukiweka sheria za namna gani, lakini kama hatutazifuata, au kama hatutaelewa athari kubwa ya mazingira kwa maendeleo ya binadamu hatuwezi kufanikiwa.

Na. 69

**Kubomolewa kwa Nyumba Wanazoishi Wakimbizi**

**MHE. FELIX KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mikoa ya Kigoma, Kagera, Tabora na Rukwa imekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza falsafa ya ukarimu wa Watanzania kwa kuwapokea wakimbizi katika Mikoa hiyo; na kwa kuwa wakimbizi hao wamekuwa wakiishi kwenye nyumba zilizojengwa na Shirika la *UNHCR;* na kwa kuwa mara wanapoondoka Shirika hilo hubomoa nyumba hizo na kuacha uharibifu wa mazingira:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha majengo hayo baada ya kuondoka wakimbizi yanabaki mikononi mwa Serikali badala ya kuyabomoa na kuhamisha vifaa vya ujenzi kupeleka mahali pengine penye wakimbizi?

(b)Je, Serikali inadhibiti vipi uamuzi usiofaa wa Shirika hilo ili kuhakikisha kwamba hakuna ukiukwaji wa makubaliano ya mkataba unaokwenda sambamba na sheria zinazowasimamia wakimbizi kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa *Viena Convention Article 51* kuhusu ukarabati wa maeneo yanayoathiriwa na ujio wa wakimbizi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida nyumba au vibanda wanamoishi wakimbizi ambavyo hujengwa kwa udongo na kuezekwa kwa majani ama plastiki, zimekuwa zikibomolewa mara wakimbizi wanaporejea kwenye nchi yao ya asili ama kuhamishwa baada ya kambi husika kufungwa kwa sababu zifuatazo:

- Kuepuka nyumba au vibanda hivyo kuwa maficho ya majambazi.
- Kudhibiti tabia ya baadhi ya wakimbizi kurejea nchini kwao na kurudi kinyemelea ili waendelee kupata misaada (*recycling*).
- Kusawazisha ardhi na kupanda miti katika maeneo yaliyokuwa na nyumba au vibanda hivyo katika jitihada za kupambana na uharibifu wa mazingira.

Hata hivyo, majengo ya kudumu ambayo hutumika kama shule, zahanati, ofisi za mashirika mbalimbali, mabweni pamoja na miundombinu mingine iliyojengwa na Jumuiya ya Kimataifa, kupitia *UNHCR,* havitakiwi kubomolewa bali, *UNHCR* huvikabidhi kwa Serikali ili vitumike kwa shughuli za kijamii kwa wananchi wa maeneo hayo baada ya kambi husika kufungwa. Mfano wa makabidhiano hayo upo katika yaliyokuwa makazi ya Kigwa, Tabora ambayo sasa ni shule ya sekondari ya Serikali. Pia yaliyokuwa Makazi ya Likuyu, Ruvuma ambayo sasa yamekuwa Chuo cha Maliasili na iliyokuwa Kambi ya Umukaliro, Karagwe ambayo nayo imekuwa shule ya msingi. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, imeamua kuyatumia majengo na huduma nyingine zilizopo katika eneo lililokuwa Kambi ya Karago kama shule ya sekondari ya wasichana. Kwa sasa taratibu zinafanyika ili kukabidhi Serikalini maeneo ya Kambi zilizofungwa hivi karibuni za Lukole B. na Mbuba zilizoko wilayani Ngara.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko Mbunge wa Muhambwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi, mkakati wa Serikali ni kutumia mali, majengo na miundombinu yote iliyotolewa na Jumuiya ya Kimataifa kusaidia hifadhi ya wakimbizi kwa manufaa ya wananchi wa sehemu husika na Taifa kwa ujumla baada ya makambi hayo kufungwa.

(b) Kuhusiana na hatua zinazochukuliwa kudhibiti vitendo vya ukiukwaji wa makubaliano ya Geneva ya mwaka 1951 kuhusu Hifadhi ya Ukimbizi, vinavyofanywa na watumishi wa *UNHCR*, tunapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa tumekuwa tukichukua hatua muafaka za kidiplomasia dhidi ya watumishi wote wa *UNHCR* wanaobainika kujihusishwa na vitendo vinavyohatarisha maslahi ya Taifa.

Na. 70

**Vifungo kwa Akina Mama Wanaojifungua Magerezani**

**MHE. MOHEMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa baadhi ya akina mama wanaohukumiwa kifungo baadhi yao huwa na mimba na baadaye hujifungua wakiwa Gerezani.

Je, Serikali haioni kuwa ni vyema kwa akina mama wanaokutwa na hali hiyo kutumikia nusu ya kifungo chao kwa sababu baada ya kujifungua wamekuwa watu wawili yaani mama na mtoto?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mbunge wa Jang’ombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa wapo wanawake ambao huingia gerezani wakiwa wajawazito na hatimaye kujifungua wakiwa bado gerezani kama ama mahabusu au wafungwa.

Mheshimiwa Spika, wafungwa wajawazito hupewa huduma muhimu zinazowafaa kwa hali yao kwa muda wote hadi wanapojifungua. Baada ya kujifungua wafungwa hao huwa huru kuwaacha watoto wao wakalelewa uraiani na ndugu zao mara baada ya kipindi cha kunyonyesha kumalizika. Wafungwa wanawake ambao watoto wao hukosa ndugu wa kuwachukua, asasi binafsi huruhusiwa kuwachukua na kuwalea.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Mheshimiwa Mbunge la kutumikia nusu ya kifungo halikubaliki kwa sababu itakuwa kama kumshirikisha mtoto kwenye adhabu isiyo ya kwake. Hata hivyo wanawake hawa hupewa kipaumbele kwenye Mpango wa *Parole,* Mpango wa Huduma kwa Jamii *(Community Service Programme)* na Msamaha wa Rais kwa kutegemea makosa yaliyowatia hatiani na vifungo walivyohukumiwa.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, huwa wakati wanapojifungua ndiyo wakati mgumu wa kulea mtoto mpaka anapoachisha, kwanini Serikali haiamui kuwaachia kwa muda huo wakanyonyesha wakamaliza halafu wakaanza kutumikia vifungo vyao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kitu ambacho kinafanya atoke ndani ya gereza hasa wanawake ambao ni wajawazito tunaangalia kosa wanalolifanya pale ambapo *Parole* inatumika au pale ambapo tunaamua kuwaingiza katika *Community Service Programme*. Suala la kujifungua mtoto si kati ya masuala ambayo yanaangaliwa. Ni suala la kosa lililotendeka na muda ambao mtu amekaa gerezani.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba hawa akina mama wakijajifungua kwa miezi mitatu wanabaki kule magereza wakinyonyesha watoto wao. Swali langu ni kwamba wakati akina mama wakinyonyesha watoto wao. Je, wanapewa sehemu maalum za kulala ili waweze kunyonyesha watoto wasiambukizwe magonjwa ya kuambukiza huko gerezani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Magereza ya akinamama hapa nchini hayana msongomano. Pili wanawake ambao wamejifungua ndani ya magereza yetu wanapewa sehemu maalum ya kulala na wanapewa huduma zote ambazo akina mama ambao wamejifungua wanastahili kupata. *(Makofi)*

Na. 71

**Kufutwa kwa Zabuni kwa Kivuko cha Pangani**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH** aliuliza:-

Baada ya aliyepewa zabuni ya kivuko cha Pangani kufutiwa zabuni yake. Je, Serikali inasema nini sasa juu ya tukio hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU – (MHE. DR. MILTON MAKONGORO MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kivuko kilichopo sasa cha *MV* Pangani hutoa huduma ya kuvusha abiria na magari katika Mto Pangani na kina uwezo wa kubeba tani 35 na kilinunuliwa mwaka 1972. Kutokana na uchakavu huo, ikiwa ni pamoja na umri wa kivuko kuwa mkubwa na pia kutokana na ongezeko la abiria wanaotumia kivuko hicho tarehe 20/01/2006 Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) ilitangaza zabuni ya ununuzi wa kivuko hicho. Baada ya ufunguzi wa zabuni tarehe 12/04/2006 na kufanya uchambuzi, kampuni *M/S Africa Marine* ya Mombasa, Kenya ilishinda zabuni ya kuleta kivuko kipya.

Kampuni hiyo ilikataa kusaini mkataba huo kwa visingizio mbalimbali na kutaka masharti mapya ambayo hayakuwepo kwenye *tender documents* za awali. Kutokana na masharti hayo kutokukubaliwa hatimaye zabuni hiyo ilifutwa mwezi Agosti 2006 na *Bid security* ikachukuliwa (*forfeited*). Baada ya hapo kampuni hiyo ilifungua kesi Mombasa Kenya dhidi ya *TANROADS* ili warudishiwe *bid security* pamoja na kupewa ruhusa ya kusaini mkataba kwa masharti waliyotaka kuongeza.

Hadi sasa kesi hiyo bado inaendelea. *TANROADS* wameomba Benki ya Dunia kibali cha kutangaza zabuni hiyo upya toka tarehe 13/09/2006 lakini hadi sasa kibali hicho hakijatolewa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) inatarajia kutangaza tena zabuni ya kununua kivuko hicho kipya cha Pangani baada ya kupata kibali *(no objection)* toka Benki ya Dunia. Kwa sasa Wizara yangu inafuatilia kwa karibu Benki ya Dunia ili kibali hicho kiweze kutolewa haraka.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yenye kusikitisha kidogo. Unafahamu kwamba mwaka jana kwenye Bajeti nilizungumza kwa nguvu sana suala la kivuko cha Pangani na Serikali ilikubali kwamba mpaka Aprili mwaka huu kivuko kingekwishafika Pangani.

Lakini kutokana na hayo yaliyotokea Wilaya ya Pangani inaathirika kiuchumi kwa maana ya ujenzi wa Barabara vijijini, huduma za jamii, mashamba ya mkonge na kadhalika. Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba kwa hali ilivyo kwa kivuko cha Pangani sasa hivi Serikali ipo tayari kusimamisha kivuko ili kisije kikaleta athari au maafa kwa wananchi wa Pangani?

La pili, Mheshimiwa Rais alipokuja Pangani wakati wa kampeni alishindwa kuvuka kwa sababu ya usalama wa kivuko, Mheshimiwa Waziri Mkuu ziara yake ilikuwa *within one hundren metres* kwa sababu tulishindwa kumvusha kwa sababu ya kivuko cha Pangani. Majimbo yetu ni ya Chama cha Mapinduzi (CCM) tunataka kutekeleza na kusimamia Ilani ya Uchaguzi.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba awahimize watendaji ili kivuko cha Pangani kipatiwe ufumbuzi wa dharura ili kisije kikaleta maafa?

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua sana umuhimu wa kivuko hicho na ndio maana juhudi ambazo nimezieleza tunaendelea kuzifanya ili tuweze kupata kivuko kipya na kwa kweli tunavyofikiria kama itakuwa Benki ya Dunia bado wanaendelea kujivuta na kutotoa *no objection,* tunafikiria katika Bajeti zinazokuja tuweke Bajeti ya fedha zetu wenyewe ili Serikali inunue kivuko hicho kwa umuhimu uliopo. Lakini hiyo itategemea kama kweli tumeona kwamba hii njia ya kupata fedha kutoka Benki ya Dunia imekwama kwa sababu hatuwezi tukangojea wakati Wananchi wanateseka.

Mheshimiwa Spika, kusema kwamba tusimamishe kila kivuko, kwa kweli hilo napingana tena na lile swali lake la pili kwa sababu mimi ningedhani twende kwenye mapendekezo ya pili kwamba tuhakikishe kile kivuko kinaendelea kufanya kazi, tuwahimize watendaji na mafundi wetu waendelee kuhakikisha kwamba kivuko kiko katika hali angalau ya kuendelea kufanya kazi ili kuendelea kuwahudumia Wananchi. Iwapo tukikisimamisha tunaamini kabisa kwamba wananchi wataendelea kupata tabu zaidi na kwa kweli mimi nilikuwa pale na Waziri Mkuu na tuliona vile vimtumbwi vinavyotumiwa na Wananchi ni hatari zaidi, lakini kama wataalam watafika mahali wakatuhakikishia kwamba kivuko hiki hakiwezi kutumika ni hatari kabisa, basi hatuwezi kuwa na njia tutakisimamisha lakini baada ya kuona kwamba kwa kweli haiwezi kuwa *serviceable* kabisa.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba kampuni ambayo ilikuwa imeshinda zabuni imefungua mashtaka katika Mahakama ya Mombasa, Kenya lakini waliotangaza zabuni ni *TANROAD* ya Tanzania. Hivi ni kwa nini shauri hilo lisingefunguliwa katika mahakama ya Tanzania ambako ndiko kulikotolewa kazi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Manju S.O. Msambya kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, siyo sisi tuliofungua shauri hilo ili tuamue tufungue wapi, wao wenyewe ndio waliofungua na ni halali yao kufungua hapa au kule waliko wao kwa sababu ni Kampuni ya Kenya na tumewekeana mkataba tukijua kwamba ni Kampuni ya Kenya wameamua kutumia sheria za nchi walikokuwa *registered* kufungua shauri, hii ni juu yao lakini sisi tuko tayari kuji-*defend* kwa sababu tunaamini kabisa kwamba taratibu za *tender* hazikufuatwa au zisingeweza kufuatwa na tungejiletea matatizo kama

tungekubali wao wabadilishe masharti baada ya kwamba tumeshamaliza na tumefungua zabuni.

Na. 72

**Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege na Bandari Zanzibar**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki imelenga kuboresha mahusiano ya kiuchumi kwa wananchi wa nchi hizo zote tatu ikiwa ni pamoja na visiwa vya Zanzibar na kwa kuwa mtandano wa usafiri wa anga na majini utawawezesha wananchi wa nchi hizo kujiendeleza kijamii na kiuchumi kwa upana zaidi:-

(a) Je, kuna mpango gani wa kupanua na kuviimarisha viwanja vya ndege vya Zanzibar na Karume?

(b) Je, kuna mpango gani wa kuzipanua na kuziendeleza bandari za Zanzibar, Wete na Mkoani?

(c) Kama mipango hiyo ipo ni lini inatarajiwa kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:

Jumuiya ya Afrika Mashariki inasisitiza ushirikiano katika masuala ya kiuchumi hususan katika kuboresha miundombinu. Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar ni miongoni mwa miradi iliyopewa kipaumbele katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tayari Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeombwa na *Secretariat* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwasilisha miradi ikiwemo ya Bandari kabla ya mwisho wa mwezi Aprili, 2007.

Ni matumaini yetu kuwa Zanzibar itawasilisha kwenye *Secretariat* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki miradi ya uendelezaji wa bandari kabla ya mwisho wa mwezi huu. Hatua hiyo itaiwezesha Jumuiya kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo na hivyo kuimarisha juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ambayo ilishaanza kupanua uwanja wa ndege wa Zanzibar na kuboresha viwanja vya ndege vilivyosalia ili viwe vya kisasa zaidi.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Swali langu ni kama ifuatavyo. Kwa kuwa sasa hivi mchakato wa kuchukua maoni ya Shirikisho la Afrika Mashariki unaendelea na kwa kuwa baadhi ya Watanzania wameonyesha kutokuwa na imani na shirikisho hilo au wameingiwa uwoga, swali langu ni kama ifuatavyo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukatueleza ni vitu gani ambavyo Tanzania tutavikosa ambavyo sasa hivi hatuna na vitu gani ambavyo tutavipata ambavyo unadhani kwamba vinatupelekea sisi mpaka tujiunge katika shirikisho hilo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amina Mpakanjia, kama ifuatavyo. Kwanza kabisa niseme kwamba hivi sasa Kamati iliyoundwa kukusanya maoni inaendelea kufanya kazi hiyo na kwa hivi sasa Serikali isingependa kuonekana kwamba iko upande wa kupigia debe shirikisho au kulikataa shirikisho kwa sababu tumesema tuwaachie Watanzani watoa maoni yao na mwisho wa siku tutazingatia maoni yao. Kwa hiyo, nikianza sasa hivi kueleza ni vitu vipi tutavikosa huenda katika kufanya hivyo watu wengine wakatafsiri kwamba sasa Serikali inapiga debe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niruhusu nisifanye hivyo ila tu nimwombe Mheshimiwa Amina Mpakanjia, tusubiri Kamati imalize kazi yake. (*Makofi*)

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza na pia nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jibu lake katika swali la msingi. Wakati akijibu swali la msingi Mheshimiwa Waziri alizungumzia habari ya bandari na viwanja vya ndege vya Zanzibar, lakini alipokuwa anajibu swali la nyongeza lililopita amesema kwamba hivi sasa bado tuwaachie Wananchi waendelee kutoa maoni halafu swali la Afrika Mashariki lifanye kazi baada ya maoni hayo. Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba katika jawabu la viwanja vya ndege na bandari za Zanzibar alikuwa akifanya nadharia kuliko ukweli kwa sababu suala la shirikisho bado halijakaa sawa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Tahir, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa nikijibu swali kuhusu miundombinu nimezungumzia masuala ya miundombinu, katika maswali ya ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zipo hatua nne. Hatua ya kwanza ni ushuru wa forodha, hatua ya pili ni soko la pamoja na hatua ya tatu ni sarafu moja na mkataba unasema mambo yakiwezekana tunaweza kwenye shirikisho. Lakini sasa masuala ya miundombinu hivi sasa tunaendelea kushirikiana na hayo yataendelea shirikisho liwepo au lisiwepo na ndio maana tuna masuala ya barabara za Afrika Mashariki, ndio maana tunalenga kuboresha miundombinu ya reli za Afrika Mashariki, ndio maana tunalenga kuboresha masuala mbalimbali ya usafiri katika Ziwa Victoria na katika mambo mengine, mambo hayo yanaendelea shirikisho liwepo au lisiwepo. (*Makofi*)

Na. 73

**Matumizi ya Visa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki**

Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na mwuliza swali.

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Michael Lekule Laizer amenitaarifu kwamba ameliondoa. Kwa hiyo, tunahamia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Natulia kidogo kumpa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu hakutarajia alidhani bado tutaendelea na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ahsante ameshafika sasa swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Severina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 74

**Nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Nyumba la Taifa lina majukumu ya kuzifanyia matengenezo nyumba zake na kukusanya kodi katika nyumba hizo; na kwa kuwa Shirika hili linamiliki nyumba katika Wilaya ya Bukoba Mjini katika Mtaa wa Miembeni ambapo kuna wakazi waliokaa kwa muda mrefu katika nyumba hizo na wanalipa kodi.

(a) Je, kwa nini nyumba hizo hazifanyiwi matengenezo na shirika hilo?

(b) Je, kwanini viwanja vinavyozunguka nyumba hizo, zinagawiwa kwa watu tofauti na wakazi wanaokaa katika nyumba hizo tena bila kuwahusisha?

(c) Je, kama Shirika limeshindwa kuzihudumia nyumba hizo halioni kuwa huo ni muda muafaka wa kuwauzia nyumba hizo wale wanaoishi katika nyumba hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Savelina Mwijage Mbunge Viti Maalum, swali lake lenye vipengele (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika nyumba alizozitaja Mheshimiwa Mbunge katika Mtaa wa Miembeni sio mali ya Shirika la Nyumba la Taifa. Nyumba hizo zipatazo 68 zilihamishiwa katika miliki ya Halmashauri ya Mji wa Bukoba mwaka 1991 ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali ambalo lilitolewa wakati huo. Kutokana na hali hiyo

namshauri Mheshimiwa Mbunge aelekeze swali lake kwa Halmashauri ya Mji wa Bukoba ambapo ndo wamiliki halali wa nyumba hizo na viwanja vinavyozizunguka.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kufuatana na majibu ya Naibu Waziri aliyonijibu sikuridhika nayo kwa sababu mimi swali langu nimelielekeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwa hiyo, kurudisha Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba nitakuwa sijatendea haki. Kwa hiyo, naomba yeye mwenyewe anieleze na aweze kunifafanulia kwa sababu zile nyumba ziko Manispaa na ofisi ni ya Ardhi. Kwa hiyo, anipe jibu kamili la kuniridhisha.

**SPIKA:** Naona Mheshimiwa Mbunge amekung'ang'ania kabisa. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mehshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge Savelina Mwijage, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo au maelezo kutoka Serikali kwa sababu Serikali ni moja.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1993 Serikali iliamua kurudisha nyumba katika Halmashauri za Miji pamoja na Halmashauri za Wilaya. Katika Mkoa wa Kagera walirudishiwa nyumba 185 zikiwepo nyumba zilizopo katika Mji wa Bukoba.

Mheshimiwa Spika, nyumba nyingine ziliuzwa kwa Wananchi katika miji mbalimbali ukiwemo pia Mji wa Bukoba. Halmashauri zina uwezo wa kuwauzia Wananchi zile nyumba wakipenda au ina uwezo wa kuingia ubia na watu mbalimbali. Kwa kumsaidia Mheshimiwa Mbunge na pia akitaka tutashauriana Halmashauri ya Mji wa Bukoba kuwashauri wafanye nini na hizo nyumba kwa sababu tumeshauri Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni. Kwa mfano nyumba ambazo ni *old urban quarters* wameingia ubia na wafanyabiashara mbalimbali na nyingine wako tayari kuziuza kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningependa kumridhisha Mbunge kwamba nitakuwa tayari kabisa kushirikiana na Halmashauri ya Bukoba na kwenda kuzitizama hizo ili kuweza kuwashauri wafanye nini kuwafurahisha Wananchi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Namwona Mheshimiwa Mbunge Savelina Mwijage, anatabasamu kuonyesha jinsi alivyotoshelezwa na jibu, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofi*)

Na. 75

**Fidia Zinazotolewa Baada ya Kunyang'anywa Eneo**

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH (K.n.y. MHE. MWINCHOUM A. MSOMI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ina mpango wa kuendeleza Mji wa Kigamboni kwa kupima viwanja na kuvigawa kwa ajili ya makazi, viwanda, masoko, shule na nyumba za ibada; na kuwa, katika zoezi kama hilo Serikali huchukua ardhi zenye mimea na mazao kutoka kwa wananchi wa maeneo husika na kuwalipa fidia ndogo isiyokidhi mapato aliyokuwa anapata mwananchi huyo. Mfano fidia isiyopungua shilingi 50,000/= kwa mwembe unaoingiza mapato yasiyopungua shilingi 200,000/= kwa mwaka, na kumpatia kiwanja kimoja ambacho hutakiwa kukilipia:-

(a) Je, Serikali haiioni kuwa, inawaongezea wananchi umasikini badala ya kuwapunguzia, kwa sababu fidia ni ndogo na haithamini uhai uliobaki kwa mimea?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kutoa viwanja kutokana na ukubwa wa eneo lililochukuliwa badala ya utaratibu unaotumika sasa wa kutoa kiwanja kimoja tu tena kwa kununua?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo, fidia ya ardhi na mimea inayotolewa na Serikali wakati wa kuendeleza miji hutolewa kwa mujibu wa Kanuni za Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 (Kanuni ya 3 ya Kanuni za kukadiria fidia za mwaka 2001) ambazo zinaelekeza kuwa mlipaji wa fidia anatakiwa kutambua mali halali itakayohusika na kufidia kutokana na hali ya soko kwa wakati huo pamoja na fidia ya ardhi tupu. Aidha, sheria hiyo inatoa fursa kwa mfidiwa kulipwa posho mbalimbali kama vile:-

(i) Posho ya usumbufu wa posho ya usafiri;

(ii) Posho ya upotevu wa faida kulingana na mtiririko wa mapato na faida inayopatikana kwa kuzingatia: "*Audited Accounts*" inayotolewa na vyombo vya kisheria kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Sheria ya Ardhi, Kanuni ya 12;

(iii) Kodi ya pango kwa miaka mitatu;

(iv) Umri wa zao husika; na

(v) Kulipwa kwa wakati na kadhalika.

Katika fidia ya mashamba na mimea iliyomo, posho inayotolewa kwa mfidiwa na ile ya usumbufu na upotevu wa faida.

Mheshimiwa Spika, viwango vya fidia ya mimea vinavyotumiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi hufanyiwa uchambuzi wa kitaalam na wataalam wenye elimu na ujuzi wa tabia za mimea, kuhusu ukuaji wake na gharama ya utunzaji hadi kuanza kuzaa matunda na kutoa Ankara ya viwango hivyo kwa kila aina yam mmea.

Wataalam hawa ni kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Wizara yangu huweka kipengele cha hali ya "Soko" kutokana na utafiti unaofanywa. Viwango vya fidia ya ardhi hufanyiwa utafiti wa soko lililopo la ardhi kutokana na sehemu ardhi hiyo ilipo, kwani thamani ya ardhi hutofautiana kutokana na pale ilipo.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo haya ya utangulizi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

(a) Fidia itolewayo kwenye mimea inazingatia thamani ya zao hilo kwa mujiubu wa soko la wakati huo na makadirio yake hutegemea hali halisi ya mmea kama ulivyokutwa na mtaalam siku ya uthamini. Serikali kwa kuwianisha tabia za ukuaji na gharama za utunzaji wa mmea kwa mimea mbalimbali na kutafiti soko lake, inaweza kuweka viwango thabiti vya thamani ya mimea mashambani.

Aidha, kwa vile hali ya soko la mimea hubadilika sana utafiti wa bei za soko hufanywa mara kwa mara ili kuendana na soko kwa mujibu wa sheria. Ni kwa sababu hii Serikali inalipa viwango hivi na wala hailengi kumwongezea umaskini mtu bali kuhakikisha Ardhi inatumika vizuri na kwamba mwananchi aliyechukuliwa ardhi yake anafaidika kwa kulipwa fidia anayostahili kisheria. Kuna ushahidi wa kutosha wa wananchi waliofidiwa katika maeneo ya mradi ambayo kwa kiasi kikubwa yalikuwa hayazalishi wametumia fedha za fidia kununua nyumba, kujenga nyumba au kununua magari.

(b) Lengo la Serikali kutwaa maeneo makubwa ni kupata maeneo yatakayowezesha kupata viwanja vingi ili wananchi wengi wenye uwezo wa kujenga wajenge nyumba hivyo kupunguza uhaba wa nyumba mijini na kupata maeneo kwa ajili ya huduma mbalimbali za kijamii. Azma hiyo ya Serikali haitafikiwa iwapo baada ya kutwaa maeneo hayo yatakamilishwa kwa wamiliki wa awali ambao hata hivyo walishindwa idadi ya nyumba na majengo ambayo sasa yanajengwa na wamiliki wapya.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sheria haki ya mwananchi aliyemiliki eneo hukoma baada ya mwananchi huyo kulipwa fidia. Ardhi hiyo inakuwa ni ya Serikali. Hata hivyo kwa misingi ya ubinadamu Serikali imekuwa ikitoa kipaumbele kwa mwananchi kununua kiwanja/au viwanja katika eneo hilo; na kama alikuwa na nyumba humilikishwa kiwanja chenye nyumba kwa bei ndogo sana, iwapo nyumba yake itaangukia ndani ya kiwanja cha makazi.

**MHE. ABDULKARIM ESMAIL HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Kwa kuwa Serikali imeona kwamba mimea na ardhi ni suala muhimu ambalo linaweza likamwondolea umaskini mwananchi. Je, sasa hivi Serikali iko tayari kutoa waraka maalum ambao unaelezea uwazi wa thamani ya ardhi na mmea kwa Wilaya zote katika nchi hii?

(c) Kwa kuwa hivi karibuni pametokea kuchukuliwa mashamba na Halmashauri ya Mafia kwa ajili ya kupima viwanja na kujenga shule pamoja na mambo mengine ya kimaendeleo kwa maana ya Halmashauri ndio imechukua eneo hilo. Je, Serikali inaweza ikaielekeza Halmashauri ya Mafia kwamba wale waliochukuliwa mashamba hivi sasa Halmashauri ikae, iangaliea na ithamini na itoe tathmini halisi kwa wale waliochukuliwa mashamba ili waweze kulipwa kulingana na thamani ya mmea uliopo na hali kama alivyoelezea Mheshimiwa Naibu Waziri kuliko walivyolipwa sasa hivi kwa mmea Shs.6,000/= kitu ambacho kinamdidimiza Mwananchi na mwananchi yule kunyimwa kiwanja katika eneo la shamba lake ambalo Halmashauri imeitwaa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Abdulkarim Shah, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Mheshimiwa Mbunge amezingatia kwamba tuwaeleze wananchi ukweli uliopo na taratibu ambazo zinafuatwa katika kutoa fidia na ameomba tutoe taarifa kamili ambayo itaelezea wananchi. Ninapenda kusema kwamba Serikali imeelezea yote hayo katika sheria zake namba nne na namba tano na hata juzi sheria ambayo tumeitoa ya Mipango Miji tumeelezea kwa kirefu kabisa na Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni Mwinchoum Msomi alitupa ushauri kwamba tutoe elimu kwa wananchi ili waweze kuelewa thamani ya ardhi na vitu ambavyo tunavitumia au njia ambayo tunaitumia kuthamini ili waelewe na waweze kuridhika na Serikali yao, tumekubali hilo tutalifanya kwa kutoa elimu ya sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu eneo la Mafia, Serikali imeweka mikakati maalum kupitia Wizara yangu ya Ardhi tumewaelekeza Halmashauri kupima maeneo ya viwanja katika miji na katika maeneo mengine na vile vile ilipe fidia ambayo inatosha. Naomba kumfafanulia Mheshimiwa Mbunge kwamba fidia tunayotoa ya mazao tunatumia wataalam wa Wizara ya Kilimo na wataalam hawa wanajua kabisa tabia ya mmea umekuwa kwa muda gani, mmea huo unaweza kudumu kwa muda gani kwa mfano hatuwezi kulinganisha mmea kama mti wa mtiki tulinganishe na mti wa korosho au tulinganishe na mpapai au na mgomba. Kwa hiyo Wizara ya Kilimo imezingatia haya kitaalam kabisa nitakachoweza kufanya sasa hivi Mheshimiwa Mbunge ni kuwasiliana na Halmashauri ya Mafia kuwaelekeza wazingatie sheria namba tano ya vijiji na sheria namba nne ya miji kuhakikisha kwamba wanachi wanalipwa fidia kama tulivyoelekeza katika sheria hizo. (*Makofi*)

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la Wananchi kuchukuliwa ardhi yao kwa ajili ya kupisha miradi mbalimbali ya Serikali lililopo Mafia na Kigamboni linafanana kabisa na tatizo linalowasibu Wananchi wa Kata za Burige, Ngaya na Kinaga kwenye Jimbo la Msalala ambao ardhi yao imechukuliwa kupisha mradi wa maji wa kwenda Kahama kutoka Victoria na mpaka sasa hivi wananchi wale hawajalipwa chochote na hawajui watalipwa namna gani.

Je, Serikali ina mpango gani au inasema ni lini itawalipa Wananchi hawa ili kuwaondolea tatizo ambalo wamekuwa nalo na wameongezewa umaskini kwa sababu mashamba yao yamechukuliwa na hawana pesa ya kununua maeneo mengine?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ezekiel Maige, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, haya matatizo kusema kweli yako katika maeneo mengi nchi nzima, la kwanza ambalo Wizara yangu inaweza ikalifanya ni kutoa elimu kufuatana na sheria tatu sasa zimekuwa pamoja na hii ambayo mmetupitishia juzi itakaposainiwa na Rais nadhani matatizo haya mengi yatapungua.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba naomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie kushirikiana na Serikali katika kuleta maendeleo katika maeneo yetu. Kwa mfano viwanja ambavyo vinapimwa eneo mojawapo la Kigamboni lililopimwa viwanja 8000 katika watu waliokuwa na maeneo 2500 waliolipwa fidia, ni wazi kabisa kwamba kwa watu 8000 kuhamia katika lile eneo wataleta maendeleo zaidi kuliko wale 2500 ambao walikuwepo pale.

Mheshimiwa Spika, huo ni mfano tu lakini kuhusiana na maeneo yanayochukuliwa kwa ajili ya vyanzo vya maji, kwa ajili ya barabara hayo yote ni kuleta maendeleo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, nimeongea na Mheshimiwa Ezekiel Maige jana na nimekubaliana naye kulifuatilia suala hili kupitia Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Ardhi, kuhakikisha watu wa eneo lake wamelipwa.

Na. 76

**Ucheleweshaji wa Fedha za Mikopo Vijijini**

Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na mwuliza swali.

**SPIKA:** Kwa bahati nzuri lile swali refu sana linalofuata limeondolewa na Mheshimiwa Kilimbah kwa hiyo tunahamia Wizara ya Maliasili na Utalii swali linaulizwa na Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu.

Na. 77

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Jimbo la Magu hasa waishio kando kando ya Ziwa Victoria wamekuwa wakiliwa na mamba na wakulima kusumbuliwa sana na wanyama waharibifu wa mazao kama vile nguruwe mwitu, nungunungu na tumbili, ambao wmezaliana sana.

Je, kwa nini Serikali isichukue hatua ya haraka ya kuwawinda wanyama hao kwa kuwaua ili kuwapunguzia wananchi kero?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Usimamizi wa wanyamapori unaendeshwa kwa kuzingatia Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 na Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974. Kwa mujibu wa Sera ya Wanyamapori, jukumu mojawapo la Wizara ni kutatua migogoro baina ya binadamu na wanyamapori.

Katika kutekeleza mkakati huu, jukumu la kudhibiti wanyamapori waharibifu kimsingi ni kazi ya Halmashauri za Wilaya ikiwemo wananchi kujilinda dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu. Hata hivyo, kwa kuzingatia ukubwa wa kero, Wizara huwa imashirikiana na Halmashauri za Wilaya pale inapotokea taarifa za kuwepo kwa tatizo.

Njia zinazotumika kudhibiti kero kutokana na wanyamapori ni kuwaua wanyama wanapotishia usalama wa binadamu, mifugo na mazao kuwaweka wanyama kama mamba kwenye *quota* maalum ili kuwawinda kibiashara kwenye maeneo yenye matatizo sugu na kuwashauri wananchi kuchukua tahadhari za kujilinda wenyewe na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Kikosi Dhidi Ujangili Kanda ya Serengeti, imefuatilia suala la kuwepo kwa wanyamapori waharibifu hususan mamba, tumbili na nungunungu kwa kuwasiliana na Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu ili kupata picha halisi kuhusiana na kero hizi. Taarifa zilizopatikana zinaonesha kuwepo kwa matukio ya wanyamapori kusababisha madhara kwa wananchi.

Kwa mfano, kati ya mwaka 2004 – 2007, kumekuwepo na matukio manne (4) ya watu kuuawa na mamba kando ya Ziwa Victoria, Wilayani Magu. Watu waliouawa ni kutoka Vijiji vya Kongoro, Bukome na Senga.

Hata hivyo, matukio haya hayakutolewa taarifa kwa Wizara yangu katika wakati muafaka kwa ajili ya ufuatiliaji na hatua za kuchukuliwa. Mbali ya kujitokeza kwa hali hii, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, kuwa Wizara yangu itakuwa tayari wakati wowote kudhitibi wanyama waharibifu pindi itokeapo na taarifa kutufikia kwa wakati muafaka.

Aidha, baada ya taarifa ya wananchi wanne (4) kuuawa na mamba kufika Wizarani, mawasiliano yanafanyika ili kupata kumbukumbu za wananchi hao kuwezesha familia zao kulipwa kifuta machozi.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Magu ambao wanaathirika mara kwa mara na tatizo la kuliwa na mamba, napenda kuipongeza Serikali kwa kufanya mawasiliano ya kuwezesha kulipwa familia za wahusika walioliwa na mamba kifuta machozi na naomba hilo lifanyike haraka ili angalau wafarijike.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mamba halipo tu kwenye vijiji alivyovitaja vya Kongolo, Bukome na Senga kuna matukio yameripotiwa na mimi nimeyaripoti matukio haya kwa wahusika katika Kata za Rutale, Kitongosima, Kahangala, Magu Mjini na Lubugu.

Mheshimiwa Spika, watu walioliwa na mamba siyo hawa wanne katika miaka minne ambayo ameitaja mwaka 2004 mpaka 2007.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri atapokea kumbukumbu nyingine tukimletea za watu ambao ni wazi kwamba waliliwa na mamba?

Mheshimiwa Spika, je, Waziri hawezi kukubaliana na mimi kwa sababu tatizo hili ni kubwa katika Wilaya ya Magu kwa wanyama waharibifu wanaokula binadamu kama mamba na viboko na pia kwa wanyama waharibifu kama nungunungu na tumbili wanaoharibu mazao. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna umuhimu wa kufanya *operation* maalum ya kuwawinda wanyama hawa ili wapungue?

Kama hilo haliwezekani Serikali au Wizara iko tayari kutenga fedha maalum kwa ajili ya kuwawezesha wananchi watekeleze mikakati yao ya kuwapunguza wanyama hao waharibifu?

Kama nungunungu na tumbili wanaoharibu mazao. Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna umuhimu sasa wa kufanya *operational* maalum ya kuwawinda wanyama hawa ili wapungue? Na kama hilo haliwezekani Serikali ama Wizara iko tayari kutenga

fedha maalum kwa ajili ya kuwawezesha wananchi watekeleza mikakati yao ya kuwapunguza wanyama hao waharibifu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (MHE. ZABEIN MUHAJI MHITA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu katika jibu la msingi kwamba taarifa ambayo tumeipata kutoka kwa Halmashauri ya Wilaya ya Magu ni kuwa wananchi wanne tu ndiyo waliouawa na mamba, lakini kutokana na kauli ya Mheshimiwa Mbunge kwamba wapo zaidi ya watu wanne ambao wameuawa na mamba. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, kwamba tukipata taarifa hizo tutazifanyia kazi na waliopata adhari hizo familia zao zitalipwa kifuta machozi. (*Makofi*)

Vilevile Wizara iko tayari kufanya *operational* maalum kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge kutokana na hali mbaya ya wanyama ambao wapo katika Wilaya ya Magu wanaoleta uharibifu kwa binadamu na kwa mali zao. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, swali la nyongeza.

**MHE. ERNEST GAKEYA MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa sababu katika vijiji alivyovitaja vya Senga na Mkome viko katika Wilaya ya Geita na tatizo kubwa la hawa mamba linatokana na kuzaliana katika Hifadhi ya Taifa ya Rubondo na Hifadhi ya Rubondo ndiyo ina mamba wengi ambao wanawasumbua wananchi wa Kijiji cha Mharamba, Senga yenyewe na Mkome.

Je, Serikali inasema au itakuwa na tamko gani kuhusu hawa mamba ambao wamezaliana sana katika Hifadhi hii ya Rubondo na kuwasumbua wananchi wanaolizunguka Ziwa Victoria?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafanya sensa ya mamba katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja na baada ya kupata idadi kamili ya wanyama hao itapanga mkakati wa kuanza kuwavuna ili kupunguza madhara yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, swali la nyongeza la mwisho.

**MHE. HASNAIN GULAMABBAS DEWJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii.

Sambamba na mamba kwetu kuna matatizo makubwa na tembo. Kwa kuwa tembo au ndovu hawapigwi siku hizi wamekuwa wengi na wanaingia kwenye mashamba ya wananchi na kusababisha athari kubwa na hasara kwa wananchi.

Je, Serikali ina mpango wa kuwapa vibali ili ndovu hao au tembo hao wapunguzwe?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mbunge wa Kilwa, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika maeneo machache tembo wameongezeka na wanastahili na wanaharibu mashamba na maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itashirikiana na Halmashauri za Wilaya husika ili kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoshwa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa kuwa bado muda tunao na maswali yamebaki matatu tu natoa upendeleo maalum kwa Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mwenyekiti wa *NEMC,* kwa sababu yeye ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mazingira nchini.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa upendeleo maalum.

Bado ninarudi kwenye eneo la mamba. Pamoja na matatizo haya ya mamba yanayoendelea katika sehemu nyingi sana katika maziwa mbalimbali hapa nchini vilevile katika ziara zangu kule Chunya maeneo ya Songwe kandokando ya Ziwa Rukwa kumekuwa na malalamiko mengi sana ya kwamba mamba wamezaliana kiasi ambacho hupiti hatua tano bila kuona mamba na wamekuwa na tabia hiyo hiyo ya kula binadamu.

Je, Mheshimiwa Waziri ana mpango gani ambao uwe mpango endelevu atakaosaidia ili kupunguza idadi ya mamba katika Ziwa Rukwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya na Mwenyekiti wa Baraza la Mazingira la Taifa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Chunya hasa Chunya na eneo la Ziwa Rukwa mamba waliokuwa wametolewa kwenye *quota* ya uwindaji wa mwaka jana haikuwindwa ikakamilika hivyo hilo limechangia kwa mamba katika eneo hilo kuongezeka kupita kiasi.

Mheshimiwa Spika, katika *quota* ya mwaka huu mamba watakaoondolewa katika eneo hilo itaongezwa ili kukabiliana na tatizo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wanyama wa pori wanaweza kuongezeka katika maeneo kwa muda mfupi na hili huwa tunalibaini kwa ripoti tunazopata pamoja na kufanya sensa. Napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametupa taarifa hizi na wale ambao wametuandika barua na kwamba taarifa hizo tutazifanyia kazi na kuhakikisha kwamba tunapunguza madhara ya wanyamapori kwa binadamu. **(***Makofi***)**

**SPIKA:** Ahsante sana lakini kabla sijamwita Mheshimiwa Fatma A. Mikidani nimepokea tu taarifa hapa kutoka kwa Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kwamba kuna mpiga kura wake ameliwa na Simba wanne**,** Simba wanne wamemshambulia mtu mmoja, pole sana.

Na. 78

**Viwango vya Malipo ya Pensheni kwa Wastaafu**

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI** aliuliza**:-**

Kwa kuwa, malipo ya pensheni kwa watumishi mchanganyiko yaani wenye taalum na fani mbalimbali wa Serikali waliostaafu kuanzia mwaka 1995 mwezi Juni kurudi nyuma kima cha chini ni Sh. 21,600/= kwa mwezi bila kujali cheo mtu alichokuwa nacho wakati wa utumishi wake na kwa kuwa katika Sheria ya Fedha yaani *Finance Act Na. 15* ya mwaka 2004 ukurasa wa 961 *part (x) Amendment of Public Retirement Benefits Act 1999* haikutoa ufafanuzi wowote kuhusu kima cha chini cha wastaafu kuwa ni kiasi gani kwa tarakimu wala kwa asilimia fulani isipokuwa inazungumzia *Minimum Pension* tu, na kwa kuwa, watumishi waliostaafu baada ya mwaka 1995 hadi 2005/2006 na kuendelea wanalipwa Shilingi 85,000/=

(a) Je, Serikali haioni kuwa kima cha chini cha Sh. 21,600/= kinacholipwa kwa wastaafu wa miaka ya 1995 hakifanani na hali halisi ya kupanda kwa gharama za maisha?

(b) Je, kwa nini Serikali isiangalie upya Sheria hiyo kwa lengo la kuweka viwango vilivyo sawa kwa wastaafu wote?

(c) Je, kwa nini Serikali isibadilishe mfumo wa malipo ya pensheni ili uwiane na mabadiliko ya mishahara ya watumishi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kima cha chini cha Shilingi 21,600.00 kinacholipwa kwa wastaafu wa miaka ya 1995 na kurudi nyuma hakifanani na hali halisi ya kupanda kwa gharama za maisha.

(b) Mheshimiwa Spika, haitawezekana kuweka viwango sawa kwa wastaafu wote kwa sababu malipo ya pensheni yanakokotolewa kwa kutumia mishahara na muda mtumishi aliyotumikia Serikali, sasa mtumishi aliyetumikia Serikali kwa miaka 10 ilingane na mtumishi aliyeitumikia Serikali yake miaka 40 je, itakuwa umemtendea haki aliyetumikia miaka 40? Hata hivyo, kwa upande wa mishahara watumishi wote hawapati mishahara sawa hata kama waliajiriwa pamoja kwa sababu wana vyeo tofauti hata nyongeza zao pia ni tofauti. Hata hivyo, Serikali kwa kupitia watalaam wa pensheni wanaangalia uwezekano wa kuboresha malipo ya pensheni ili viwango hivyo viweze kulingana na hali ya maisha.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu (b) Serikali kupitia wataalamu wa masuala ya pensheni wanaangalia namna ya kuweza kuboresha viwango vya pensheni kwa wastaafu wake wote.

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mishahara hii ya pensheni ni mikataba kati ya wafanyakazi na Serikali na wala siyo hisani.

(a) Je, ni kwa nini inachelewa kulipwa? Inachukua muda ndipo ilipwe kwa watu wenye kima cha chini?

(b) Mishahara hii inalipwa kwa wale watu wa chini kabisa inachukua muda mrefu sana kulipwa kwa miezi miwili au mitatu na tujue kwamba kundi kubwa la wafanyakazi Serikalini ni lenye watoto hawa wanaolipwa mishahara hii. Je hatuoni kwamba tunakaribisha rushwa kazini?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Kwa kweli, pensheni zote zinalipwa wakati mmoja bila kulinganisha kwamba pensheni ya huyu ni ndogo na ya mwingine ni kubwa. Pensheni nyingi zinalipwa kila baada ya miezi sita kwa utaratibu uliopo na wala haichukui kwamba huyu ni mstaafu ambaye ana pensheni ndogo na pensheni kubwa. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILBROD PETER SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wastaafu ni watu waliojitolea maisha yao katika kutumikia taifa na taifa tumefika hapa tulipo kwa ajili ya jasho la hawa wastaafu wetu, na kwa kuwa mapato haya au fedha hizi wanazolipwa ndicho kinachowawezesha sasa wao waweze kuishi baada ya kujitolea maisha yao.

Je, Waziri atakubaliana kwamba sasa wakati umefika wa kurekebisha sheria kama tatizo ni sheria ili pensheni hii iendane na maisha na kiwango cha chini cha malipo ya mshahara kwa wakati uliopo sasa hivi ili hali yao iweze kuwa bora na tusiendelee kuwaumiza watu ambao walijitolea maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Willbrod Peter Slaa, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi hiyo kazi sasa inafanywa na haitegemei Sheria peke yake. Lakini vilevile itategemea na uwezo wa Serikali na mimi nikiwa ni mmojawapo naumia kwa sababu na mimi ni mstaafu wa miaka 12 iliyopita. Kwa hiyo, nakuhakikisha kwamba na mimi vilevile naathirika.

**SPIKA:** *Order Paper* yangu kumbe imekosewa lilirukwa swali la Namba 80 na 81 loh! Kumbe bado tuna kibarua kikubwa.

Swali linalofuata ni la Wizara ya Kilimo naona, bado fedha? Samahani kidogo ukurasa mmoja wa *Order Paper* ya Spika naona haupo.

Ah! Swali namba 79 linaulizwa na Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kwa niaba ya Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji.

Na. 79

**Ripoti ya Tume Kuhusu Gharama za Muungano**

**MHE MOHAMED HABIB JUMA MNYAA (K.n.y. MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tume ya Pamoja ya Fedha iliyoundwa mwaka 2003 iliwasilisha Serikalini ripoti ya mapendekezo kuhusu vigezo vya kuchangia gharama za mambo ya

Muungano na kugawa mapato yatokanayo na vyanzo vya Muungano, mwezi Agosti, 2006; na kwa kuwa, ni muda mrefu sasa umepita;

Je, ni nini hatma ya ripoti hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha ilikamilisha kazi ya kuandaa mapendekezo ya vigezo vya kugawa mapato na kuchangia gharama za Muungano na kuwasilisha ripoti yake kwa Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi Oktoba, 2006. Waziri wa Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Mungano wa Tanzania (SMT) ambaye ndiye msimamizi wa Tume ya Pamoja ya Fedha *(JFC)* kisheria, alimpatia nakala za ripoti hiyo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, anayeshughulikia Mipango na Fedha, kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kwa lengo la kufanya mchakato wa ndani ya Serikali kupitia mapendekezo hayo ya Tume. Kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uchambuzi wa ripoti hiyo umekamilika na maoni yameandaliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata Maoni ya pande zote mbili za Muungano, Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) itakamilisha Waraka wa Baraza la Mawaziri kwa lengo la kupata uamuzi rasmi wa Serikali.

**MHE MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je Mheshimiwa Waziri haoni kwamba uchelewashaji huu unawakatisha tamaa wananchi kwa kuona kwamba hakuna *seriousness* ya jambo hili? Hilo ni swali la kwanza.

Swali la pili, je, endapo upande mmoja wa muungano utakataa mapendekezo hayo ni nini kitafanyika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kama ifuatavyo:

Wananchi wasikate tamaa, kama nilivyosema kila kitu ni lazima kiende na mchakato wake na kuhakikisha kwamba kinafanywa barabara na kwa ufanisi ili pande zote mbili ziridhike.

Tutaangalia kama upande mmoja watayakataa yote hiyo bado ni dhana potofu ambayo naomba tusiifikirie hivyo kwa vile tunaombea mafanikio siyo kushindwa. Aidha tutakaa Serikali zote mbili kuangalia namna ya kufikia muafaka kwa faida ya nchi yetu.

Na. 80

**Ruzuku Itolewe na Serikali kwa Wakulima**

**MHE. EPHRAIM NEHEMIA MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliamua kuinua kilimo kwa kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa mazo mbalimbali:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kuwa, samadi ya ng'ombe ni pembejeo muhimu katika ukuzaji na uendelezaji wa kilimo cha zabibu?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba wakulima wengi wa Dodoma hivi sasa wana harakati za kulifufua zao la zabibu baada ya bei na soko lake kuanza kuimarika?

(c) Je, Serikali iko tayari kutoa ruzuku katika upatikanaji wa samadi, kama pembejeo muhimu kwa wakulima wa zabibu kwa kuchangia angalau katika usafirishaji wake kutoka kwa wenye mazizi hadi mashambani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mbunge wa Dodoma Mijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba samadi ya ng'ombe ni pembajeo muhimu katika uzalishaji wa mazao likiwemo zao la zabibu. Matumizi ya samadi katika maeneo mengi ya Mkoa yamesaidia kuongeza rutuba ya udongo na hatimaye kuongeza tija na uzalishaji wa mazao. Napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Madeje na Viongozi Mkoani Dodoma kwa kuhimiza matumizi ya samadi mkoani humo.

(b) Mheshimiwa Spika, Kutokana na takwimu za uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuna ongezeko la uzalishaji wa zao la zabibu. Katika mwaka wa 2005/2006 inaonyesha kwamba eneo lililolimwa mizabibu lilikuwa hekta 470 na uzalishaji ulikuwa tani 1,670 za zabibu. Lengo ni kwamba, ifikapo mwaka wa 2009 hekta 2,561 na mizabibu zitalimwa na kuzalisha tani 10,895 za zabibu katika Mkoa wa Dodoma. Kwa hiyo, nakubaliana na Mheshimiwa Madeje kwamba Wakulima wengi mkoani Dodoma wameamua kuongeza uzalishaji wa zabibu kwa kasi kubwa.

(c) Mheshimiwa Spika, bei ya mbolea za viwandani imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na hivyo kufanya wakulima kushindwa kununua mbolea na matumizi ya mbolea kuwa chini. Kutokana na hali hii matumizi ya mbolea nchini ni kilogramu 9 kwa hekta ikilinganishwa na kg 53 Afrika ya Kusini, 27 Malawi, na China kilo 279 kwa hekta. Serikali ilianza kutoa ruzuku ya mbolea katika mwaka wa 2003/2004 ili kuongeza matumizi ya mbolea viwandani na kumpunguzia mkulima makali ya bei ya mbolea.

(d) Kutokana na sababu za msingi kama vile mazingira ya kuzalisha mbolea ya samadi, kutokuwepo mfumo rasmi wa soko la mbolea ya samadi na kadhalika. Mbolea ya samadi bado haijaingizwa katika mpango wa ruzuku hata hivyo, kupitia Mpango Maalum wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya *(DADPs)*, wakulima wa Mkoa wa Dodoma wanaweza kusaidiwa kupata mikokoteni ya kukokotwa na ng'ombe ili kurahisisha usombaji wa samadi. Hivyo, napenda kumshauri Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, kuhimiza Halmashauri yake kuingiza uongezaji wa matumizi ya samadi kupitia *DADP.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. EPHRAIM NEHEMIA MADEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana lakini nitauliza swali moja tu la nyongeza.

Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana ambayo yametoa sura nzuri kuhusu maendeleo ya zao hili ambalo ni muhimu sana katika maendeleo ya wakulima wa Dodoma.

Inabidi nikubaliane naye ingawaje kwa shingo upande kwamba mazingira ya uzalishaji na ugavi wa mbolea ya samadi kwa hivi sasa hayaruhusu mfumo wa utoaji ruzuku.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na samadi kuwa pembejeo muhimu pia kuna umuhimu wa kuwa na madawa ambayo yanadhibiti magonjwa na wadudu ambao wanashambua zabibu.

Je, kwa kuwa bei za madawa haya zinapanda mwaka hadi mwaka Serikali iko tayari kutoa ruzuku kwa wakulima wa zabibu ili nao wafaidike kama wenzao ambao wanapata ruzuku kwenye mazao mengine?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ruzuku zilizotolewa kama nilivyoeleza mwanzoni kwamba tulitoa ruzuku ya mbolea ya mwaka huu yaani mwaka 2006/2007 lakini mwaka huu tutatumia kitu kinachoitwa vigezo mkakati. Vigezo mkakati ni kutoa ruzuku kwa kuzingatia ni wapi kunazalishwa nini kwa mfano mbolea tungependa itolewe kwa maeneo yale ambayo yanalimwa mahindi kwa wingi kwa mfano *the big four* yaani Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa *of course* Kigoma, Kilimanjaro na Manyara kule Kiteto waweze kupata mbolea ya mahindi mapema.

Lakini vilevile, mazao kama pamba na korosho wanatakiwa wapate madawa ama ruzuku ya madawa ya kuweza kuongeza uzalishaji bado hilo tunalizungumza katika ngazi ya Wizara.

Mazao mengine kwa mfano kahawa na chai wale wanatakiwa wapate angalau ruzuku kidogo kwa ajili ya miche bora kuongeza tija na uzalishaji. Kwa hiyo, vilevile katika zao hili la zabibu naweza kusema kwamba tunaweza tukazungumza tukaangalia ni vipi pengine hata kama siyo msimu huu pengine msimu unaokuja na wao pia kwa sababu pia tunataka uzalishaji uongezeke na wao waingizwe katika ruzuku ya madawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba tunasisitiza zaidi utumiaji wa mbolea za viwandani kwa mfano kama nilivyosema uzalishaji wa mboji ama samadi hauko *systematic* maana yake ni nini?

Hatuwezi tukapata *supply* ya samadi inayotosha kwa mashamba yetu yote, ukitaka kutumia samadi katika hekta moja tani 20 ndiyo sawa na mfuko mmoja wa *NPK.* Kwa hiyo, ni gharama kubwa na uzalishaji wa samadi utakuwa ni mdogo labda pengine huko baadaye tunaweza tukaangalia ni jinsi gani tunaweza tukafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 81

**Mgodi wa Mpanda**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mgodi wa Mpanda (*Uruwira Minerals Co. Ltd.*) uliomilikiwa na Bwana George Cohen, ulifungwa mara tu baada ya Uhuru wa Tanganyika na kwa kuwa, tafiti nyingi zimefanywa kwa lengo la kufufua mgodi huo ikiwa ni pamoja na zilizofanywa na Warusi (1970 – 1975)

(a) Je, nini matokeo ya tafiti hizo hususan zile zilizofanywa na Warusi kwa muda mrefu?

(b) Je, kutokana na tafiti hizo kuna uwezekano wa mgodi huo kuanzishwa tena?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said A. Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, lenye sehemu a na b, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kampuni ya *Uruwira Minerals Company Limited* ilichimba Madini ya risasi, fedha, shaba na dhahabu katika mgodi wa Mukwamba katika Wilaya ya Mpanda kuanzia mwaka 1946 hadi 1959. Uchimbaji wa Madini hayo ulisimama baada ya kushuka kwa bei ya Madini hayo katika soko la dunia mwaka 1957 na 1958 pamoja na upungufu wa mashapo katika eneo hilo.

Katika jitihada za kugundua mashapo zaidi, kati ya mwaka 1970 – 1973 Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Urusi kupitia kampuni ya *Tecno Export* zilifanya uchunguzi wa kijiolojia, kijiokemia na kijiofizikia katika Wilaya ya Mpanda, likiwemo eneo la Mukwamba, uliojumuisha uchorongaji wa miamba. Matokeo ya uchunguzi huo katika kina kifupi yalionyesha kuwepo mashapo ya tani 941,177 zenye tani 37.430 za risasi na tani 32.400 za fedha katika eneo la Mukwamba. Aidha, matokeo ya kazi za utafutaji madini katika eneo la Magamba yalionyesha kuwepo zaidi ya tani 10.593 za dhahabu katika eneo hilo na hayakugundua mashapo ya kutosha ya Madini ya risasi na shaba.

Tarehe 3 Desemba, 1999 kampuni ya *Kapufi Gold Mining Company Limited* ilipewa leseni ya uchimbaji dhahabu *Mining License No 43/99* kwa ajili ya kuchimba dhahabu katika eneo la Singililwa. Kampuni hiyo ilianza uchimbaji katika eneo hilo Novemba, 2000 na kufikia Novemba, 2001 uchimbaji uliposimama kilo 53.7 za dhahabu zilishazalishwa kutoka katika eneo hilo.

Kusimama kwa shughuli za uchimbaji kulipisha utafutaji wa Madini ili kupata mishapo zaidi kwa lengo la kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa kilo 4 kwa mwezi hadi kilo 100 kwa mwezi. Kwa sasa kampuni hiyo inashughulika na utafutaji wa Madini unaojumuisha uchorongaji wa miamba.

(b) Katika Ukanda wa Madini wa Mpanda kwa sasa kuna leseni za utafutaji wa madini za kampuni za *Crystal Mkwamba Gold Mining Co. Ltd, Sun Mining Ltd.* na *Nyati Mining (T) Ltd*. Kampuni hizo zinaendelea kufanya utafutaji wa Madini, Iwapo mashapo ambayo yanaweza kuchimbwa kwa faida yatagundulika ni dhahiri mgodi utaanzishwa katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni dhahiri matumaini tuliyokuwa nayo watu wa Mpanda ya kufufuliwa kwa mgodi inaonekana yanayenyuka na hili lilikuwa linafahamika na ndiyo maeneo hayo yakawa yanaendelezwa na wachimbaji wadogo wadogo:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wametoa leseni ya utafutaji madini kwa makampuni ikiwemo Cyrstal Mkwamba *Gold Mining Company Limited*, limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa wachimbaji wadogo wadogo waliokuwa wakitafuta riziki zao katika eneo hilo kwa sababu wamepewa eneo lenye urefu wa zaidi ya kilomita 80; Je, Serikali sasa itatazuia vipi mgogoro kati ya *Gold Mining Company* na wachimbaji wadogo wadogo kule Mpanda?

(b) Nilipata kuuliza kuhusu wachimbaji wadogo wadogo ambao wamezagaa katika nchi nzima, nini sera na mwelekeo wa Serikali kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo kule Mererani, Tarime, Tunduru, Kahama, Mpanda, Chunya na maeneo mengi katika nchi yetu ambao wanahangaika kama kuku wa kienyeji.

Sasa Serikali inasemaje kuwasaidia hususan wachimbaji wadogo wadogo waliopo katika maeneo ya Katisunga, Ipidi na maeneo ya Kampuni katika Wilaya ya Mpanda? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru na kumpongeza kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia kero za wapiga kura wake.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba pia kumtia matumaini kwamba asikate tamaa, Serikali inafahamu uchungu na kilio cha Watanzania na hasa wale ambao amewaongelea wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunaendelea kushughulikia utatuzi wa migogoro mbalimbali inayohusu maeneo ya madini. Ningependa tu nimweleze Mheshimiwa Mbunge na niliarifu Bunge hili Tukufu pamoja na kwamba sasa hivi hatujapata mgao rasmi katika Wizara yetu kutoka maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, lakini juhudi zinaendelea kuhakikisha kwamba tunaboresha shughuli za wachimbaji wakubwa lakini pia wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, la pili, la sera na mikakati ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo. Suala hili linajibiwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kuanzia mwaka 2005 mpaka 2010, mikakati mingi imeorodheshwa pale. Namkaribisha Mheshimiwa Said Arfi apitie Ilani yetu.

Lakini pia kwa ufafanuzi naomba niwaarifu wananchi kwamba juhudi zimekuwa zikiendelea kama wanavyosikia tunashirikiana na wawekezaji wakubwa kwanza kwa kuwapatia maarifa lakini pia vitendea kazi.

Tunawaratibu na tunawahamasisha kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wanajiunga katika Vyama vya Ushirika ili iwe rahisi zaidi kwa Serikali kutekeleza mipango yake kupitia vikundi ambavyo vimejiandaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, pia tunajaribu kuona namna gani tunaweza kuwasaidia kuwawezesha kimitaji na pia tunaendelea kuwatengea maeneo wachimbaji wadogo wadogo. Ahsante sana! *(Makofi)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, swali la mwisho linaulizwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**Na. 82**

**Msamaha wa Mafuta kwa Kampuni za Madini**

**MHE. LUCY T. MAYENGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika kuwavutia wawekezaji wa Madini inawapa msamaha wa mafuta wa Madini:-

(a) Je, kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Mei, 2004 hadi Aprili, 2006 kampuni za madini zimesamehewa jumla ya tani ngapi za aina zote za mafuta?

(b) Je, Kampuni gani iliyopewa msamaha mkubwa na imesamehewa mafuta kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge wa Viti Maalum, naomba nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatayo:-

Mheshimiwa Spika, msamaha wa kodi mbalimbali zinazotozwa kwenye mafuta hutolewa kwa wawekezaji wa madini kama mojawapo ya vivutio kwa makampuni ya utafutaji na uchimbaji wa Madini. Msamaha wa kodi hutolewa kwa wawekezaji wakubwa na wadogo katika sekta ya madini na siyo kwa kampuni za mafuta.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwepo kwa msamaha huo, kampuni za Madini zenye mikataba ya uendelezaji wa Madini (*Mining Development Agreement*) kati yake na Serikali hulipa dola za Marekani 200,000 kwa mwaka kwa mujibu wa mikataba hiyo

kama kodi za mafuta wanayoyatumia kwa mwaka. Kiasi hicho cha pesa ni kwa ajili ya *Road Toll* na *Fuel Tolls*.

Mheshimiwa Spika baada ya kutoa maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye maelezo ya awali, msamaha wa mafuta kabla ya swali kurekebishwa huwa hauzihusu kampuni za mafuta, hivyo, katika kipindi cha mwaka huo kwa jinsi ambavyo swali lilikuwa limetayarishwa hapakuwa na msamaha kwenye makampuni ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge baada ya kufanya marekebisho kama ifuatavyo:- Katika kipindi hicho jumla ya lita 178,217,477 za mafuta ziliagizwa au kununuliwa na kutumiwa na kampuni sita zinazochimba dhahabu ambapo jumla ya shilingi bilioni 62.8 za kodi ya mafuta zilisamehewa.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho Kampuni ya Geita *gold Mines* Limited inayomiliki Mgodi wa dhahabu wa Geita, ndiyo iliyonunua mafuta zaidi yenye msamaha wa kodi kuliko kampuni zingine. Kampuni hiyo ilinunua na kutumia jumla ya lita 62,082,039 ambapo shilingi bilioni 24.7 zilisamehewa kama kodi mbalimbali za mafuta.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Baada ya majibu mazuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa makampuni hayo hasa makubwa yanayatoka nje ya madini ambayo licha ya kupewa misamaha hiyo ya mafuta pamoja na misamaha ya kuingiza vifaa vyao, bado baadhi ya hayo makampuni yamekuwa yakiendelea kusema kwamba yanapata hasara; Je, Serikali haioni sasa kwamba umefika wakati kwa Serikali kuweza kurudisha kodi zote za mafuta pamoja na vifaa ambavyo hayo makampuni yanaviingiza ili fedha hizo ziweze kuongeza kipato kwa nchi yetu na hasa maeneo yale ambayo migodi hiyo ipo?

Mheshimiwa Spika, la pili, nilikuwa naomba kuuliza kwamba kwa kuwa migodi ya Almasi imekuwa ikitoa mrabaha wa asilimia 5 kwa Serikali na migodi ya dhahabu imekuwa ikitoa mrabaha wa asilimia 3 kwa Serikali ambapo hata hivyo Kampuni ya Alex Stuart imekuwa ikipata asilimia 1.9 na Serikali imekuwa ikipata asilimia1.1, kiwango ambacho ni kidogo kisicholingana na hali halisi ya mapato katika migodi hii?

Je, Serikali haioni sasa kwamba umefika wakati wa mikataba hiyo kwanza kabisa kuisitishwa, kuto-*renew* mkataba na Alex Stuart? La kwanza. Lakini pili, ukaguzi huo ufanywe na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, napenda kumpongeza Mheshimiwa Lucy Mayenga kwa swali lake ambalo lina lengo la kuuelimisha umma wa Watanzania ambao kila wakati hapa Bungeni tumekuwa tukiuliza je, nchi inanufaika vipi na uwekezaji wa madini?

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nijielekeze kwenye haya makampuni sita ambayo ameyazungumzia, nafikiri alikuwa anazungumzia mambo ya Kahama *Mining, North* Mara, TULAWAKA, LEZOLUT, Geita, Buhemba. Hayo makampuni sita kwa miaka ambayo ameizungumzia tumeona kwamba lita za mafuta zilizosamehewa tumesema ni bilioni 60. Mtu anaziona ni nyingi na kuuliza je, nchi tumenufaika vipi? Nchi katika hao wawekezaji kuna vitu mbalimbali ambavyo huwa inavipata wakati mtu akiwekeza nchini. Ni kodi mbalimbali mtu anazozilipa, anatumiaje katika jamii iliyomzunguka, je, amewaajiri wafanyakazi wa namna gani na wangapi, matumizi gani kwa mafunzo ya wafanyakazi na vitu vingine na amenunua vitu gani hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, sasa nilipokuwa nafanya tathmini ya haraka haraka kwa miaka miwili, nimekuta kwamba hayo makampuni manne yamelipa kodi mbalimbali hapa Tanzania ambazo tunazitoza hapa. Kwa miaka hii miwili makampuni yamelipa zaidi ya bilioni 100, matumizi kwa miradi ya kijamii zaidi ya bilioni 11, mafunzo kwa wafanyakazi zaidi ya bilioni 6, manunuzi ya hapa nchini zaidi ya bilioni 341. Kwa hiyo, hayo makampuni sita yametumia hapa nchini zaidi ya bilioni 459.6 kwa miaka miwili. Sasa mtu akiangalia tu kwa jumla jumla kwamba wamesamehewa bilioni 60 anaweza akafikiri kwamba hatuna kitu tulichofaidika nacho. Lakini hata vile tunaelewa na tunakumbuka kwamba Mheshimiwa Rais alizungumzia namna ya kurudia hii Mikataba iliyopo kuona namna gani tunaweza tukanufaika zaidi, na hilo limefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juu ya mrabaha imekuwa bahati mbaya sana kwamba huo Mkataba wa Alex Stuart ulizungumzia juu ya *percent* ya mauzo na mrabaha vilevile upo katika *percent* ya mauzo. Kwa hiyo, ikaunganika kwa pamoja kama mrabaha ni *percent* 3, na Alex Stuart *percent* 1.9 karibu kinachobaki hakuna. Lakini kwa kuanzia kweli tulikuwa tuna shaka kweli kama ile dhahabu yote ambayo inazalishwa ni kweli ni hiyo hiyo inayopatikana na Alex Stuart wametusaidia kuhakikisha kwamba ni kweli. Hakuna dhahabu yoyote inayopotea katika uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, kwa kuangalia kwamba kweli gharama hiyo ni kubwa tumekaa kama Serikali tukatathmini, sasa hii kazi tumekwishaamua kwamba tutaifanya wenyewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumepitiliza sana muda wa maswali. Sasa ni matangazo, nikianza na wageni. Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, ameniomba niwatambulishe wageni wake ambao ni watoto wake Margreth, Janeth na Anna Cosmas. Ni wale pale! Ahsante, karibuni sana vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Viti Maalum kutoka Mjini Magharibi, ameniomba pia nitambulishe watoto wake ambao ni Kassim, Yahya, Bungi na Mkewe Mwanaidi Kitiba na pia mdogo wao Faisa Ali, wale pale karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee anaye mgeni wake mmoja ndugu Ali Yussuf. Kaimu Katibu wa Wazazi CCM Jimbo la Kiembe Samaki Zanzibar yule pale! Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Killimbah anao wageni wawili, nao ni Bakari Maharia, Katibu wa CCM Kata ya Mtoha, naomba asimame yule pale! Ahsante sana, na Jumanne Mtenya Katibu wa Vijana CCM, Kata ya Kasenja yule pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Christopher Ole- Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, ameomba niwatambulishe wageni wake na Waheshimiwa hao ni wageni wa Dorah Mushi Viti Maalum, Manyara. Sasa wageni wenyewe ni Mheshimiwa Peter Tendehe ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, yule pale mkono wa kulia, karibu sana Mwenyekiti, na Bwana Paul Magatinda Mshauri wa Mradi wa *Land Management Programme* wa Simanjiro yule pale. Karibu sana. Ahsante sana. *(Makofi*)

Mheshimiwa Pindi Chana ameomba nimtambushe mgeni ambaye Mhubiri wa neno la Mungu anaitwa Pallangyo. Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa ameniomba nimtambulishe, Katekisita Zebedayo Mchiwa wa Kanisa la Anglikana, Berege Wilaya ya Mpwapwa kule Jimboni kwake. Karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa matangazo ya mikutano. Mheshimiwa Raynald Mrope, Mwenyekiti wa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara anawaomba Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kuhuduria semina ya matumizi ya umeme wa gesi asilia ya Mnazi- *Bay,* semina hiyo itafanyika leo saa 7.30 katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Kabwe Zitto ameomba nitangaze kwamba kutakuwa na Kikao cha Kambi ya Upinzani, saa 7.00 katika ukumbi wa Chifu Kasusura.

Mheshimiwa Martha Umbulla kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Kamati ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ameomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wakutane leo mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge hapo saa 7.00 mchana pale *reception* ya jengo la utawala.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anawaomba wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii wakutane leo katika ukumbi namba 133 saa 5.00 asubuhi.

Mheshimiwa George Mkuchika, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anawaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo kuwa wakutane leo saa 5.00 asubuhi hii katika ukumbi namba 219, jengo la utawala.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ameomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa wakutane saa 7.00 mchana katika ukumbi namba 219, ghorofa ya pili, jengo la utawala.

Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ameniomba niwatangazie wajumbe kwamba kutakuwa na mkutano wa Kamati ya Maliasili na Mazingira leo saa 7.00 mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa, naona wamegongana, basi Sekretarieti itaweza kuwapatia ukumbi mwingine wasikutane pale.

Mheshimiwa Juma Nh'unga Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane kwa mkutano mfupi sana saa 5.00 asubuhi kwenye ukumbi namba 227 ghorofa ya pili.

Waheshimiwa Wabunge, nakumbushia pia leo saa 7.30 mchana kutakuwa na Mkutano wa Kamati ya Uongozi ya Bunge saa 7.30 mchana katika ukumbi wa Mikutano wa Spika. Kesho saa 7.30 mchana katika ukumbi huo huo wa Mikutano wa Spika kutakuwa na kikao muhimu cha Tume ya Huduma za Bunge. Ahsante sana. Katibu kwa shughuli zinazofuata!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kusimamia Huduma ya Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona wa Mwaka 2007(*The Optometry Bill, 2007)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa hoja yangu napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wananchi wa Jimbo la Rungwe Magharibi, kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, aliyefariki tarehe 13 Aprili, 2007. Katika kipindi cha uhai wake, Marehemu Dr. Aaron Chiduo, alilitumikia Taifa hili katika nafasi mbalimbali hususan katika Sekta ya Afya. Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na maboresho mengi katika Sekta ya Afya ambapo mchakato mzima wa *Health Sector Reform* daima utaambatana na jina la Dr. Aaron Chiduo.

Marehemu Dr. Aaron Chiduo alizikwa jana na tunamwomba Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba vilevile nitumie fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wawili ambao wameungana na sisi katika kipindi cha hivi karibuni, nao ni Mheshimiwa Florence Kyendesya na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura.

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge kumtakia buheri ya afya na kumkaribisha tena Bungeni , Mheshimiwa Benedict Kiroya Losurutia, Mbunge wa Kiteto aliyerejea hivi karibuni kutoka kwenye matibabu nchini India. Ni matumaini yangu kuwa atafuata ushauri na maelekezo aliyopewa na wataalamu ili kuendelea kuwa katika afya njema kama tulivyomwona kipindi hiki hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Huduma za Upeo wa Macho Kuona wa Mwaka 2007 (*the Optometry Act*, 2007) kama ulivyopangwa kwenye shughuli za leo pamoja na marekebisho yaliyoambatishwa sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, Muswada ulio mbele yetu unakusudia kupendekeza sheria mpya itakayosimamia usajili wa wataalam wa huduma za upeo wa macho kuona na kuvisaidia vituo vya kutolea huduma za aina hiyo.

Sheria iliyopo sasa hivi ni ya mwaka 1965. Hiki ni kipindi cha miaka 42 na katika kipindi hicho mabadiliko mengi yametokea katika Sekta ya Afya, wataalam wanaosajiliwa sasa hivi chini ya Sheria hawasomeshwi tena nchini yaani *opticians* kwa sasa wanahitimu kama *Optometry* baada ya mitaala yao kubadilika kutokana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na fani yenyewe duniani. Hivyo, imefanya sheria hii ya sasa kuwa haina kazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko yanayotokea hivi sasa katika Sekta ya Afya yaani *Health Sector Reform,* madhumuni ya kuifuta sheria iliyopo ya *Optician Act*, 1965 na badala yake kutungwa nyingine *the Optometry Act*, 2007, ni kuongeza ufanisi na kuboresha huduma kwa jamii ili iendane na wakati uliopo katika nyanja za Sayansi na Teknolojia. Pamoja na mapendekezo ya kutunga sheria mpya mambo yafuatayo yanajitokeza:-

Jina la taaluma hii limebadilika kutoka *optician* kuwa *optometry,* hii ni kutokana na mabadiliko ya mitaala ya kufundishia wataalam hao. Sheria iliyopo sasa ilitungwa wakati huduma za afya kwa kiasi kikubwa zilikuwa zikitolewa na Serikali. Kutokana na kupanuka kwa Sekta ya Binafsi ni muhimu kuwepo kwa Sheria itakayoongoza na kudhibiti utoaji wa huduma hii kwa lengo la kuilinda jamii.

Matatizo mengi yametokea katika utoaji wa huduma hii kiholela. Kwa mfano, miwani ya kusomea inauzwa ovyo barabarani na wafanyabiashara wadogo na hii inaweza kuleta madhara kwa watumiaji. Vilevile Tanzania ni nchi mojawapo iliyokubali kutekeleza tamko la Kimataifa la kupunguza upofu unaozuilika ifikapo mwaka 2020 yaani *(vision 2020).*

Mheshimiwa Spika, Sheria iliyopo sasa imeonekana ina upungufu mwingi, na nitautaja kama ifuatavyo:-

Kwanza, Sheria iliyopo haizingatii jina la taaluma lililobadilika kutoka *optician* kuwa *optometry* kutokana na mabadiliko ya mitaala.

Pili, Sheria iliyopo hakuzingatia kupanua kwa sekta binafsi na hivyo kutoa mianya ya kutoa huduma hii ya macho kiholela na bila ufanisi.

Tatu, Sheria iliyopo haiko wazi kuhusu hatua zipi za kisheria zichukuliwe ili kudhibiti utoaji huu holela wa huduma hii ya macho.

Nne, Sheria iliyopo haielezi wazi ni utaratibu upi ufuatwe katika kusajili wataalam na maeneo yanayotoa huduma hii, vilevile na maadili ya wataalam hao.

Mheshimiwa Spika, tumezingatia mambo yafuatayo:-

Moja, kuhusu uhusiano wa Baraza na wataalam wanaotoa huduma. Kufuatana na utaratibu unaopendekezwa na kutungwa kwa sheria mpya uhusiano utakaokuwepo kati ya Baraza na wataalam hao umeainishwa. Masuala yafuatayo yatajumuishwa. Moja, ni kwamba msajili wa Baraza atakuwa ni msimamizi na mtekelezaji mkuu wa Sheria inayopendekezwa. Aidha, msajili katika utendaji wake wa kazi atakuwa akisaidiwa na Naibu Msajili. Pili, Baraza litawajibika kutoa viwango vya ubora wa huduma ya macho, kama vile sehemu ya kutolea huduma hii. Vifaa vya kupimia, vifaa vya kurekebishia upeo wa macho kuona na kadhalika. Kubainisha wazi shughuli za Baraza ambazo zilikuwa hazikutajwa katika sheria iliyopo sasa na vilevile Baraza litakuwa na uwezo wa kudhibiti viwango vya huduma zinazotolewa. Sheria hii vilevile itatoa maelekezo yatakayosaidia katika usajili na vilevile kuangalia maadili ya wataalam hao. Sheria hii itaainisha utaratibu wa kudhibiti utoaji holela wa huduma hii muhimu ya macho.

Mheshimiwa Spika, katika maandilizi ya Muswada huu tuliwasiliana na wadau mbalimbali ambao walitupa michango yao na imeboresha kwa kiasi kikubwa Muswada huu. Wadau hao ni pamoja na Idara mbalimbali za kujitegemea, Mabaraza ya Taaluma za Afya, Vyuo vya Elimu ya Juu, Sekta Binafsi za Taaluma za Macho, Hospitali za Rufaa, Mikoa na Wilaya wote hao walishirikishwa kikamilifu. Idara nyingine za Serikali ni pamoja na Wizara ya Elimu Juu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Chuo cha *Optometry K*CMC, Madaktari wa Macho kutoka Hospitali za watu binafsi na wataalam kutoka Vituo binafsi vya huduma za macho na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile tuliwasiliana na wadau wa *vision* 2020 *the right to see* ikiwa na maana kwamba kila mwananchi ana haki ya kuona. Hao wanasisitiza uzuiaji wa upofu unaoepukika kama vile mtoto wa jicho, vikope, kupungua kwa upeo wa macho kuona, upungufu wa vitamini A kwa watoto, *pressure* ya macho na usubi.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kuweka utaratibu wa kisheria wa kusajili wataalam wa upeo wa macho kuona na kusajili vituo vya kutolea huduma hizo. Huduma za kurekebisha upeo wa macho kuona hivi sasa zinasimamiwa na sheria ambayo imepitwa na wakati. Sheria ya sasa haiko wazi kuhusu hatua zipi za

kisheria zichukuliwe ili kudhibiti utoaji holela wa huduma hii. Mfano, kama nilivyosema hapo awali miwani ya kusomea hivi sasa inauzwa kiholela barabarani na vilevile katika baadhi ya maduka makubwa yaani *super markets*. Athari za kiafya kwa watumiaji holela wa miwani zinaweza kuleta matatizo makubwa kwa watumiaji wanaponunua miwani hiyo mitaani bila ya kupimwa au kupata ushauri wa daktari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maeneo yaliyoainishwa hapo juu, Muswada ulio mbele ya Bunge lako Tukufu umegawanyika katika sehemu tisa zifuatazo:-

Sehemu ya kwanza, inahusu mambo ya utangulizi yaani jina la Sheria, matumizi ya tasfiri mbalimbali ya maneno yakiwemo yanayoleta dhana ya kuwepo kwa kada tofuati katika utoji wa huduma ya kurekebisha upeo wa macho kuona.

Sehemu ya pili inahusu kuundwa kwa Baraza la Kusimamia watoa huduma wa kurekebisha upeo wa macho kuona, kazi za Baraza na uteuzi wa Msajili na Naibu Msajili.

Kwa mujibu wa mapendekezo hayo Baraza hilo litakuwa chombo cha juu cha kusimamia Sheria hii na kutoa ushauri katika mambo yote yanayohusu utoaji huduma ya kurekebisha upeo wa macho kuona. Katika kutekeleza hayo, Baraza limepewa uwezo wa Mamlaka ya kuunda kamati mbalimbali ili kutekeleza majukumu ya Baraza.

Sehemu ya tatu, inahusu masuala ya usajili na uorodheshwaji wa wataalam chini ya Sheria inayopendekezwa. Aidha sehemu hii inapendekeza Usajili wa wataalam wa kurekebisha upeo wa macho kuona pamoja na kuorodhesha wataalam wa kada ya *Ophthalmic Optician.*

Sehemu ya nne, inazungumzia masuala ya kufuta ama kusimamisha usajili, taratibu za kufuata katika kuchukua hatua hizo na namna ya kumrudisha muhusika katika daftari la usajili.

Sehemu ya tano, inahusu mambo ya kupokea malalamiko, uchunguzi wa malalamiko hayo na rufaa.

Sehemu ya sita, inahusu haki na wajibu wa watoa huduma ya kurekebisha upeo wa macho kuona, namna ya kumiliki vituo na kliniki za kutoa huduma za kurekebisha upeo wa macho kuona na vigezo na taratibu za kuanzisha vituo hivyo.

Sehemu ya saba, inahusu masuala ya fedha, mwaka wa fedha wa Baraza, mapato na matumizi na ulazima wa kuwasilisha taarifa za ukaguzi Bungeni.

Sehemu ya nane, inahusu makosa na adhabu mbalimbali zinazopendekezwa kutolewa kwa watakaovunjwa masharti yaliyoainishwa katika Muswada huu. Sehemu ya tisa na ya mwisho inapendekeza kuweka masharti mbalimbali kuhusiana na kutoa hati ya kuruhusu wataalam wasio watanzania kutoa huduma ya kurekebisha upeo wa macho kuona kinga za kisheria kwa Wajumbe wa Baraza la Kusimamia Huduma ya Kurekebisha

Upeo wa Macho kuona, Waziri kutengeneza Kanuni na Sheria ndogo ndani ya Sheria hii pamoja na kufutwa kwa sheria ya sasa yaani *the Opticians Act* ya mwaka 1965.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya mwisho ya Muswada ina jedwali ambalo limeainisha Muundo wa Baraza, utaratibu wa kumchagua Makamu Mwenyekiti wa Baraza, taratibu za uendeshaji wa vikao na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha mapendekezo niliyoyawasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, kama nilivyosema hapo awali yamezingatia maoni, mapendekezo na ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali. Aidha, naomba niwashukuru wadau walioalikwa na Kamati ya Huduma za Jamii ya Bunge lako Tukufu na kutoa maoni yake mbele ya Kamati Jijini Dar es Salaam tulipowasilisha tarehe 4 Aprili, 2007.

Pia nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa dhati waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Huduma za jamii chini ya uongozi thabiti wa Mwenyekiti, Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw,' Mbunge wa Babati Mjini na Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji kwa michango yao waliyoitoa kwa lengo la kuboresha Muswada. Jedwali la Marekebisho lililoambatishwa katika shughuli za leo ni matokeo kwa kiasi kikubwa ya michango mizuri tuliyopata kutoka katika Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho nimalizie kwa kuomba Waheshimiwa Wabunge mjadili mapendekezo yaliyomo katika Muswada huu na hatimaye kuupitisha na kuwa Sheria ya Kusimamia Huduma za Upeo wa Macho Kuona *(The Optometry Act 2007).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mwenyekiti au Mwakilishi wa Kamati ya Huduma za Jamii, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji karibu.

**MHE. HAJI MWITA HAJI – (Kny. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):** Bisimillah Rahman Rahim! Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Shaban Kwaangw,' naomba kuwasilisha Mezani, Maoni na Ushauri wa Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu Muswada wa Sheria ya Kusimamia Huduma za Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona wa Mwaka 2007. *(The Optometry Bill 2007).*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, uliyoipa jukumu la kufikiria na kuchambua Muswada wa Sheria mpya ya kusimamia Wataalam wa Kurekebisha upeo wa macho kuona *"The Optometry Bill"* Namba 3 ya mwaka 2007 kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa Maoni ya Kamati, naomba kuchukua fursa hii kutoa rambirambi za dhati kwa kifo cha marehemu, Dr. Aron Chiduo, Mungu

ailaze roho yake mahala pema peponi. Pia natoa pongezi zangu za dhati kwa ushindi wa kishindo alioupata Mheshimiwa Mtutura A Mtutura, (Mb.), katika uchaguzi Mdogo uliofanyika katika jimbo la Tunduru. Ushindi huo ni kielelezo sahihi kuwa wananchi wana imani kubwa kwa Serikali ya Awamu ya Nne katika utekelezaji wa sera za CCM. Karibu Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura katika Bunge hili Tukufu tuwakilishe wananchi waliotupa sote dhamana hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilikutana Dar es Salaam na kupata muda wa kutosha kufanya uchambuzi wa Muswada wa Sheria hii na pia iliweza kusikiliza maoni ya uchambuzi wa wadau wa muswada ikiwa ni pamoja na wanataaluma. Aidha, Kamati ilipitia vifungu vyote vya Muswada wa Sheria na kuhoji kila ilipobidi na kupata maelezo ya ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii na Naibu wake wakisaidiwa na jopo la wataalam na hatimaye kuridhishwa na kushauri kuwa Muswada wa Sheria hii uende hatua inayofuata ya kusomwa kwa mara ya pili hapa Bungeni. Hivyo, Kamati ya Huduma za Jamii inaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati yangu kuunga mkono hoja hii, Kamati inatoa maoni yafuatayo na ni vyema Serikali ikayazingatia kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada wa Sheria hii Bungeni unaolenga kuboresha na kuweka utaratibu mpya na mzuri kwa ajili ya kuongoza njia bora ya kutoa huduma ya kurekebisha upeo wa macho kuona kwa kutambua kuwa Sheria inayosimamia utoaji wa huduma hii *"The Optician Act,*'" *1966* imepitwa na wakati, kwani ilitungwa miaka 41 iliyopita na ni wazi kuwa mabadiliko makubwa yametokea katika taaluma na mazingira ya kutoa huduma hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa sheria hii imeletwa wakati muafaka ikizingatiwa kuwa Sheria iliyotungwa mwaka 1966 wakati ule huduma ya kurekebisha upeo wa macho kuona ilikuwa ikitolewa kwenye hospitali za Serikali tu, ambapo kwa wakati wa sasa wa utandawazi na biashara huria, huduma hiyo inapatikana pia katika hospitali za watu binafsi na mashirika mbalimbali kama vile ya dini.

Mheshimiwa Spika, mbali ya huduma kutolewa kwenye hospitali za Serikali na mashirika ya dini na watu binafsi zilizosajiliwa na Serikali chini ya utaratibu uliowekwa na sheria hiyo, jinsi huduma hiyo inavyotolewa imefikia hatua mbaya na ya hatari kwa usalama wa wagonjwa wanaohitaji kufanyiwa marekebisho ya upeo wa kuona kutolewa kiholela na watu ambao hawana utaalam wa ngazi yoyote.

Mheshimiwa Spika ni dhahiri kuwa wengi wetu tumewahi kushuhudia miwani ya kurekebisha upeo wa macho kuona ikiuzwa katika maduka ambayo si maalum kwa vifaa vya tiba.

Kwa mfano kwenye maduka ya bidhaa mchanganyiko *(Super markets)* na hata mitaani wafanya biashara ndogo ndogo wanauza miwani ya kusomea, kitendo ambacho

ni hatari kwa huduma hii muhimu kutolewa kiholela na watu ambao si wataalam na kuhatarisha macho ya wanaohitaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile, hakuna chombo kilichothibitisha kuwa vipimo vinavyobandikwa kwenye miwani hiyo ni vya kweli au hapana na Serikali haikuwahi kuchukua hatua yoyote kudhibiti uchuuzi wa miwani ya kurekebisha upeo wa macho kuona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuunda Baraza la Usajili ambalo litakuwa na jukumu la kusimamia na kuona kuwa huduma ya kurekebisha upeo wa macho kuona inatolewa na wataalam waliothibitishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa masharti yanayowekwa na Sehemu ya tatu ya Muswada wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inashauri kuwa ili Baraza hilo liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ni vema muundo wa Baraza hilo ufike ngazi ya wilaya ikizingatiwa kuwa mazingira ya utekelezaji wa sheria ya sasa kwa kiasi kikubwa umevurugwa na mabadiliko ya wakati huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali iliwezeshe Baraza la Usajili kwa kulipatia nyenzo (fedha) za kutekelezea majukumu yake na kulipa meno ya kuweza kurekebisha upungufu unaoonekena wazi kwa huduma hii kutolewa mitaani na watu ambao si wanataaluma. Mathalani miwani ya kurekebisha upeo wa macho kuona kuzagaa mitaani, na pia kuhakikisha kuwa huduma hii ambayo ni moja ya taaluma nyeti ya Afya itolewe na watalam wanaotambuliwa na Baraza kwa mujibu wa Muswada wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati inatoa maoni kuwa Muswada wa Sheria haukuweka kifungu kitakachowabana wataalam watakaosajiliwa kutoa huduma ya kurekebisha upeo wa macho kuona kujiendeleza kitaaluma mara kwa mara *(Continuous Professional Development)* kwa lengo la wataalam waliosajiliwa kwenda na wakati na mabadiliko katika tafiti za taaluma hiyo.

Hivyo, Kamati inashauri kuwa Baraza liweke utaratibu huo ikiwa ni pamoja na mitihani ya kupima uwezo wa watoa huduma kabla ya kuwapa usajili na pia baada ya kupewa usajili wa kudumu kwa lengo la kupima viwango vya utaalam wao.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya nane ya Muswada huu inayoelezea adhabu zitakazotolewa na Baraza kwa watakaokiuka taratibu zilizowekwa kuwa mwongozo wa utendaji wa waliosajiliwa, *"Code of Conduct"*, Kamati inashauri kuwa kuwepo kipengele cha kusimamishwa kwa muda usajili wa mhusika ili apate muda wa kujieleza na kurekebisha dosari zilizoainishwa katika utendaji wake kuliko kumfuta moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu adhabu mbali mbali zilizoainishwa katika ibara ya 36 ya Muswada wa Sheria, ukurasa wa 19, Kamati yangu inashauri kuwa Serikali ione umuhimu wa kutofautisha viwango vya adhabu zitakazotolewa kati ya Kituo cha Huduma na Mtaalam anayefanya makosa ya kitaaluma. Kamati inapendekeza Kituo cha huduma kipewe adhabu kubwa kuliko mtaalam. Vile vile kuhusu udhibiti wa usajili wa

watu ambao si raia wa Tanzania, Kamati inashauri liwe Baraza makini sana na kuona kuwa wageni wanaosajiliwa ni wataalam waliobobea katika taaluma za kurekebisha upeo wa macho kuona.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni hayo, Kamati yangu inapendekeza kuwa marekebisho yafanyike katika Muswada kama ifuatavyo:-

Ibara ya 3, Ukurasa wa 3 wa Muswada, Tafsiri ya neno *"Optometrist"* ambaye ni mwanataaluma wa juu kwa mujibu wa Muswada huu ameelezwa kuwa ni *''Primary Health Worker"*. Kamati inapendekeza kuwa aitwe *''Health Worker"*, neno *''Primary"* liondolewe sehemu hii na liwekwe kwa *''Opthalmic Optician"* ambaye ni mtaalam wa ngazi ya chini katika taaluma hii.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Aidha, namshukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii - Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa na Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda, pamoja na wataalam kutoka Wizara hii, ambao kwa pamoja tulishirikiana katika kufanikisha kukamilika kwa kazi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati wajumbe wa Kamti ya Huduma za Jamii kwa ushirikiano wao mkubwa wakati wa kuchambua na kutoa maoni na ushauri wa kina uliowezesha kuboresha Muswada huu naomba niwatambue kwa majina. Mheshimiwa Omari S.Kwaangw' Mwenyekiti, pamoja na mimi mwenyewe Makamu Mwenyekiti, Dr. Haji Mwita Haji na wajumbe wengine wa kamati kama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. Hemed Mheshimiwa Phares K. Kabuye Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Sameer I. Lotto, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Omari A. Mzee, Mheshimiwa Khadija S. Ngozi, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Usi Amme Pandu, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, Mheshimiwa Mwanakhamisi K. Said na Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L. Foka na Ofisi yake kwa kutuhudumia vema kipindi chote cha Kamati ilipokuwa kazini. Pia nampongeza Katibu wa Kamati hii Ndugu Theonest Ruhilabake, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kutolewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni hayo naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Sekta ya Afya ambaye ni Dr. Ali Taarab Ali. (*Makofi*)

**MHE. DR. ALI TARAB ALI - (MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa maoni kuhusu Muswada wa Sheria wa Kusimamia Huduma ya Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona wa Mwaka 2007 (*The Optmetry Act* , 2007) kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni za 43(5)(b)(c) na 70(1) Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii pamoja na kazi yako kubwa ya kuweka Bunge lako katika hali ya kuwajibika kwa Watanzania. Aidha, nawapongeza Waziri na Naibu wake bila kuwasahau watendaji wote katika Wizara kwa kazi kubwa ya kufanikisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki, ikiwa nitawasahau wapiga kura wangu wa Jimbo la Konde, kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Vilevile naishukuru kambi ya Upinzani, chini ya viongozi wetu, Mheshimiwa Hamad Rashid, na Mheshimiwa Dr. Slaa, kwa kazi kubwa ya kutufanya tushiriki vyema hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa huzuni kubwa naomba kutoa salamu zangu za rambirambi kwa familia ya marehemu Dr. Aron Chiduo, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amina! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza, Kifungu cha 3 kinaongelea tafsiri ya maneno yaliyotumika kwenye Muswada, unaohusiana na Huduma ya Kurekebisha Upeo wa Macho kuona.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 2, Kifungu cha 4(1), kinaongelea kuanzishwa kwa Baraza ambalo litashughulikia watoa huduma wa kurekebisha upeo wa macho kuona. Kifungu cha 5(2) kinaelezea pia kazi na uwezo wa baraza hili, uteuzi wa msajili na kaimu wake na kifungu cha 7 kinaelezea kazi na uwezo wa baraza.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ingawaje haiongelei kuhusu taaluma ya kaimu msajili, Kambi ya Upinzani inaona ni muhimu kaimu huyu awe ni mtaalam wa fani ya kurekebisha upeo wa macho kuona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 4, kifungu cha 21(1), kinahusiana na kufutwa na kusimamishwa kwa muda kwa mhudumu wa kurekebisha upeo wa macho kuona. Aidha, sehemu hii kifungu cha 23 kinahusika pia na utaratibu wa kurejeshwa kwenye orodha kwa mhudumu aliyefutwa au kusimamishwa hapo mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa sehemu hii haikuweka bayana, utaratibu wa kuchukuliwa hatua hizi mbili. Hivyo, ni muhimu kwa mhudumu wa kurekebisha upeo wa macho kuona kwanza, kusimamishwa kwa muda kutoa huduma hizo. Muda huo usizidi miezi mitatu, na pindi mhudumu akishindwa kujirekebisha katika

kipindi hiki ndipo ifuate hatua ya pili ya kufutwa kutoka kwenye daftari la utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, aidha, kipengele cha 23(2), hakikueleza kwa makini utaratibu wa mhudumu kurejeshwa kwenye daftari la kutoa huduma. Kambi ya Upinzani inaona ni muhimu kwa mhudumu aliyefutwa kutoka kwenye daftari hapo mwanzoni mbali ya kufaulu mtihani au kutoa malipo yanayostahili, muhimu kwanza kuleta barua ya maombi kwenye baraza ndipo afikiriwe kuruhusiwa kutoa huduma upya.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 8, kifungu cha 36 kinahusu makosa na kifungu cha 37 adhabu wanayostahili wahudumu wa kurekebisha upeo wa macho kuona kwa makosa mbalimbali. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuongeza adhabu kwa mhudumu aliyesajiliwa kumruhusu mtu yeyote asiyesajiliwa kutoa huduma ya kurekebisha upeo wa macho kuona.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dk. Ali Tarab Ali, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Waheshimiwa Wabunge ninayo orodha ya wachangiaji watatu, nao ni Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa George Lubeleje, na Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, nitaanza kwa mpangili huo. Mheshimiwa Shellukindo hayupo kwa sasa, wala Mheshimiwa Lubeleje pia hayupo, aliyepo ni Mheshimiwa Idris Mtulia.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada uliopo mbele yetu. Hakika kabla sijaenda mbele niungane na Wabunge wenzangu kutoa rambirambi na pole nyingi kwa familia ya Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo. Dr. Chiduo, alikuwa Daktari bingwa na mshauri, na ni mmoja kati ya madaktari wakubwa wa nchi hii.

Baada ya hapo nilitaka nianze kusema tu kama ingekuwa hakuna magazeti, katuni za kipanya jana Serikali ilionyeshwa inatoa Muswada kwa Mheshimiwa Spika, na kisha ikajibiwa pale pale umeshapita! Hakika Muswada huu ulitakiwa upite tu bila hata mjadala, kwa sababu umeandikwa vizuri unahitajika na huduma zake ni muhimu. Lakini kuna pointi mbili tatu za kutia msisitizo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri pamoja na wataalam wote katika Wizara hiyo hususan wale wa idara ya macho. Kama inavyofahamika, mimi nimefanya kazi pale, lakini huyu Waziri wa sasa na watendaji wake amenipiku kweli kweli, hongera sana Mheshimiwa Waziri! Tumekaa pale miaka lakini hatukupata kuona umuhimu wa kubadilisha Sheria hii. Kwa hiyo, lazima tuna haki ya kumpongeza na kwamba aendelee na kama nilivyosema hapo awali kwa kweli huu Muswada ni huduma kwa watu na umekuja kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya upeo wa macho kuona ni mengi, watu wengi wanaathirika, lakini tofauti kubwa sana ni kwamba macho ni kiungo muhimu lakini

madaktari wanasema sio kiungo muhimu sana. Kama ingekuwa mtu anaumwa moyo, mapafu, maini au figo, mtazamo wake ungekuwa mwingine. Umuhimu wake wa kuchukua hatua za haraka ungekuwa mwingine, kuliko mtu ambaye kawaida ana afya nzuri ila hawezi kusoma tu, au ana afya nzuri kwa bahati mbaya kabisa haoni. Ndiyo maana labda Muswada huu umechelewa kuja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mimi ninazungumza kwa uchungu sana kwa sababu nilikuwa nimeanza kupewa miwani tangu 1960 nilipokuwa kidato cha kwanza. Kwa hiyo, kama huduma hii isingekuwapo nisingekuwa hapa nilipo sasa.

Naishukuru sana huduma hii. Nina hakika vilevile humu ndani ya Bunge zaidi ya asilimia 30 ya Waheshimiwa Wabunge wanaosoma Miswada hii wanawezeshwa na miwani waliyotoa wataalamu hawa ambao sheria yao leo tunataka kuipitisha. Kama ungefanya utafiti huko mjini ungeona kuwa kila mtu anajiona yupo mzima, lakini si kweli, kwa kuwa watu wengi hawasomi, wakianza kusoma wangejigundua wenyewe kwamba wanahitaji huduma hii mara moja.

Mheshimiwa Spika, lakini kilichonisimamisha, sio kusifu tu Muswada, ni kuwa nina hoja kubwa sana, nayo inatoka katika sera yenyewe ya Wizara ya Afya, kwamba Wizara itapeleka huduma zote mpaka vijijini. Kwa bahati mbaya kabisa, huduma za upeo wa macho kuona zipo mijini tu. Tena zinagongana, saa nyingine mtaa mmoja utakuta kuna ofisi kama tatu au nne au maduka matatu au manne yanauza, yanapima huduma hizi, na ukienda mikoani labda utapata bahati. Watu wa Dodoma naona wangeshukuru sana kwa sababu Hospitali ya Mvumi ni hospitali iliyopata sifa kubwa, na kwa bahati nzuri hata mimi mwenyewe nimeenda pale nimeikuta ile shughuli inayofanywa pale, huduma zake nzuri sana. Lakini huduma hizi zipo mijini tu, ninaloomba Mheshimiwa Waziri afanye utaratibu unaoeleweka kwa kufuata sera ya Wizara yake, kwamba sasa na sisi tunaokaa vijiji tupate huduma hii kwa njia rahisi. Kwa mfano, ipatikane kwanza katika Makao Makuu ya Wilaya na ikiwezekana hata katika zahanati zetu na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Spika, inawezekana na mimi najua hali ya Wizara na hali ya watumishi wake wachache. Lakini inawezekana kabisa kutunga ratiba, kwanza, kuigawa Tanzania katika kanda, halafu tukawa na watu ambao wanatungiwa ratiba ya kwenda katika vituo hivi, hasa vya Wilaya na vituo vya afya wakaenda wakavitembelea, kwa sababu hawa wagonjwa kwa kawaida wanajifanyia shughuli zao nyingi tu.

Mheshimiwa Spika, lakini wakielezwa kwamba mtapimwa macho siku kadhaa, tarehe kadhaa, vyombo vya habari vinazungumza, utakuta wangeweza kuonwa pale Utete – Rufiji, watu wakakusanyika wakapimwa. Hili si jambo jipya kwa sababu watu na vyama vya hiari wanaweka vitu vinaitwa kambi ya macho, watu hawa watiwe nguvu.

Waziri katika bajeti yake nitamwomba sana aongeze kwa makusudi kabisa kwamba safari hii tunavamia kutibu wagonjwa wa macho nchi nzima. Tunaanza na Wilaya, halafu tukitoka pale tunaenda katika Vituo vya Afya. Kama hilo halitawezekana

kwa mara moja, lakini mpango wa kufanya ziara, yaani wapimaji hawa wapite katika sehemu zilizo mbali na Makao Makuu ya nchi hii na Makao Makuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia na ninaomba sana Mheshimiwa Waziri achukue hii hoja ya kuwatibu wanavijiji na aitilie mkazo sana. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Prof. David H. Mwakyusa kwenye Muswada wake huu wa Sheria ya Kusimamia Huduma ya Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona wa mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni muhimu sana na umeletwa wakati mzuri. Mimi nasema hivi, kwa sababu kuna mambo ambayo yalitokea yanahusiana na Muswada huu na kwa bahati nzuri wakati yanatokea nilikuwa nao na nimesikia watu wanavyozungumza. Kwa hiyo, ni Muswada muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii huduma ilikuwepo, lakini sasa inapewa mwelekeo zaidi, mwelekeo mpya wa kitaaluma. Kwa hiyo, mimi naunga mkono sana mapendekezo yaliyoko katika Muswada huu.

Kwanza kabisa, napenda kuwashukuru madaktari wa macho wa *KCMC* pamoja na madaktari wa macho waliopo katika hospitali ya Mkoa ya Bombo. Mwezi Februari, 2007 wa Tanga kama alivyosema mwenzangu hapa Mheshimiwa Prof. Mtulia, walikuwa na utaratibu wa kuzungukia kwenye hospitali za Wilaya, kwa hiyo, walikuwa katika hospitali ya Wilaya ya Lushoto. Pale walifanya kazi nzuri sana. Sasa, mimi nasema Muswada huu umekuja wakati mzuri kwa sababu wakati huo wanafanya kazi, mimi nilikuwa na Muswada huu na nilikuwa nausoma kwa sababu nilikuwa na muda pale.

Kwa bahati nzuri mama yangu mzazi ana miaka 94, hakuwa mgonjwa, ni mmojawapo wa wazee ambao walikwenda kurekebishwa upeo wa macho wa kuona zaidi. Kwa hiyo, nilikaa siku nne pale, na nilipitia Muswada vizuri sana kwa sababu ulikuwa unafanyiwa kazi. Nilikuwa nauona pale, Madaktari wa macho wakifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza sana madaktari hawa kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kama mtu huelewi, unaweza usielewe umuhimu wa kazi hii ambayo inafanywa ya kurekebisha upeo wa macho, maana kuna hii ya kupimwa na kuvaa miwani, ni kitu tofauti na ya kurekebisha upeo wa macho. Kwa kweli hii, sidhani kama kuna *bonus* ya kuwapa wazee kama kuimarisha huduma hii ya kurekebisha upeo wa kuona.

Mheshimiwa Spika, nitapenda kuwataja wazee wangu wachache ambao walisema wao wenyewe kwamba kwa kweli huduma hii tunamuomba Mwenyezi Mungu aijalie Serikali ya Mheshimiwa Kikwete idumu, iendelee kuwahudumia: Akina Mzee Timothy Kibangu wa pale Bumbuli, Mzee Juma Hazari wa Soni na mama yangu mzazi ambaye tulikuwa tunamshika mkono, sasa anaweza kutazama hata *TV*. Muswada huu kwa kweli,

mimi umenitia moyo sana kwamba ni muhimu sana. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa na mwenzangu Mheshimiwa Prof. Mtulia kwamba huduma hii iimarishwe. Twende hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, najua Serikali inaweza isipate nafasi ya kwenda moja kwa moja vijijini. Lakini, katika kila Mkoa tuimarishe hii. Kwa mfano waliopo Tanga pale, inabidi washirikiane na waliopo *KCMC*. Sasa kuzungukia Kanda hiyo, inakuwa ni kazi. Lakini, ikiimarishwa hiyo, itakuwa ni nzuri. Na vile vile katika hospitali zetu za Wilaya tuweke nafasi kwa ajili ya wagonjwa hawa ambao wanakuja kwa muda.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwepo pale Lushoto kwa siku nne nikimngonjea mama yangu mzazi yupo pale mzee wa miaka 94. Kwanza hakuamini kwamba inaweza kufanyika hiyo na akasema yeye alikwenda tu kuondolewa machozi, haihitaji operesheni. Lakini, alipotoka alipofanyiwa jicho moja, akasema na hili la pili nataka nalo lifanyiwe. Sasa, watalifanyia mwezi Mei, 2007.

Hao madaktari wana mahitaji ya sasa hivi, waimarishwe hao kiusafiri, sio waje kwa basi kutoka Tanga. Kitengo hiki cha macho kipewe umuhimu sasa hivi ili wazee hawa kweli waweze kuishi maisha yao yaliyobaki vizuri zaidi bila kutegemea watu wengine. Kwa hiyo, mimi napenda kuwapongeza sana sana madaktari wale kuwa wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikuwa nimeona umuhimu wake, lakini nimeona umuhimu wake. Kwa hiyo, naunga mkono. Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake, mimi nitakuwa mmojawapo wa kuangalia kifungu hicho kwamba kinawekewa fedha ili upate nguvu ya kuweza kuhudumia wazee hawa pamoja na watu wengine ambao si wazee lakini ni vijana wanahitaji wasome na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Muswada wenyewe. Nina maoni tu kwenye baadhi ya vifungu. Kama nilivyosema Muswada huu nimeupitia sana, nitamwomba Mheshimiwa Prof. Mwakyusa wakati tunakwenda kwenye Kamati ya Bunge zima, aniwie radhi kuna maeneo mengine nitamsaidia, kwamba hapa nadhani pangekaa hivi, kwa sababu niliukalia kwa kweli vizuri sana, nilikuwa na muda wa kutosha na ndio uzuri wa Miswada hii kuipata mapema na tukawa na muda mzuri wa kuisoma.

Mheshimiwa Spika, katika Kifungu cha 18(3), pale panapoonyesha *enrolment*. Kuna ile sehemu tumeandika majina katika kujiorodhesha pale tumeandika majina, anwani, na kadhalika. Kwa sababu mle kwenye Muswada wenyewe mmetaja vile vile madaktari ambao si raia. Sasa, ninadhani kati ya lile neno *names and addresses*, tungeingiza *nationalities* ili tujihakikishie kwamba watu tunaowaandikisha, kuna Watanzania wangapi! Twende namna hiyo ili tuweze kujua kuna wageni wangapi na Watanzania wangapi katika ile *registration* kwa sababu nimeona kuna sehemu mmesema wageni vile vile watakuwa *registered*.

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani ni vizuri tukaweka hiyo ya *nationalities*, naomba aikubali hii iingie kwa sababu inaboresha zaidi. Halafu katika Kifungu cha 30(4),

pale ambapo tunazungumzia ukaguzi wa hesabu n.k. Nadhani pale ni vizuri kumtaja kabisa *Controller and Auditor General* kwa sababu fedha hizi zinatoka kwenye Bunge, yeye ndiye anatakiwa akague. Lakini uwezo wake na kazi yake sio kubwa kiutumishi, apewe madaraka na amekwishapewa katika baadhi ya sheria ya kumteua *Auditor* mwingine binafsi ili amsaidie kufanya kazi hiyo. Nadhani ni vizuri tukaiweka pale, isije akategemewa yeye peke yake. Kwenye fedha zinazotoka Bunge, moja kwa moja ni yeye anakagua, lakini kazi ni kubwa sana. Kwa hiyo, tumtaje pale, lakini aweze kuteua Mkaguzi yeyote ambaye atamsimamia yeye kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu kingine ni kile kifungu 42. Nadhani katika marekebisho mmesoma vile vile Jedwali la Marekebisho, nadhani itakuwa 42 ya zamani, lakini sasa hivi ni kifungu 43 kwa mujibu wa marekebisho katika jedwali. Pale, ule muda wa kushughulikia maombi katika muda wa siku 90, nadhani siku 90 ni nyingi sana kwa sababu ukiangalia hata taaluma yenyewe kwa kweli haina watu wengi. Mimi nafikiri tungeteremsha muda huo. Mimi nasema iwe haraka sana.

Lakini haraka sana wakati mwingine haikupi nafasi ya kuweza kusimamia vizuri. Tufanye siku 60, tusiweke muda mrefu sana, watu wasicheleweshwe sana. Kwa mfano, mtu anatoka nje, anakuja, anataka labda kwa muda afanye hiyo kazi. Sasa, *application* ikiwekwa kwa muda wa siku 90 anasubiri tu, nadhani tuseme si zaidi ya siku 90 na ikiwezekana iwe hata siku 14 ili tuweze kuwapa moyo wa kuweza kuhudumia vizuri.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Muswada huu kwa kweli ni muhimu sana, mimi naunga mkono. Kwa hiyo, naomba niishie hapa. Nakushukuru sana!

**SPIKA:** Mheshimiwa Shellukindo, ahsante sana! Sasa Msemaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa George M. Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia huu Muswada muhimu ambao umeletwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, tatizo la magonjwa au tatizo la wananchi wengi kutokuona ni tatizo kubwa na si la Mkoa wa Dodoma tu, lakini karibu maeneo mengi, kwa sababu kuna dhana potofu kwamba inawezekana tatizo hili lipo Mkoa wa Dodoma. Lakini kwa kweli lipo karibu nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, ni kwamba sheria hii ya mwaka 1965 inafutwa na kwa kweli na mimi nakubaliana naye kwamba imepitwa na wakati hasa ukiangalia hivi sasa tuna karne ya 21 ya sayansi na teknolojia kwa sababu hata vifaa vinavyotumika ni vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuna wataalam wachache sana wanaoshughulikia magonjwa ya macho *(Eye Specialists)* na tatizo hili kwa kuwa nimesema ni kubwa karibu nchi nzima, ninashauri basi ni vizuri katika kila hospitali ya Wilaya na Mkoa tuwe na wataalam wa kutosha kwa sababu hivi sasa tunategemea sana hospitali ya Mvumi

*Mission* pamoja na *KCMC*. Kwa hiyo, wagonjwa wengi tunawapeleka kule kwa ajili ya tiba na kwa ajili ya kurekebishwa ili waweze kuona mbali.

Mheshimiwa Spika, nina mapendekezo au naomba kusisitiza mambo yafuatayo pamoja na kwamba hii ni sheria mpya, ya zamani inafutwa, lakini kuna mambo ambayo yanafutwa na kuna mambo ya kusisitiza: Kwanza, ni kuhakikisha kwamba ni muhimu tuwe na sheria itakayodhibiti wanaouza miwani kiholela. Hivi sasa unakuta madukani mtu anauza miwani. Ukienda kutaka miwani ya jua, miwani ya kusomea, mtu anayenunua, hajapimwa na daktari.

Kwa hiyo, nashauri tuwe na sheria ambayo itadhibiti suala zima la uuzaji wa miwani katika maduka.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nasisitiza pia sheria itoe adhabu kali kwa wanaokiuka maadili na kuuza miwani kiholela, unapovaa miwani unaharibu macho, kwa hiyo, unashindwa kuona mbali. Kwa hiyo, nashauri kwamba kuwe na sheria ambayo itatoa adhabu kali kwa wale wote watakaohusika na kuuza miwani kiholela.

Mheshimiwa Spika, vile vile nasisitiza kwamba tuangalie vile vile mitaala. Kama nilivyosema hii ni karne ya 21 ya sayansi na teknoloji.

Kwa hiyo, mitaala katika vyuo vyetu mara kwa mara kuwe na marekebisho, kuwe na mabadiliko ili vijana wetu waweze kupata mafunzo ambayo ni ya kitaalamu zaidi ili waweze kutumia vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, jambo la nne ambalo napenda kusisitiza ni suala zima la sheria iweke utaratibu wa usajili. Usajili kwa sheria inayofutwa, waliokuwa wanatambulika ni wale tu wataalamu ambao wana shahada. Lakini, ninashauri sheria inayotungwa sasa iwatambue vile vile wataalamu ambao wana diploma na vyeti kwa sababu nao ni wataalamu wetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho kama nilivyosema, katika maeneo yetu au katika hospitali zetu, tunaomba vifaa vya kisasa na tunaomba wataalamu hawa wawepo kila hospitali ili wananchi wasiwe wanasafiri kwa muda mrefu kufuata wataalamu wa magonjwa ya macho hospitali ya Mvumi pamoja na *KCMC*.

Lakini Muswada huu ni mzuri, mimi nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Nawashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuupitishe ili uweze kuanza kufanya kazi. Baada ya kusema hayo machache, naomba kuunga mkono kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa Spika, ahsante sana! *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mara nyingine tena ili niweze kuhitimisha hoja yangu. Napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuzungumza. Nadhani wachangiaji walikuwa wachache, sisi tunachukua kama ni ishara kwamba huu Muswada umekubalika, lakini changamoto kwetu sasa ni kuutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kufanya masahihisho wakati namtambua Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, nilimtaja kama Mheshimiwa Omary Said Kwaangw', huyo ni mtu mwingine. Jina sahihi ni Mheshimiwa Omar Shaban Kwaangw'. Ningeomba wanaohusika na *Hansard* tusahihishe hilo.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji walikuwa tisa. Watano walipata nafasi ya kuzungumza na tumepata wanne ambao wametuletea mawazo yao kwa maandishi.

Naomba niwatambue wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni:- Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Makamu wa Mwenyekiti ambaye ametoa maelezo na maoni kutoka kwenye Kamati, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab, Msemaji wa Upinzani, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa William H. Shellukindo na Mheshimiwa George M. Lubeleje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mheshimiwa Rosemary Kirigini na Mheshimiwa Shari Raymond na vile vile Mheshimiwa Susan Lyimo ametuletea mchango wake kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nafarijika kwamba wote waliochangia, wameunga mkono hoja yangu, nawashukuru sana. Nipitie tu mambo machache yaliyojitokeza ambayo yanahitaji ufafanuzi. Mambo mengi ilikuwa msisitizo wa mambo ambayo yamejitokeza katika Muswada kama ulivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetushauri tuweke fedha za kutosha ili chombo hiki kiwezwe kufanya kazi na nashukuru Wabunge waliochangia wakasema nitakapoleta bajeti yangu watakuwa mstari wa mbele kuweza kunisaidia kuipitisha. Nashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, kumejitokeza suala la kuwaendeleza wafanyakazi kwa maana kwamba wanapohitimu, kuwe na kujiendeleza. Hii imejitokeza katika taaluma mbali mbali hasa wataalamu wanapokwenda maeneo ambayo hayana intaneti, hawachanganyikani na watu, basi inakuwa mambo waliyojifunza miaka 20 yanakuwa ni yale yale.

Mheshimiwa Spika, napenda nilichukue hili wazo na nadhani tulichukue kijumla kwa taaluma zote. Tuliangalie leo tunazungumzia hawa watu wa macho, lakini kutakuwa na watu wengine wa afya, watu wengine wa *X-ray* na watu mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, ni wazo zuri ambalo kama serikali tutalichukua kwa mapana yake ili iwe ni lazima kwamba kila mtu aonyeshe kwamba amejiendeleza kwa kila namna itakavyokuwa, itabidi tufuate utaratibu wa watu wengine wanafanyaje.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la *code of conduct,* kwamba kuwe na *code of conduct* na hiyo kuna kipengele ambacho kinasema kwamba: *"The Minister may after*

*cosultation with the council, prescribe the code of conduct and ethics to be observed by Optimetrits and Otharamic Opticians"*.

Kwa hiyo, hili niseme limekwishafikiriwa, hatuwezi kuliweka kwenye sheria, lakini itakuja kwenye kanuni ambazo Mheshimiwa Waziri atakuwa amepewa nguvu ya kuzitengeneza. Wengi wamezungumzia habari za viwango vya adhabu kwamba ni vidogo kwa sababu watu watakaokiuka maagizo yaliyomo kwenye sheria ni watu ambao watakuwa wanaathiri afya za watu, kwa hiyo viwango vya adhabu, niseme tu kwamba tutaviangalia na suala la *optometry* kama ilivyojitokeza kwenye ripoti ya Kamati, hilo limekwishashughulikiwa katika jedwali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Ali Taarab, amependekeza kwamba taaluma ya Naibu Msajili iwe taaluma ya *Optimetrist*, hiyo hatuna shida nayo, tutaingiza kwenye sheria na vile vile kwamba suala la kufutwa na kurejeshwa katika daftari ni suala ambalo haliko wazi. Lakini ukiangalia katika jedwali la marekebisho tumeliweka hilo kwa sababu tulilizungumza wakati wa Kamati na wote tulikubaliana kwamba ni kitu cha muhimu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia amezuingumzia zaidi kuhusu sera ya kupeleka huduma karibu na wananchi. Hilo tunakubaliana nalo kabisa na mtakuwa mashahidi kwamba kwa upande wa macho, tumekuwa na wafadhili wengi ambao Serikali tunatoa wataalam tu kuambatana na hao wafadhili kama *Rotary Club, World Vision, Lions Club* na hawa *Vision 2020* ambao wanaweka makambi maeneo mbali mbali.

Nadhani kinachokosekana hapa, ni kwamba labda tuwe karibu zaidi nao kuratibu kwa maana kwamba tuwaambie waende kwenye maeneo ambayo yapo pembezoni zaidi. Mheshimiwa William H. Shellukindo, pia hili alilizungumzia na sisi tunalichukua katika utekelezaji wa hii sheria, tutalifanyia mkakati. Lakini kwa ujumla, nadhani tunaelewa kwamba idadi ya wafanyakazi wetu ni ndogo. Mheshimiwa George Malima Lubeleje alisema kwamba ni wachache, kweli ni ndogo. Lakini si hawa tu, hata wataalam mabingwa katika maeneo mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu ambao tunapenda tujipange vizuri kwa maana hawa wataalamu wachache tulionao waweze kuwafikia watu wengi zaidi. Tuna *outreach programs*, kwa mfano, kwa upande wa hospitali za Rufaa, tumezigawa katika Kanda. Bugando inaangalia Kanda ya Ziwa, *KCMC* - Kanda ya Kati mpaka Tanga, Muhimbili – Kanda ya Kusini na Mashariki, ambapo Mbeya inaangalia Kanda ya Nyanda za Juu. Wanachofanya ni kujipanga na kupeleka taarifa katika hospitali zinazohusika, wanakwenda kama timu. Kwa mfano anaweza akawepo daktari wa macho, daktari wa magonjwa ya akina mama, madaktari wa *internal medicine*, basi kule wanakokwenda wanakuta wagonjwa ambao madaktari wa kule wanataka kupata utaalamu zaidi basi wanawakuta wapo tayari.

Kwa hiyo, watakaa kule siku moja, siku mbili, wanafanya oparesheni halafu wanarudi. Huo ni utaratibu ambao upo kwa muda mrefu na katika sera yetu ni kwamba

tumeelekeza vile vile kwamba Mikoa na Wilaya na zenyewe zifanye hivyo hivyo. Kwa hiyo, nadhani kinachokosekana hapa ni usimamizi kwa sababu sera ipo wazi kuhusu suala hilo. Hivyo, kwa vile tunazungumzia habari za macho pia tutaweka msisitizo kwamba suala hili nalo tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa William H. Shellukindo amesema kwamba kutakuwa na haja ya kuweka suala la uzalendo, tutalizingatia hilo, na akaongeza kwamba mkaguzi atajwe. Sheria inayohusu *Auditing*, inatamka wazi kwamba pesa zote za Serikali kwa maana ya Wizara na Idara za Serikali, *Auditor* ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Sasa, hatuoni kwamba kutakuwa na ulazima. Kwa sababu katika sheria hiyo imetamka wazi, hii itakuwa kama tunaweka *exception*. Lakini, ni kweli *Auditor* ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na ndiye atakayekagua na akiona ni vema, basi anaweza akamteua mwingine.

Mheshimiwa Spika, suala la muda wa kushughulikia, hili sijui kama limejitokeza kwenye jedwali, lakini tulilizungumza sana kwenye Kamati na kweli tulisema kwamba tupunguze muda uwe siku 60 na nikumbushe tu kwamba mwenye mamlaka ya mwisho kupitisha nani asajiliwe, nani aendeshe hizi shughuli, ni Baraza.

Sasa, Baraza siyo tendaji kwa maana lipo kila wakati. Kwa hiyo, itabidi tulenge vikao, huo muda usiwe mfupi mno, vinginevyo wataona wanachelewa mno, walipelekwa tuliwaambia siku 15, lakini hawapati majibu. Kwa hiyo, hilo la kupunguza muda mpaka 60, ni jambo ambalo tulikubaliana nalo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa George Malima Lubeleje aliwekea msisitizo tu kwamba tuwe wakali kwa watu wanaouza miwani holela na pia suala la adhabu kali tumelizungumza na mitaala iangaliwe upya. Mitaala imeangaliwa upya, zamani walikuwa wanafuzu kama *Opticians*, sasa hivi kutokana na mabadiliko ya mitaala wanatoka kama *Optimetrists*. Lakini mitaala kama mnavyojua siyo kitu cha kudumu, kila wakati lazima kupitia.

Vile vile alisema usajili uwe wa watu wengi zaidi kwa maana ya ngazi za taaluma na ndivyo ilivyo, hata ukiangalia kwenye *application* ya sheria, inazungumzia habari za *Otharamic Opticians* pamoja na *Optimetrists* ambao ni ngazi tofauti. Madaktari yaani *Othamologists*, hawamo katika sheria hii, wana sheria tofauti. Na amesisitiza kwamba pia tuangalie suala la vifaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, amependekeza kwamba katika sheria tuandike kwamba huyu mtu anayeomba aandike refarii wake na Wasifu ili tuweze kujua ni mtu wa namna gani. Sasa nadhani huo ni utekelezaji. Hatuwezi tukaandika kwenye sheria, lakini tutazingatia wakati tunawasaili hawa watu. Vile vile kuna masuala ya uhariri ambayo tumeyasahihisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Siyame na Mheshimiwa Kirigini, wote wameunga mkono na kutupongeza, nashukuru sana, na kuweka misisitizo katika mambo

ambayo tumekwishayazungumza. Tutambue tu kwamba Mheshimiwa Dr. Luka Siyame yeye ni Daktari Bingwa wa macho, lakini mwanafunzi wangu.

Kwa hiyo, alishindwa kujizuia kuchangia, lakini kusema kweli anasema hii hoja imechelewa na anaiunga mkono na kwamba kwa sababu ni Serikali moja, tutasaidiana katika kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwashukuru wote ambao wamechangia na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kusimamia Huduma ya Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona wa Mwaka 2007*(The Optometry Bill, 2007)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 3

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nilisema Muswada huu nimeupitia kwa kina sana.

Naomba Waziri akubaliane na mimi pale kwenye *interpretation,* ibara hii kifungu cha 3 pale kwenye *license* nadhani kwa *interpretation* ya 1, 2, 3, 4, 5, 6, 7, inayosema *license means a permit to authorizing the holder to, should be practice* pale imetumika *noun "practice"* haya maneno yana matatizo sana *practise and practice* nadhani tukubaliane hiyo ni kuimarisha hii *bill* tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Spika, ni mtaalamu wa Kiingereza, lile neno lililopo *practice* ni sahihi kabisa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 5

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa uliyofanya. Katika kifungu cha 5(2)(c) nilitaka tu tukubaliane maana yake kuna shule nyingi, kuna *license* kwa maana ile *document* inaandikwa '*ce'* kuna wengine wanaandika '*se.'* Sisi nadhani kwa Kiingereza cha Kiingereza ni *"c" license*. Hapo nadhani tutakubaliana, halafu tukiendelea kwenye kifungu (e) kwa sababu pale juu tumesema *shall be to a device* na siyo *to advice*. Nadhani hapo tutakubaliana na wewe hapo.

**MWENYEKITI:** Kwanza nakupongeza Mheshimiwa William Shellukindo, umeusoma kwa makini sana huu Muswada kiasi kwamba unaona mpaka *spelling errors,* kwa hiyo, neno hili litarekebishwa tu, Waziri huna haja ya kujibu *license is 'c' note 's'* na pia *to advise* haiwezi kuwa *to advice*.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, wakati tunachambua Muswada huu kwenye Kamati tuliongea sana suala la ibara hii ya tano kwamba hili Baraza lisijihusishe na masuala ya *business* au *raising of funds* ile *(l) (m) and (o),* tuliongea sana na Mheshimiwa Waziri alisema atalichukua lakini naona bado liko vile vile. Sasa nilikuwa naomba ufafanuzi imekuaje. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Rudia vipengele hivyo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *(l), (m) and (o).*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, (i) inasema *establish committees, approve names of proposed committees Members and prescribe their functions.*

**MWENYEKITI:** Naona hakika haihusiki hiyo.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani ni *(l) (m) and (o)*.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni utaratibu wa kawaida kwamba fedha zinazotumika katika Baraza kwa mfano, wanaozisimamia ni *council*. Kwa hii haina maana kwamba wao wanaelekeza mtendaji wake mkuu ambaye ni msajili ili afanye hiyo kazi, *by the end* ambaye yuko *responsible* ni *council* ambao wanaleta hata haya mahesabu hata Bungeni. Ni kweli tulilizungumza halafu tulipopata ushauri wa kisheria ndio tukaambiwa kwamba hiyo ni *standard*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Isitoshe ku-*raise funds* Mheshimiwa Susan Lyimo, maana yake siyo kufanya biashara. *You can raise funds* bila kufanya biashara. Kwa hiyo, sijaelewa mantiki yako kuhusu kuizuia hii Halmashauri/taasisi kufanya biashara. Mimi

sidhani kama inafanya biashara. Lakini itapokea *funds* kwa namna nyingi ruzuku na kadhalika.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru lakini tukiangalie ile *(m) and (o)* ambayo hajaizungumzia, unaona kabisa kwamba kwa mfano (m) inazungumzia *prescribe modalities for the acquisition and upkeep of the council's properties and assets.* Lakini ile (o) inaongelea kabisa *authorize and supervise all activities related to vision testing and distribution of optical appliances.* Kwa hiyo, ina maana watu wote watakaokuwa wanashughulikia suala la miwani itabidi waende kwenye hii *council,* hivyo, tunaona kwamba kutakuwa na usumbufu. Lakini pia kuna *provision* ya *financial part 6* ambayo nadhani ilipaswa hizi shughuli zote ziende kwenye *financial provisions*.

**MWENYEKITI:** Waziri unapenda ku-*comment* hapo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la pili hatuna matatizo kulihamisha liende kwenye *section* inayohusika. Lakini hii namba (o), hapana!

**MWENYEKITI:** Hoja ya Mheshimiwa Suzan Lyimo, ni kwamba ikikaa hivyo ilivyo ina maana hata yeyote anayetaka kupimwa miwani itambidi apate idhini ya Baraza ndivyo anavyoisoma, kwamba kabla hata hujaenda kwa mtaalamu unapata idhini ya Baraza.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tungeichukulia tu kama sheria.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali anataka kusaidia.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sioni kwamba kuna haja ya kuhamisha chochote kilichopo kwenye vifungu hivi vya hii ibara ya 5 kwa sababu mimi ninavyoielewa inasema; *"Authorize and supervise all activities related to vision testing and distribution." To authorize and supervise* kusimamia siyo lazima mtu akitaka kupima lazima aende kwenye *council,* atakwenda kwenye wale wanaohusika lakini hawa ndiyo wasimamizi wakuu wa hiyo shughuli. Mimi sioni kwamba kuna tatizo lolote kwenye hiki kifungu.

**MWENYEKITI:** Nina matatizo hata mimi nadhani hivi *supervise* haitoshi, mpaka *authorize* inakuwaje tena. *To authorize all,* hasa ukija kwamba tena inasema *all activities related to vision testing.* Sasa sijui.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba wao ndiyo wana-*control,* wao ndiyo wanasimamia zoezi zima hili, ndiyo kazi ya hiyo *council,* ni *functions and powers, council*. Mimi sioni kama kuna matatizo.

**MWENYEKITI:** Tunawezaje kufanya, hapa namwelewa Mheshimiwa Suzan Lyimo, nakuelewa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tufanyeje ili isije ile sura kwamba Baraza hili siyo tu linasimamia sera na uendeshaji kwa ujumla, lakini linasimamia *all activities of the nature,* nadhani kuna kazi hapa *AG* ya kufanya. *You can't supervise all activities* na *even to authorize*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hili tunaweza kuliangalia tena, hili tatizo. Lakini mimi nilikuwa naangalia ile *sub- clause (1)* ilikuwa inasema; "*The council shall be the sole authority for registering and enrolling,"* hiyo ni mojawapo. Sasa kwa hiyo shughuli ni kusimamia mambo yote haya yanayohusiana na hizo shughuli za hao watu, hiyo ikiwa moja ambayo nimezungumzia. Lakini kama inaonekana kama haileti vizuri tutaangalia.

**MWENYEKITI:** Kama tulivyofanya jana kuhusu masuala ya rushwa Mwandishi Mkuu wa Sheria aangalie ili *final observation* isilete mkanganyiko. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 7

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyosema Muswada huu ni wa Waziri, lakini ukitoka hapo ukiwa sheria ni wa Bunge kwa hiyo, na sisi tuna mchango wetu. Katika ibara ya 7(4)(f) pale inaposema; *"to record all minutes of the council,"* nadhani *the minutes* ni *outcome* ya *record*. Kwa hiyo, nadhani tungesema pale *proceedings or transactions*. Sijui kama mmepata mantiki yake?

**MWENYEKITI:** Hebu rudia Mheshimiwa William Shellukindo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imeandikwa *to record all minutes,* sasa *minutes* ndiyo *record* yenyewe, nadhani *to record all transactions and proceedings* halafu *minutes* ije hapo kwenye *to keep properly* a*ll minutes, records and documents.*

**MWENYEKITI:** Lakini kwa uzoefu tuliouona hii ndiyo lugha kabisa wanayotumia karibu kila Muswada wanapotaka kuelezea kazi za msajili. Wanaandika kurikodi *minutes* nadhani ni *special usage* tuikubali tu Kibunge.

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 8

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hicho cha 8(1) tulikuwa tumesema kwamba *Deputy Registrar* lazima awe pia *optometrists* yaani awe na taaluma ya upeo wa macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sijamsikia Mheshimiwa Waziri akizungumzia hilo kwa sababu tunajua kwamba yule msajili asipokuwepo Naibu wake ndiyo wanachukua madaraka yale. Sasa kama naye hayupo kwenye hiyo taaluma tunaona mambo yasiende vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema hakusikia, ni kweli hakusikia kwa sababu alikuwa ametoka nadhani. Kwa sababu hii hoja imeletwa na Wapinzani na tumeikubali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, ina-*read* vipi sasa maana yake sasa tunapitisha kifungu, wapi inataja *qualification* kwa sababu inavyosimama hivi haina sifa, huyu *Deputy Registrar*? *AG* utusaidie basi ili wote wawili wawe na sifa za kuwa *optometrists*. Msajili na Naibu wake.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda *there shall be a Deputy Registrar who shall be appointed by the Minister and who shall be optometrist to assist the registrar.*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu sawa? Ahsante sana. Kwa kweli tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kusoma kwa makini sana Miswada hii.

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 9

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 10

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mchango wangu nilikuwa nimemshauri Waziri kwamba kwa kuwa kuna wageni wataandikishwa lakini tumia kifungu cha 18, lakini iliyozungumzwa inahusu kifungu cha 10(2) kinachosema; *"The Register shall contain the names,"* sasa nilitoa pendekezo kwamba ingekuwa *and nationalities, addresses and qualification*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, uki-*apply* kwenye kifungu hicho cha 10 na kile cha 18 ambacho kinahusu *environment*. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa William Shellukindo, wakati anachangia alizungumzia habari za tuwe

na *nationality* ya watu husika, lakini wao wana kifungu chao cha 20 ambacho kinazungumzia namna wanavyoweza wakaingia katika soko letu la mtoa huduma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa William Shellukindo, utaona kile kifungu cha 20 kinasema kwamba hawa siyo raia *in fact* kwamba watapata tu *temporary enrolment to start with,* kwa hiyo, naona inawatenganisha hasa toka mwanzo. Hawawezi kupata *permanent registration* lazima waanzie *temporary enrolment* kwenye 20. Mimi naona inatosheleza kabisa hii. Hiyo inatoa nafasi ina maana Serikali hapo ina maana kwamba wachunguzwe hawa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 11

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kifungu cha 11 pale kwenye *qualifications (a)* nilitaka tu tubadilishe pale ile sentensi inayosema *undergone* ukiendelea mpaka kwenye *diploma* halafu inafuata siyo *advance diploma* ni *advanced.*

**MWENYEKITI:** Ni kweli kabisa nakubali. Inaelekea Mheshimiwa William Shellukindo, anatumia *optometrists* mzuri sana katika shughuli zake. Tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 12

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ushauri wangu nilisema kwamba mtu huyu anaye-*submit application for registration* ni vema akai-*include CV* au *curriculum vitae* ili isaidie kuweza kutambua *experience* na uzoefu wake katika kazi hiyo kitu ambacho sikukiona kwenye Muswada huu.

**MWENYEKITI:** Nadhani kitakuwa *covered* kwenye *subsidiary legislation,* kwa sababu inatosha *such other documents* ukiisoma ile Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, 12 (2)(c) *such other documents containing information as may be required by the Council*. Inaweza kuwa nzuri zaidi kwa sababu inaruhusu sasa kwenye *regulations* atakazotunga Waziri aongeze siyo *CV* tu pengine na mengine zaidi. Tuiache zaidi hivyo. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila na mabadiliko yoyote)*

Kifungu 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 15

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 16

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17
Kifungu cha 18

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 19

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 20

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 20 (3) ule ukurasa wa 15 pale palipoandikwa *a person temporary enrolled* nadhani *temporarily,* nadhani hata Waziri katika ile Ibara ya 17 (3) amesahihisha pale, *a person temporarily registered.*

**MWENYEKITI:** Ni kweli kabisa, naona *AG* anakubali pale.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni marekebisho madogo tu kwenye hicho kifungu cha 21(b) kinachosema; *"direct the registrar to,"* basi yale yanayofuata tena yasiwe na *to* iwe ni *notify remove otherwise* ingekuwa *registrar to notify.*

**MWENYEKITI:** Ni kweli hayo yanajirudia hapo. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 37

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 38

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 39

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 39 (2) chenye (a) sijafanya marekebisho ya hizi namba lakini kinachoanza na *manufactures, distributes and supplies optometry appliances which does not,* nadhani ile ni *do*.

**MWENYEKITI:** Nadhani ile ni kweli. Waziri nadhani *which do not meet the councils* kwa sababu ni wingi.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kifungu hicho cha 39 ni kwamba katika Kamati tulifikiri kwamba kama *institution* imefanya makosa pia nayo iwe pia na kifungu kwa sababu pale tunaona hakuna kifungu, wamepewa tu faini. Je, akishindwa kulipa faini inakuwaje? Kwa hiyo, tulikuwa tumeongea na tulikubaliana hivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mimi napenda kujua ninyi wawili Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Suzan Lyimo jana mlikaa pamoja kujadili hili au?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Nilikuwa kwenye msiba. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Naona unajibu haraka haraka kwa sababu Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, yuko hapa siyo? Waziri kuna ufafanuzi hapo? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hili nilizungumzia wakati nahitimisha hoja kwamba tulikuwa tumetoa adhabu inayofanana kwa mtu anayekiuka sheria na pia *institution* na kwamba *to separate* hiyo na hili tumesema tutaliangalia litakuwa *separate*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tumepata faida ya wenzetu waliosoma kwa makini Muswada kwa hiyo, itatenganishwa hapo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 49
Kifungu cha 50

*(Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*
*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kusimamia huduma ya Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona wa mwaka 2007 *(The Optometry Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge, imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Optometry Bill, 2007* pamoja na marekebisho yake kifungu hadi kifungu na kuubali. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Optometry Act, 2007* sasa ukubaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii ni ya kukubalika kwa Muswada wa Kusimamia Huduma ya Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona wa mwaka 2007 yaani *Optometry Bill 2007*. Hoja ameitoa Mheshimiwa Waziri na imeungwa mkono. Ahsante sana. Kazi hii tumeshaimaliza ya Muswada huu, sasa ninayo matangazo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu amemteua Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo akaimu Shughuli za Serikali Bungeni kwa sababu yeye amekwenda kwenye shughuli nyingine na atakuwa nje ya Dodoma hadi hapo kesho. Kwa niaba yenu nina hakika tutapenda tumpongeze sana Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, hii ni ishara nzuri na Spika anamuombea dua katika hilo.

Nakumbusha tena kwamba Kamati ya Uongozi saa 7.30 mchana, tukutana ofisini kwa Spika. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe.Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na *Order Paper* ya leo kwa hiyo, tujiweke tayari kwa shughuli yetu ya mchana.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Mambo ya Nje

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati mbili ziliweka hoja zao mbele ya meza ya Spika leo asubuhi na sasa tutatoa nafasi kwa taarifa za Kamati hizo ziweze kusomwa mbele ya Bunge na baada ya hapo tufuate utaratibu unaotakiwa wa kuzijadili. Tunazo Kamati mbili, tutaanza kwa kuwaita Wenyeviti wa Kamati waweze kusoma hoja zao na baada ya hapo wasemaji wa Upinzani na wao watatoa maoni yao na baadaye mjadala wa jumla na baada ya hapo watoa hoja watahitimiza hoja walizoziweka mezani kwa Spika. Naomba kama kuna anayetaka kuchangia hoja hizo basi anaweza kuleta jina lake hapa mbele ili tuweze kuendelea na utaratibu. Kwa hiyo, baada ya kusema maneno hayo nitaomba niwape taarifa, tutaanza na uwasilishaji kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, halafu Msemaji wa Kambi ya Upinzani baada ya hapo nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje na baadaye Msemaji wa Kambi ya Upinzani na ndipo tutakapopata muda wa Waheshimiwa Wabunge wote kuchangia hizo hizo. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kwa niaba ya Kamati na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo langu na kwa niaba yangu mwenyewe niungane na Wabunge wenzangu kutoa salaam za rambirambi kwa ndugu, jamaa na wananchi wa Kilosa kwa msiba uliotupata wa kifo cha Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho ya Marehemu. *Amin!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa niaba ya Kamati hiyo naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa mujibu wa Kanuni ya 88(11) Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004. Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ni kama ifuatavyo:-

Mwenyekiti wetu ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, ni Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Fatma

Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Said Mohamed, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na mimi ninayewasomea taarifa hii naitwa Charles Keenja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala yameainishwa chini ya Kanuni ya 93. Kutokana na mabadiliko ya Wizara yaliyofanyika katika Awamu ya Nne, Kamati imepewa majukumu yafuatayo:-

Kwanza kushughulikia Bajeti za Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Siasa na Uhusiano wa Jamii, Ofisi ya Makamu wa Rais, masuala ya Muungano na Wizara ya Katiba na Sheria. Shughuli ya pili, ni kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo inatokana na Ofisi na Wizara hizo.

Ya tatu, ni kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Ofisi na Wizara hizo, ya nne, ni kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa ibara ya 63(iii) sehemu (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inaeleza kazi zilizofanywa na Kamati kwa kipindi cha mwaka 2006. Aidha, Kamati inatoa maoni na mapendekezo kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kama yalivyofanunuliwa katika Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwezi Januari hadi Desemba, 2006 Kamati ilifanya shughuli nyingi zikiwemo semina, ziara na uchambuzi wa Miswada ya Sheria. Kwa upande wa semina na mafunzo, mara tu baada ya kuwateua Wajumbe wa Kamati hii Ofisi yako iliandaa Semina ya Wabunge wote iliyofanyika katika Jengo la *Ubungo Plazza,* lililopo kwenye Jimbo la Ubungo Jijini Dar es Salaam. Katika semina hiyo, mada kadhaa zilitolewa zikiwa na lengo la kuwaelimisha Waheshimiwa Wabunge juu kazi za Bunge, stahili zao, kazi na mambo mengine yaliyohusika. Aidha, mara baada ya semina hiyo, Kamati ilifanya uchaguzi wa viongozi wake ambapo Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa alichaguliwa kuwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Tatu Ntimizi, alichaguliwa kuwa Makamu wake. *(Makofi)*

Baada ya uchaguzi huo Kamati ilipata fursa ya kujifunza historia fupi ya iliyokuwa Kamati ya Mambo ya Katiba na Sheria ilipobadilishwa na kuitwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala katika marekebisho ya kanuni za Bunge yaliyofanyika mwaka 2003. Mada iliyotolewa ilijulikana kama Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Uzoefu hadi 2005 na iliwasilishwa na Sekretarieti ya Kamati tarehe 2 Februari, 2006.

Katika kipindi hiki Kamati ilishiriki katika semina ya siku moja iliyoandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na semina hii ilifanyika Dar es Salaam tarehe 22 Mei, 2006. Katika semina hiyo, Kamati ilijifunza juu ya haki za binadamu nchini Tanzania na juu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na watu. Semina hiyo iliongeza uelewa wa Kamati kuhusu maeneo hayo na napenda kuchukua nafasi hii

kumpongeza na kumshukuru Bi. Hellen Kijo Bisimba, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, kwa kutuandalia semina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo mengine ambayo Kamati yangu ilihudhuria ni Warsha ya Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania inayojulikana kwa kifupi kama SHIMVYAWATA iliyofanyika Dodoma wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge la Bajeti ambayo ilihusisha pia Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii. Aidha, tarehe 21 Julai, 2006 Kamati ilishiriki katika majadiliano *(dialogue)* na asasi isiyo ya kiserikali inayojulikana kwa jina Ondoa Umaskini Tanzania kwa kushirikiana na Kamati ya Huduma za Jamii.

Napenda kuwapongeza wote walioandaa mafunzo haya ambayo yameisaidia sana Kamati yangu kuelewa vizuri masuala yanayohusu walemavu na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Kamati ilipelekewa na kufikiria Miswada minne na kuwasilisha maoni na ushauri wake Bungeni. Miswada hiyo ni: kwanza, Muswada wa Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa ya mwaka 2006 *(The National Leaders Funerals Bill, 2006).* Muswada wa pili, ni Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa, wa mwaka 2006 *(The Local Authorities Pensions Fund Bill, 2006),* Muswada wa tatu, ni Muswada wa Sheria, Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa mwaka 2006 *(The Written Laws (Miscelleneous Amendments) Bill, 2006)* na Muswada wa nne na wa mwisho ulikuwa ni Muswada wa Marekebisho katika Sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa 2006 *(The Local Government (Miscelleneous Amendments) Bill, 2006).*

Aidha, kwa kushirikiana na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Kamati yangu ilishiriki katika mazungumzo ya pamoja *(briefing)* kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Nyongeza wa Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu *(The Protocol to the African Charter on Human and Peoples' Rights on the Establishment of an African Court on Human and Peoples' Rights).* Mazungumzo haya yalifanyika Dodoma na kuwasilishwa na Mheshimiwa Dr. Cyril Chami, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kwamba wengi wa Wajumbe walikuwa wapya, hivyo kutokuelewa vizuri na kwa kina uhusiano uliopo kati ya Kamati na asasi zinazoainishwa katika Kanuni ya 93, tarehe 14 hadi 24 Machi, 2006 Kamati ilifanya ziara fupi katika Jiji la Dar es Salaam kutembelea Mfuko wa Akiba wa Serikali za Mitaa yaani *LAPF,* Asasi inayojitegemea na iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Kabidhi Wasii Mkuu, Chuo cha Utumishi wa Umma, Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania *(TACAIDS),* Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha tarehe 5 Aprili, 2006 Kamati ilitembelea Ofisi za Waziri Mkuu zilizopo Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hiyo ilikuwa na manufaa makubwa sana kwani iliwezesha Wajumbe kujifunza masuala mbalimbali yanayohusiana na utendaji wa kazi za Kamati unaofanywa na vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 23 hadi 26 Kamati ilifanya ziara fupi kutembelea Visiwa vya Unguja na Pemba na Mkoa wa Tanga kwa ajili ya kukagua miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii yaani *TASAF.* Kamati ilijigawa katika sehemu mbili, sehemu moja ikatembelea Zanzibar na sehemu nyingine ilikwenda Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hii Kamati ilijionea miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya maji, shule na hospitali iliyotekelezwa na wananchi kwa kushirikiana na *TASAF.* Kwa upande wa Zanzibar Kamati ilifurahishwa sana kwa jinsi wananchi wa visiwa hivyo walivyoonyesha mshikamano kwenye masuala yanayohusu maendeleo bila kujali tofauti zao za itikadi za kisiasa. *(Makofi)*

Aidha, Kamati imejionea hatua mbalimbali zilizofikiwa za miradi ya aina hiyo Mkoani Tanga na kuridhishwa kwa kiasi kikubwa na jukumu la *TASAF* la kuwa kichocheo cha moyo wa kujitolea na kujitegemea miongoni mwa wananchi. Hii inajidhihirisha kwa jinsi wananchi walivyochangia nguvu na rasilimali zao katika miradi iliyochangiwa na *TASAF.*

Pamoja na mafanikio hayo Kamati imejionea upungufu wa wataalamu wa afya katika baadhi ya zahanati zilizojengwa kwa nguvu za wananchi, kwa sababu hiyo, Kamati imezishauri Mamlaka zinazohusika ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutatua tatizo hili. Aidha, Kamati imeshauri kuwa elimu zaidi itolewe kwa wananchi vijijini ili waweze kuibua miradi mingi zaidi itakayowaendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ziara ya Kamati katika Manispaa ya Dodoma na Wilaya za Mpwapwa na Kongwa, tarehe 9 Agosti, 2006 Kamati ilitembelea Mahakama ya Mwanzo ya Makole iliyopo katika Manispaa ya Dodoma na Mahakama za Wilaya za Mpwapwa na Kongwa pamoja na Ofisi za Wakuu wa Wilaya hizo. Lengo la ziara hii ilikuwa ni kukagua majengo ya Mahakama hizo na Ofisi za Wakuu wa Wilaya kufuatia maagizo yaliyokuwa yametolewa na Kamati mwaka 2004 ilipofanya ziara katika sehemu hizo. Kamati imeridhika sana na kazi iliyofanywa na kushauri kuwa Mahakama nyingine nchini nazo zifanye ukarabati ili kuinua hadhi ya mahakama hizo.

Kuhusu uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya Wizara, Kamati yangu ilitekeleza kazi ya kuchambua makadirio ya matumizi ya Wizara katika Ofisi Ndogo ya Bunge iliyopo Dar es Salaam mnamo mwezi wa Mei na Juni, 2006 kwa kuchambua makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Siasa na Uhusiano wa Kijamii, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Wizara ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilipokea maelezo kutoka kwa Mawaziri wanaohusika na kutaka ufafanuzi katika baadhi ya maeneo. Baada ya kuridhika na ufafanuzi uliotolewa Kamati ilipitisha makadirio ya Wizara zote na

kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu na kuliomba Bunge liyapitishe makadirio ya Wizara hizo katika Mkutano wa nne wa Bunge lako Tukufu.

Baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe kuwa Shirika la Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa linapanua wigo wa wanachama wake kuwahusisha pia na sekta zisizo rasmi na hata watu binafsi wakiwemo Madiwani. Pili, Serikali ijitahidi kuhakikisha kuwa jengo la Ofisi na viwanda vya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali vinakarabatiwa ili viendane na teknolojia ya kisasa ikizingatiwa kuwa majengo mengi yanayotumika sasa yamechakaa, yanavuja na kuhatarisha afya za wafanyakazi na kwamba jitihada za kuifanya Idara hii iwe Wakala anayejitegemea zifanyike haraka ili ifanye kazi zake kibiashara na kupunguza kuitegemea Serikali. Aidha, Idara ijitahidi kuwa na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kurahisisha uchapishaji wa sheria ndogo na Miswada ya Sheria.

Tatu, ili kuwawezesha Wabunge na wananchi kwa ujumla wafahamu Miswada inayotarajiwa kuwasilishwa Bungeni, Serikali iandae ratiba ya mwaka mzima *(Legislative Programme)* itakayoorodhesha Miswada hiyo kama inavyofanyika kwa nchi nyingine za Jumuiya ya Madola. *(Makofi)*

Nne, Kamati ilipotembelea Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ilipata maelezo kuwa Sheria ilivyo hivi sasa haiwezeshi Tume hiyo kufanya kazi Zanzibar. Hivyo Kamati ilishauri kuwa Sheria irekebishwe ili Tume hiyo iweze kufanya kazi zake Zanzibar. Aidha, Kamati ilishauri kwamba Tume ifungue Kanda nyingi mikoani ili iratibu vizuri shughuli zake na ifanye jitihada za kutosha kuwaelimisha wananchi juu ya haki zao.

Tano, kuhusu *TASAF* pamoja na utekelezaji wa awamu ya pili ya *TASAF* kupanua zaidi ushiriki wa jamii, awamu hiyo imeongeza vipengele katika mchakato wa kupitisha miradi. Mchakato huo unazingatia umuhimu wa kutilia maanani viwango vya ubora vilivyowekwa na sekta. Ili kutekeleza hilo miradi iliyopitishwa na Halmashauri na kuwasilishwa makao makuu ya *TASAF* inapelekwa kwanza kwa wataalamu katika Wizara hizo za kisekta. Pamoja na nia njema ya utaratibu huo utekelezaji wake unasababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi. Kamati inashauri kuwa utaratibu huo uangaliwe upya ili wataalamu waliopo katika Halmashauri watumike na pale penye udhaifu katika ngazi hiyo uimarishwe, hii itasaidia kuongeza kasi ya kupitisha na kutekeleza miradi.

Sita, kutokana na uchakavu wa jengo la Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu, Kamati inashauri kuwa jengo hilo liimarishwe na juhudi za kuifanya Ofisi hiyo kuwa Wakala ziendelee. Pia kutokana na watu wengi kufuata huduma Dar es Salaam, Makao Makuu yaimarishwe na Ofisi za Kanda zianzishwe mikoani ili mashauri yamalizike huko huko bila ya ulazima wa kuwasumbua wananchi kwenda Dar es Salaam. Aidha, Idara hii ipewe vitendea kazi vya kisasa kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu ambazo ni muhimu kwa jamii na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Saba, Kamati ilipotembelea Tume ya Kurekebisha Sheria ilielezwa kwamba tayari Tume ilikwishazifanyia utafiti sheria mbalimbali zikiwemo za mirathi na kuwasilisha taarifa zake kwa Wizara ya Katiba na Sheria ili zifanyiwe kazi. Ripoti ambazo zimekwishapelekwa kwa Waziri ni pamoja na *Report on Private Legal Practice, Report on the Exchange Control Ordinance, Report on the Commission on the Law of Succession or Inheritance* ilipelekwa Machi, mwaka 1995. *Report on the Review of the Legislational on Access of Information, 2005, Report on the Introduction of a Legal Framework on Electronic Commerce and Cibre Crimes, 2005. Final Report on the Introduction of Good Citizenship in Tanzania, Report on the Review of Legislation Relating to Corruption,* nafikiri ndiyo tulipitisha Muswada hapa juzi *presented to the Minister for Justice and Constitutional Affairs on the 22nd December, 2004* na kadhalika.

Kamati imebaini kuwa pamoja na kupelekwa kwa taarifa hizi, Tume haipati *feedback* ya mara kwa mara juu ya utekelezaji wa taarifa zake. Kwa ajili hiyo Kamati inashauri kuwa taarifa hizo zifanyiwe kazi na Tume ifahamishwe hatua zilizochukuliwa na Wizara katika kushughulikia taarifa hizo.

Kuhusu Tume ya kuzuia UKIMWI *(TACAIDS),* Kamati inashauri kuwa chombo hicho kiangalie kwa makini mbinu inazotumia kuwafikia walengwa kwani baadhi ya walengwa wanalalamika kuwa huduma muhimu haziwafikii licha ya kuwepo kwa fedha nyingi zinazotengwa katika juhudi za kupambana janga hili. Kutokana na malalamiko yanayojitokeza dhidi ya chombo hiki, Kamati inashauri kuwa kuwe na utaratibu wa kutenganisha utendaji wa sera ili kuwe na dhana ya kuchunguzana na kudhibitiana *(checks and balances). (Makofi)*

Nane, ili kuimarisha Utawala Bora wa sheria kati ya mihimili mitatu ya dola, Kamati inashauri kuwa kuwe na utaratibu wa mawasiliano na mashauriano kati ya mihimili hii kunapotokea migongano ama migogoro ama kutokuelewana.

Tisa, kutokana na umuhimu uliopo wa Chuo cha Utumishi wa Umma na kuzingatia kuwa jengo linalotumiwa hivi sasa halikidhi mahitaji halisi ya wanafunzi. Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye jitihada za kukitafutia Chuo hicho kiwanja cha kujenga kituo kipya kitakachokidhi mahitaji yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, Bunge lako Tukufu ndicho chombo pekee kilichopewa mamlaka kwa niaba ya wananchi kusimamia Serikali na namna mojawapo ya kutekeleza wajibu huo ni kupitia katika Kamati za Bunge ikiwemo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe binafsi Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza vema Bunge lako Tukufu na kufanikisha shughuli za Kamati kwa kipindi chote hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii muhimu ya kuwasilisha taarifa ya shughuli za Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Kamati yangu katika kipindi hiki chote. Hii ni pamoja na wataalamu wote na Maafisa mbalimbali wa Wizara, Idara na Mashirika ya Umma na wadau waliofika mbele ya Kamati. Wote hawa wameshirikiana na Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee ziwaendee Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi nzuri na ushirikiano wao wa dhati waliompa Mwenyekiti kwa kipindi chote hadi tulipokamilisha maandalizi ya Taarifaa hii. Shukrani maalumu zimfikie Makamu Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mbunge kwa kuiongoza vema Kamati hasa wakati Mwenyekiti alipokuwa hayupo na yeye akakabidhiwa majukumu hayo. *(Makofi)*

Mwisho kabisa napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Bwana Damian S.L. Foka, Katibu wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Nawashukuru sana Makatibu wa Kamati hii Ndugu Emmanuel Mpanda, Ernest Zulu na Charles Mloka kwa kuihudumia vema Kamati hii kwa kipindi hicho chote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa hiyo na kwa mujibu wa Kanuni ya 106 Kifungu cha pili, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liyapokee na kuyakubali mapendekezo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na kwa kadri ya Kanuni Namba 81(11) na vifungu vidogo vinavyoambatana na Kanuni hiyo, Wabunge wote ni Wajumbe ndani ya Kamati hizo na hivyo michango yao Wabunge wa Chama Tawala na Wabunge wa Upinzani watakuwa wamechangia ndani ya Kamati hizo.

Kwa hiyo, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kutoa taarifa na taarifa yake kuungwa mkono, sasa zoezi litakalofuata ni kuchangia taarifa hiyo. Sasa kwa kuwa tunazo Kamati mbili zinazowasilisha na zitachangiwa kwa pamoja ninaomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje na yeye atoe taarifa na hivyo tutakapoipokea ili tuweze kuendelea na mjadala wa pamoja. Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, karibu.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje kuungana na Waheshimiwa Wabunge wote kutoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa Marehemu Dr. Aaron Chiduo, aliyefariki hivi karibuni. Namwomba Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Tunduru na

ikiwezekana tunamwomba basi ajiunge na Kamati yetu. Baada ya kusema hayo kwa mujibu wa Kanuni ya 88 (11) ya Kanuni za Bunge lako Tukufu, Toleo la mwaka 2004 naomba kuwasilisha taarifa ya kazi ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa kunipa heshima ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kipindi hiki na ninawaomba niwatambue kwa heshima zote. *(Makofi)*

Kwanza Mheshimiwa Mussa Zungu, ambaye ni Makamu Mwenyekiti, Wajumbe ni Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Betreace Shellukindo, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Dr.James Wanyancha, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama na mimi mwenyewe ambaye ni Mwenyekiti Anna Abdallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2006 Kamati ilifanya kazi zifuatazo:-

Kwanza kupokea taarifa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, pili, kupokea taarifa kutoka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, tatu, kupokea taarifa kutoka kwa Wabunge wa Tanzania wa Bunge la Afrika Mashariki *(Tanzania Chapter)* na nne, kutembelea Bunge la Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano kutembelea Bunge la Norway, sita, kutembelea Kituo cha Mikutano cha Kimataifa ya Arusha *(AICC),* saba, kutembelea Ubalozi wa Uingereza uliopo nchini, nane, kutembelea Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa, tisa, kukutana na ujumbe kutoka nchi mbalimbali na kumi, kufanya warsha kuhusu nafasi ya Bunge katika mchakato mzima wa uridhiaji wa Mikataba ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na moja, kupitia Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati kwa mwaka wa Fedha wa 2006/2007, kumi na mbili, kufikiria Maazimio ya Kimataifa na mwisho kupitia Hesabu zilizokaguliwa za Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Arusha *(AICC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kubwa la Wizara hiyo ni kutekeleza Diplomasia ya Kiuchumi pamoja na majukumu yake ya kawaida ya kukuza na kudumisha mashirikiano ya Kimataifa na kuiwakilisha nchi yetu nje ya nchi.

Aidha, ilielezwa kuwa ili kutekeleza jukumu hilo ipasavyo Wizara imelazimika kurekebisha muundo wake ikiwemo kuongeza idara na vitengo Wizarani pamoja na

kuimarisha Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa, kuimarisha Balozi zetu nje ya nchi, kuvutia wawekezaji nchini na kutafuta fursa mbalimbali zinazopatikana nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa hiyo, Kamati inatoa maoni na ushauri na uchambuzi wa makadirio ya Wizara. Kamati yangu ilitekeleza kazi ya kuchambua makadirio ya matumizi ya Wizara katika Ofisi Ndogo ya Bunge iliyopo Dar es Salaam katika mwezi wa Mei na Juni, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa hiyo Kamati ilitoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kwanza, mambo yote yaliyofanywa kirafiki baina ya Tanzania na nchi nyingine kama vile umiliki wa Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa, nyumba za ubalozi wa Tanzania nchini Msumbiji na mambo mengine yarasimishwe kisheria ili kuondoa migogoro inayoweza kutokea baadaye kwa kuwa viongozi waliofanya makubaliano hayo hawapo tena na waliopo wanaweza kuwa na msimamo tofauti na wale waliowatangulia.

Pili, uteuzi wa Mabalozi na watumishi katika Balozi zetu nje ya nchi uzingatie taaluma na uzoefu kwa ajili ya kutekeleza Diplomasia ya Kiuchumi na idadi ya watumishi katika Balozi zetu ilingane na ukubwa wa eneo linalowakilishwa na majukumu kutokana na malengo yaliyopo. Aidha, Balozi zetu ziwezeshwe kikamilifu ili kuitangaza nchi yetu ipasavyo hususani katika nyanja za utalii na uwekezaji.

Vile vile Kamati iwe na utaratibu wa kuzitembelea Balozi mara kwa mara ili kuona hali ilivyo katika Balozi zetu hizo.

Tatu, Wizara iwe kiungo mahsusi katika kueleza fursa zinazojitokeza Kimataifa ili Watanzania waweze kuzitumia kujiendeleza. Aidha, Serikali iangalie namna ya kuwasaidia wawekezaji wazawa kwa lengo la kuboresha uchumi wa wananchi wetu.

Nne, Serikali ihamasishe mafunzo na matumizi ya lugha ya Kiswahili na lugha mbali mbali za Kimataifa ili kuwawezesha Watanzania kupata ajira katika taasisi za Kimataifa. Aidha, kuwe na juhudi za makusudi kuwahamasisha Watanzania kutafuta ajira katika taasisi za Kimataifa na tano, Serikali iwe na mpango mahsusi wa kujenga nyumba na ofisi zake katika Balozi zetu nje badala ya nyumba za kupanga ambazo zinaigharimu fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea taarifa ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na kuelezwa kuwa jukumu kubwa la Wizara hii ni kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake ikiwemo kuratibu na kusimamia majadiliano mbalimbali yanayohusu ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujadili taarifa ya Wizara hii Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Wananchi waendelee kuelimishwa kuhusu kuwepo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zilizopo ili waweze kunufaika na kuwepo kwa Jumuiya hii. Aidha, wawekezaji wa viwanda wajizatiti ili kuweza kushindana na nchi jirani kwa uzalishaji na ubora wa bidhaa ili kumudu ushindani katika soko la Jumuiya.

(ii) Serikali ihamasishe Watanzania kutumia fursa zilizopo kwa kuzalisha bidhaa bora zikiwemo za kilimo kwa kuweka vivutio maalumu. Pia yawepo mawasiliano ya ndani kuhusu bidhaa na mazao yanayopatikana nchini kabla ya kuagiza kutoka nje ya nchi, suala hili liende sambamba na kuhimiza uzalendo wa kutumia bidhaa na mazao yanayozalishwa nchini badala ya kupendelea bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi.

(iii) Idara ya Forodha ifanye utafiti kujua sababu zinazowafanya Watanzania wengi kuingiza mizigo kupitia bandari ya Mombasa badala ya bandari ya Dar es Salaam ili kuondoa kasoro zilizopo kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali kwa kutumia bandari zetu.

(iv) Viongozi katika ngazi za Vijiji, Kata na Halmashauri za Miji waelimishwe kuhusu utoaji wa ardhi kwa wageni ili wageni wasitumie kisingizio cha Jumuiya kumiliki ardhi nchini.

(v) Tanzania iboreshe viwango vya elimu katika nyanja mbali mbali ikiwemo ufundi, lugha na maadili ya kazi ili kumudu ushindani kwa kuwa kuna wasi wasi kuwa soko la ajira la pamoja likianza ajira nchini zitachukuliwa na wageni.

(vi) Lugha ya Kiswahili imekubaliwa kutumika kama moja ya lugha zinazotumika katika mikutano ya Umoja wa Afrika likiwemo Bunge la Afrika. Kamati inashauri kuwa mikutano ya Afrika Mashariki ikiwemo Bunge la Afrika Mashariki lianze kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano badala ya kutumia lugha ya Kiingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea taarifa kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Kamati ilielezwa majukumu ya msingi ya Bunge hilo kwa mujibu wa Mkataba ulioanzisha Jumuiya ya Afrika Mshariki. Katika kutekeleza majukumu hayo shughuli zilizofanywa na Bunge hilo kwa mwaka 2005 ni pamoja na kujadili na kupitisha Miswada, kujadili na kupitisha Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuijadili taarifa hiyo Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kwanza, katika mchakato mzima wa shughuli mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni vema Tanzania ikawa na mtazamo wa kiuchumi zaidi kuliko wa kisiasa. Aidha, majirani zetu sasa wanafanya juhudi ya kushika hatamu katika nyanja za kiuchumi na hivyo kujiunga kwao katika Jumuiya ni kwa manufaa ya kiuchumi zaidi. Aidha, Watanzania tujiandae kuhimili ushindani katika Jumuiya kwa kuongeza na kuboresha uzalishaji kwa vile sisi tunazo fursa zaidi kuliko wenzetu.

Pili, wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge walielewe vizuri tatizo la bonde la Ziwa Viktoria kwani kwa sasa maji ya Ziwa hilo yanapungua kwa kasi hivyo kuhatarisha maisha ya watu wapatao milioni 30 wanaotegemea Ziwa hilo na hivyo kuhitaji ushirikiano katika kukabilina na uharibifu wa mazingira ya bonde la Ziwa Victoria. Zipo taarifa kuwa nchi moja mwanachama wa Jumuiya inatumia maji ya Ziwa hilo kuzalisha umeme kinyume na makubaliano kuhusu matumizi ya maji ya Ziwa hilo.

Tatu, kuwe na ushirikiano wa karibu baina ya Wabunge wetu wanaotuwakilisha katika Bunge la Afrika Mashariki na wadau mbalimbali nchini wakiwemo Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili wanapokwenda katika Bunge la Afrika Mashariki wawakilishe mawazo ya Watanzania na siyo mawazo yao tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutembelea Bunge la Kenya, baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Kamati ya Ulinzi na Usalama walitembelea Bunge la Kenya kwa mwaliko wa Spika wa Bunge la Kenya. Ziara hiyo ilikuwa ya siku nne ambapo ujumbe huo uliondoka nchini tarehe 16 Mei, 2006 na kurejea tarehe 20 Mei, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo msafara wetu ulijifunza mambo yafuatayo:-

Kwanza, Bajeti ya Ofisi ya Bunge huidhinishwa na Bunge lenyewe na kutekelezwa na Serikali. Aidha, Bajeti hiyo haijadiliwi na chombo kingine chochote na hii inaimarisha dhana ya Bunge kuwa mhimili mmojawapo wa nchi bila kutegemea hisani ya Serikali. Hivyo Bunge limeweza kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia Serikali ipasavyo na kuleta maendeleo.

Pili, kila Mbunge ana ofisi yake katika jengo la Bunge pia ana kompyuta na mtandao *(internet).*

Tatu, Kenya ina sheria inayoelekeza kuwa 2.5% ya mapato ya Serikali igawanywe kwa kila Jimbo kwa ajili ya maendeleo *(Constituency Development Fund- CDF),* kwa wakati huo (Mei, 2006) juhudi zilikuwa zinafanywa ili asilimia hiyo ipande kufikia 7.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutembelea Bunge la Nchi ya Norway, Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Bunge la Norway kwa lengo la kujifunza masuala mbalimbali yanayohusu Bunge hilo na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijifunza mambo yafuatayo:-

(1) Maamuzi mengi yanayofikiwa Bungeni yanatokana na utafiti wa kina kuhusu jambo linalotakiwa kutolewa uamuzi.

(2) Sheria nyingi za nchi hiyo zinatokana na Miswada binafsi na hii inaonyesha kuwa Bunge halibanwi na Miswada ya Serikali tu katika kuamua mustakabali wa nchi hiyo.

(3) Rasilimali za nchi zikiwemo mafuta, gesi na misitu zinainufaisha nchi hiyo kwa 90% tofauti na hali ilivyonchini mwetu.

(4) Japokuwa kodi nchini Norway ni kubwa, wananchi wa Norway wanafurahia matumizi ya kodi yao kwa kuwa huduma za kijamii zinatolewa bure na miundombinu mbalimbali ina ubora wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha *(AICC)* ambapo ilipata fursa ya kujionea miradi mbali mbali ya Kituo hicho, pamoja na eneo la ekari 21 linalokusudiwa kujengwa kituo kipya cha kisasa cha Mikutano ya Kimataifa, Hospitali ya *AICC* na kumbi za mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujionea maeneo yote hayo Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

Kuna upungufu mkubwa unaosababisha usumbufu wakati wa mikutano katika kumbi za mikutano zinazotumika sasa kwa kuwa kumbi hizo hazikujengwa kwa ajili ya matumizi ya mikutano bali kwa ajili ya ofisi za iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati inashauri kuwa Serikali ijenge jengo la kisasa litakalokuwa mahsusi kwa ajili ya Mikutano ya Kimataifa hapa nchini; hasa ikizingatiwa kuwa Mikutano ya Kimataifa ni sehemu ya kutangaza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa kilichopo Kurasini, Dar es Salaam. Kamati ilipokea maelezo mbalimbali kuhusu maendeleo ya Kituo hicho. Tatizo kubwa linalokikabili Kituo hiki ni utata wa umiliki ya Kituo hicho kwa kuwa kisheria kinamilikiwa na nchi mbili za Tanzania na Msumbiji. Hata hivyo Msumbiji haijishughulishi kwa lolote na Kituo hiki tangu mwaka 1986. Kuna taarifa kuwa Msumbiji tayari imeanzisha chuo chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utata huu unakwamisha maendeleo ya Kituo hicho hasa linapokuja suala la kutafuta fedha kwa ajili ya kukiendeleza, hata Hazina ya Tanzania inasita kutoa fedha zote zinazohitajika kwa ajili ya maendeleo ya Kituo hicho kwa vile wao wanaelewa kwamba Kituo hiki kinamilikiwa na nchi mbili na nchi hiyo ya pili inapaswa kuchangia maendeleo ya Kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea taarifa hiyo Kamati ilitoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kwanza, Serikali ya Tanzania iwasiliane na Serikali ya Msumbiji ili kupata uhakika kama Msumbiji bado ina nia ya kumiliki Kituo hiki ili hatimaye miliki ya Kituo hicho iwe na jina moja tu la Tanzania.

Pili, Kituo kianzishe na kuimarisha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa kuwa lugha hii imekuwa ya Kimataifa na Tanzania inapaswa kunufaika nayo na kuhusika kikamilifu katika kukiendeleza katika maeneo mbalimbali duniani.

Tatu, Serikali iboreshe Kituo hiki katika nyanja mbalimbali zikiwemo miundombinu, maslahi ya wafanyakazi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukutana na Ujumbe wa kutoka Mabunge ya nchi mbalimbali, Kamati ilipata fursa ya kukutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Wabunge kutoka nchi za Thailand, Vietnam, Cuba na Marekani. *(Makofi)*

Madhumuni ya kutembelea Bunge la Tanzania ni kuanzisha ushirikiano baina ya Bunge la Tanzania na Mabunge ya nchi hizo. Wageni walisisitiza kuwa ushirikiano ni muhimu kwa kuzingatia uhusiano mzuri na wa kihistoria baina ya Tanzania na nchi hizo ulioanzishwa na waasisi wa nchi zetu. Walisisitiza kuwa uhusiano huo utaimarishwa kama Bunge la Tanzania litaridhia urafiki kati yake na Mabunge ya nchi hizo kupitia Kamati ya Mambo ya Nje kwa kutembeleana mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliwashukuru wajumbe hao na kueleza kuwa tayari kwake katika kuanzisha na kuimarisha ushirikiano baina ya Bunge letu na nchi hizo. Aidha, Kamati inatoa ushauri kuwa Bunge letu liendeleze ushirikiano na nchi hizo kwa njia mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutembelea Mabunge yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, warsha kuhusu nafasi ya Bunge katika mchakato mzima wa uridhiaji wa mikataba ya Kimataifa iliendeshwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu. Ilielezwa kuwa nchi ya Tanzania imetia saini mikataba mingi ya Kimataifa inayohusu Haki za Binadamu hususani haki za wanawake na watoto. Hata hivyo, mikataba mingi bado haijaridhiwa na hata iliyoridhiwa vipengele vyake havijaingizwa kwenye sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka siku ya warsha hiyo, tarehe 30 Mei, 2006, Mikataba 13 inayohusu masuala mbali mbali ya Haki za Binadamu ilikuwa haijaridhiwa kati ya hiyo Mkataba wa zamani zaidi ni wa mwaka 1949 unaohusu uanzishwaji wa Tume ya Kimataifa Inayoshughulikia Uchunguzi wa Masuala ya Kibinadamu *(The first Optional Protocol to Geneva Conventions of 1949 which Establishes the International Humanitarian Fact Finding Commission).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mawasilisho hayo Kamati inatoa maoni yafuatayo:-

Kwanza, Sheria za Tanzania ziandikwe au zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili ili zieleweke na wananchi wengi zaidi kwa kuwa wao ndiyo wadau muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hukumu ya kifo haitekelezeki kwa kuwa kuna mamia ya wafungwa waliohukumiwa kunyongwa na hawajanyongwa hadi leo na baadhi yao wamekuwa wakisubiri kutekelezewa hukumu hiyo kwa zaidi ya miaka kumi. Huu ni

uvunjaji wa haki za binadamu kwa kuwa wafungwa wa aina hii wamekuwa wakiishi kwa wasiwasi kwa miaka yote. Hali hii inawafanya wasione thamani ya maisha na hivyo kuwa hatari kwa wafungwa wenzao na hata kwa askari wanaowalinda na watu wengine wanaowahudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bajeti ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007, Kamati pia ilipitia mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa Fedha wa 2006/2007. Maoni ya Kamati hii kuhusu mapendekezo hayo yaliwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ipange bajeti kwa ajili ya kujenga ofisi zake badala ya kupanga kwa kuwa utaratibu uliopo sasa unaigharimu sana Serikali. Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ijenge au kununua nyumba kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi. Vile vile Wizara hii ijenge ofisi ya makao makuu yenye hadhi, ofisi zinazotumika sasa hazina hadhi inayolingana na hadhi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maazimio ya Kimataifa mwaka 2006, Kamati ilipitia Azimio moja la Kimataifa lililohusu Uanzishwaji wa Mahakama ya Afrika. Aidha, maoni ya Kamati kuhusu Azimio hili yaliwasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Pili wa Bunge hili na liliridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hesabu zilizokamilika za Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha, Kamati ilipitia hesabu zilizokaguliwa za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha *(AICC)* za mwaka 2005/2006. Katika mapitio ya hesabu hizi Kamati ilielezwa kuwa Kituo kinadai fedha nyingi kwa watu, makampuni na taasisi mbalimbali ikiwemo Idara za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** kwa mujibu wa hesabu zilizowasilishwa, kituo hiki bado kinadai jumla ya shilingi 401,756,888.46, kutoka kwa wadaiwa mbalimbali zikiwemo Idara za Serikali zinazodaiwa jumla ya shilingi 122,439,437.11, Taasisi za Kimataifa jumla ya shilingi 12,836,816.08, Makampuni binafsi jumla ya shilingi 180,988,213.32, watu binafsi jumla ya shilingi 64,517,622.95 na madeni kutoka kwenye makampuni yaliyobinafsishwa na kupelekwa *PSRC,* ni jumla ya shilingi 20,974,799.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni haya yanarudisha nyuma maendeleo ya kituo hiki, hivyo Kamati inashauri kuwa hatua madhubuti zichukuliwe ili kuhakikisha kuwa madeni yote yanalipwa ili kukiwezesha kupanga mipango yake kikamilifu. Wizara na Idara za Serikali zihakikishe kuwa zinamaliza kulipa madeni hayo kutoka kwenye Bajeti zao, aidha, kwa wadaiwa binafsi hatua za kisheria zichukuliwe ili kuhakikisha madeni hayo yanalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, tatizo kubwa linaloikabili Kamati ni kuwa na Bajeti ya Bunge finyu na kwa kweli Kamati haijui hasa Bajeti yake, Bajeti iliyo na uhakika ni posho kwa ajili ya vikao vya Kamati. Kamati imeshindwa hata kutoa

zawadi japo ndogo kwa wageni wake walioitembelea. Aidha, Bunge lenyewe halina aina yoyote ya *souvenior* inayotambulisha Bunge la Tanzania na kwa kweli hii kidogo inatupa aibu kwa sababu wageni wanapofika wanatoa *souvenior* za kwao sisi hatuna hata kitu kimoja cha kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingefaa Kamati zote za Bunge sio Kamati hii tu zijue ukomo wa matumizi yake kwa mwaka. Hii ingerahisisha Kamati kupanga kazi zake. Kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 Bunge lako Tukufu lilipitisha kiasi cha shilingi 34, 245, 022, 500 kwa ajili ya Balozi zetu nje ya nchi. Ni wajibu wa Kamati hii kufuatilia matumizi ya fedha hizi ikiwa ni pamoja na kujionea hali halisi ya namna zinavyotumika. Kwa mtindo wa Bajeti za Kamati uliopo sasa Kamati ya Mambo ya Nje haitaweza kufanya kazi zake ipasavyo ikiwa ni pamoja na kufuatilia matumizi ya fedha hizi.

Napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa mwaka 2006. Pia nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyoihusu Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya taarifa hii na kunipa heshima ya kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuwashukuru Waheshimiwa waliokuwa Mawaziri wa Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mwaka 2006, Makatibu Wakuu na maofisa mbalimbali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati wote ilipohitaji taarifa mbalimbali kutoka kwao. Napenda kukushukuru sana wewe, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, kumpongeza Katibu wa Bunge, Katibu wa Kamati na Maafisa wote wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka mzima wa 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kuikubali taarifa hii pamoja na mapendekezo na maoni yake. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na sasa tutaanza mjadala wetu wa jumla. Naomba niwataje wasemaji wetu ambao wamekwisha wasilisha maombi yao hapa mezani. Tutaanza na Mheshimiwa Ruth Msafiri halafu atafuatia Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Stephen Galinoma naye ajiandae na hao wote wameomba kuchangia hoja ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Charles Kajege na Mheshimiwa Juma Killimbah wao wameomba kuchangia hoja ya Kamati ya Mambo ya Nje. Kwa hiyo, naomba nimwite Mheshimiwa Ruth Msafiri aanze, na Mheshimiwa Grace Kiwelu ajiandae. Mheshimiwa Ruth Msafiri, karibu. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa kuchangia katika hoja ya Kamati hizi mbili, nakushukuru sana. Nawapongeza wote waliotoa hoja zao walioziwasilisha hapa kwa niaba ya Kamati, Mheshimiwa Charles Keenja kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje. Tunashukuru na tumezipokea hoja hizi na ni hoja za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naendelea kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa kutupatia nafasi Bunge kujadili hoja hizi badala ya kuziwasilisha tu mezani. Tumekuwa tunaaga Majimboni kwa wananchi kwamba tunakuja katika Kamati za Bunge lakini wananchi wanakuwa hawafahamu, tunazungumza nini katika Kamati za Bunge. Pengine wanafikiri kwamba Wabunge wanapenda kukaa Dar es Salaam kama wengine walivyo na mawazo hayo. Sasa kwa kuwa nina nafasi hii ya kujadili hoja zinazopitia ndani ya Kamati zetu za Bunge inasaidia wananchi kufahamu kwamba tunapokuwa Dar es Salaam tunakuwa katika Kamati ambazo zinajadili mambo yanayohusu huduma za wananchi wetu na mambo mbalimbali yanayohusu Taifa letu na Mataifa mengine. Kwa hiyo, napendelea kuiomba Serikali kwamba izidi kuweka nafasi kwa Wabunge kupata nafasi kuendelea kuijadili hoja za Kamati mbalimbali katika Bunge lako Tukufu. Nakushukuru sana *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kuona kwamba katika hotuba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wameelezea miongoni mwa ziara zao kwamba waliweza kutembelea katika baadhi ya miradi ya *TASAF.* Mimi napenda kusema kwamba katika miradi ambayo imeisaidia jamii moja kwa moja katika makundi yao lakini hasa inalenga moja kwa moja jamii ni pamoja na mradi wa *TASAF*. Mradi wa *TASAF* umesaidia kuendeleza miradi mbalimbali.

Kwanza kuwashirikisha wananchi katika kuibua miradi hii kuisimamia na hasa kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika. Miradi mingi ikiwemo miradi ya maji, miradi ya shule hasa shule za sekondari za kutwa, barabara mbalimbali ambazo zinahudumiwa na Halmashauri zimeweza kuhudumiwa na *TASAF,* hospitali na zahanati. Hata mimi ninayo mifano halisi katika Jimbo langu pia nimepata msaada huo kupitia *TASAF*.

Napenda kuipongeza sana Serikali na kuushukuru mfuko wenyewe wa *TASAF* kwa jinsi ambavyo umeweza kukwamua ile miradi iliyokuwa migumu kuweza kutekeleza kwa Bajeti ya moja kwa moja ya Serikali. Pia ninawashukuru sana wananchi kutimiza masharti ya mradi wa *TASAF* kuwataka wachangie. Mafanikio makubwa ambo mfuko wa *TASAF* umefanikiwa kuyafikia ni kwa sababu wananchi wameelimika, wakakubali kwamba Mfuko huu ni kwa ajili ya maendeleo yao wakajitolea kuchangia nguvu, hali na mali na kuhakikisha kwamba tumeweza kufanikisha miradi hiyo ya TASAF.

Mimi nawashukuru sana wananchi, nawapongeza na naendelea kuomba kwamba mfuko huu uendelee kutusaidia na wananchi waendelee kujitolea wakijua kwamba kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambacho kinaongoza Serikali. Pale ambapo wananchi wanajitolea kwanza kutoa mchango wao kwa nguvu zao wenyewe mradi

unapokuwa umeonekana ukathibitishwa basi na Serikali inamalizia ni pamoja na mradi wa *TASAF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kuhusu namna ya kutathimini. Kumekuwa na matatizo katika kufanya tathmini ya hii miradi, wananchi wanatakiwa watoe nguvu zao katika hii miradi. Lakini wanapokuwa wametoa nguvu ile tathmini kwa mifano ya nguvu kazi inakuwa ni ya chini mno na hili nimeliona na hasa katika uchangiaji katika shule zetu za Sekondari. Unakuta nguvu ya wananchi inatathiminiwa kwa kiasi kidogo kiasi kwamba unapoonyesha mchango wa wananchi unaweza ukafikiri wananchi hawachangii lakini wamechangia sana. Zile rasilimali zinazotolewa na wananchi mfano mawe, kokoto, matofali na mchanga kwenye *site,* tathimini yake unakuta inakuwa ni ndogo. Kwa hiyo, ukienda kuwaambia wananchi kwamba mmejitolea thamani yenu nyie ni shilingi hizi. Mimi naomba kwamba tathimini iwepo, kama inawezekana basi kuwe na utaratibu wa Kitaifa kwamba wananchi wanapojitolea nguvu zao katika siku nzima katika mradi, thamani yake ni shilingi kadhaa ili ile idadi yao na jumla ya zile pesa zinapozidishwa ijulikane kwamba wamechangia kiasi fulani itawatia moyo na itasaidia wahisani wetu kufahamu kwamba kumbe wananchi wako mstari wa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limenivutia sana ni kutembelea maeneo ya Mahakama, naomba kuendelea kuwashukuru na kuzidi kuiomba Serikali yetu kwamba mahakama ni mahali pa kutolea haki kwa wananchi. Mahali ambapo pa faraja, panatakiwa pawe ni mahali pazuri panapomvutia mwananchi anapokuwa ametuhumiwa, na kwa kawaida mtuhumiwa hana kosa hadi atakapotiwa hatiani. Basi mahakama ziwe mahali pazuri, aweze kupata mahali pa kukaa kusikiliza kesi yake. Lakini hata Hakimu naye, si mfungwa, kwamba basi asikae katika mazingira machafu, mabovu. Hata wafungwa sasa hivi hali zao zinakuwa ni nzuri, sembuse Hakimu anayesimama pale saa zote akiwa anatoa haki. Nikitoa mfano halisi wa mahakama yangu moja katika Jimbo la Muleba inaitwa Mahakama ya Muhutwe, ni Mahakama moja inayotisha kweli kweli, Hakimu akiingia pale kwa saa nne lazima atoke anaumwa kichwa ama mafua. Kwa sababu kuna mavi ya popo yanayonuka, ama nimeseme kunukia, kwa sababu yakinuka hawezi kukaa, yananukia kiasi ambacho lazima atapata *fresh* yake. *(Makofi)*

Sasa ni vizuri maeneo kama haya basi yakatiliwa nguvu, mahakama zetu zijengwe upya ambazo zimeonekana zimepitwa na wakati, zikarabatiwe zile ambazo zinaweza kukarabatiwa. Lakini mimi napendekeza kuwe na eneo la watu wengine nje. Tulipopata bahati ya kutembelewa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria, nilimwomba sana kwamba mazingira ya Mkoa wa Kagera, yana mvua nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingi katika msimu mrefu wa mwaka kunakuwa na mvua, sasa unakuta watu wanaokwenda mahakama awe ni yule aliyekosa, awe ni shahidi basi wote watanyeshewa na mvua kwa sababu hawana mahali pa kukaa, kwa sababu kule ndani kesi inaendelea lazima wajibane nje. Hii ni hali ambayo naomba ili wananchi wanapokwenda kusikiliza na kupata haki zao wawe na mahali ambapo pia pana heshima na panafurahisha ili kuweza kuwa tayari kusikiliza hukumu zao na kesi zao zinavyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba kipindi kilichopita nilipokuwa katika Bunge hili nilibahatika kuwa katika Kamati hii ya Katiba Sheria na Utawala, tuliwahi kutembelea baadhi ya Mahakama, Magereza ambapo tulitembelea gereza la Isanga hapa Dodoma.

Katika Gereza la Isanga tulikuta kesi mbili ambazo zilinitisha sana. Kesi moja ilikuwa ni ya wanawake ambao walifungwa na watoto wao, tukapenda kujua hivi ni hatma gani ya huyu mtoto ambaye amefungwa na mama yake? Lakini kesi nyingine ya kutisha ilikuwa ni wanawake waliokuwa wameingizwa mahabusu kwa sababu waume zao walikimbia kabla ya kukamatwa wakati walipokosa.

Sasa mimi sikuwa ninafahamu kwamba hivi kama mume wangu akifanya makosa akakimbia, nikamatwe mimi! Ni mimi niingie Gerezani! Ninasubiri nini? Tulipouliza, tuliambiwa eti yule mwanaume akisikia kwamba mke wake amekamatwa, basi atarudi kumdhamini mkewe na watamweka yule mwanaume ndani na yule mwanamke anatolewa. Hii ni haki gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kufahamu utaratibu huo ambao unatumika kuacha mkosaji kwa sababu tu hakupatika, basi jamaa yake wa karibu au mke wake kwa maana ya moja kwa moja tuliyoishuhudia, anaweza kuwekwa mahabusu ili kusubiri huyu mwenzake aweze kupatikana. Mimi nadhani hapa sijaelewa hii haki na ni utaratibu gani unatumika katika kulinda haki za binadamu na katika kutoa haki kwa huyu ambaye hana kosa, kwa sababu siyo mtuhumiwa na si mkosaji. Sijui anaingia vipi katika hiyo mikono! Kwa hiyo, nilipenda kuona kwamba hili liangaliwe kusudi familia zetu zisiteseke na binadamu asiteseke pasipokuwa wametenda makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda nilisemee kidogo lililotokea katika Wizara ya Mambo ya Nje ni hili la Wabunge kutokuwa na ofisi. Ni kweli kabisa kwamba katika Bunge letu Wabunge hawaibui sana Miswada ya kuleta Bungeni, lakini moja ya sababu za msingi ni Wabunge kutokuwa na mahali pa kukaa kutafakari mambo yao wanapokuwa wapo Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishi maisha ambayo kwa kweli sio mazuri sana kama ambavyo pengine mtu anaweza akafikiria. Tukitoka asubuhi majumbani tunakuja Bungeni, tunakaa ndani ya mikutano ya Bunge lakini ule muda wa kuanzia saa 7.00 mpaka saa 11.00 jioni, walio wengi huwa hatujui tufanye nini zaidi ya kuamua kurudi majumbani, au kutembelea marafiki, au kwenda kupata *siesta.* Sio lazima kupata *siesta* lakini unailazimisha kwa sababu licha tu ya huo Muswada ambao umepanga kuziandaa, au kwa maandishi, au kupata nafasi ya kuchangia dakika 15, kwa miaka mitano ni mingi mno ambayo tungeomba kwamba tuwe na ofisi ili zituwezeshe kukaa na kutafakari na kuweza kukaa na hata watumishi wa Bunge wapo hapa, watafiti waliowekwa hapa, lakini hatuwatumii ipasavyo kwa sababu tutawatumia kwa namna gani? Hatupati muda wa kutumia intaneti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna intaneti yetu ndogo hapa ambayo hata wakitaka Wabunge 20 kuingia kwa pamoja haiwezekani. Kwa hiyo, unakuta kwamba kweli bado

hata ari ya kufanya kazi tunapokuwa hapa Bungeni bado inakuwa ni ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nenda basi Majimboni, unaweza ukacheka! Nitoe mfano wa ofisi yangu mwenyewe niliyopewa na Serikali, ina kiti kimoja na ofisi ni moja. Nilikuwa na *laptop,* nilishindwa kufanya kazi kwa sababu haina hata *socket* ya kuwekea umeme. Sasa hiki ni kitu ambacho hakiwezi kutoa moyo wa kufanya kazi wala kuibua mambo mapya. Isipokuwa, ninaamua kufanya ziara nyingi, nitembelee wananchi kule walipo na nizungumze nao kule kule, yale mengine yaliyobaki mimi namwachia Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi na Chama changu cha Mapinduzi waone watafanya nini. Lakini sipati moyo wa kuwa kwenye ofisi kwa sababu akija hata mgeni mmoja lazima nikaombe Serikali masjala waniletee kiti, wakija wawili maana yake mmoja lazima asimame. Sasa Ofisi ya Mbunge inaweza ikakosa hata kiti cha kukalia wageni kweli kusikilizwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo nafikiri sasa ni wakati muafaka Serikali itujengee ofisi. Tunapokuja hapa kwa kazi, Wabunge wawe na ofisi nzuri zilizo na zana. Wabunge wamejifunza kompyuta vizuri na wana uelewa wa kutosha wa kompyuta hapa kila mmoja, lakini tunazitumia wapi? Tukishakuwa tumerudi kule kwetu tunapata matatizo. Sasa nilikuwa ninapendekeza kwamba jambo hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninalopenda kulizungumza ni kwamba, tuliwahi kutembelea Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais. Pia pale mapokezi hapakuwa pamejengwa kiasi hicho mwaka 2000 tunaingia Bungeni, lakini Kamati yetu ndio ilipendekeza pajengwe pawe na hali nzuri ya usalama, namna wageni wanavyoingia na mazingira yaonekane mazuri. Mimi nilikuwa naomba kwamba, hata Ofisi ya Waziri pale mapokezi pajengewe eneo zuri la ukaguzi na usalama ambao hakika kila anayeingia ajue anaingia Ofisi ya Waziri Mkuu na ukaguzi uwe ni wa kutosha. Sio mtu anaingia moja kwa moja kwenye ile ofisi ndogo, akitoka pale moja kwa moja anaingia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi za Mawaziri wengine waliopo pale na maafisa. Mimi nilikuwa nadhani, lango kuu la Ofisi ya Waziri Mkuu linalotumika, lingejengwa kwa hali bora zaidi na ya kiusalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililoliona katika bajeti ya mwaka 2006 tulipokuwa tunachangia hotuba, ni la uzoefu. Katika kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu miaka iliyopita, Waziri Mkuu anapewa wiki nzima, wakati ule TAMISEMI ilikuwa ipo chini ya Ofisi ya Rais. Kwa hiyo, TAMISEMI ilikuwa tunaijadili peke yake kwa siku mbili zinazojitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ni Wizara ambayo kwa kweli chini yake yapo mambo mengi sana. Kwa hiyo, kuiweka katika bajeti ya Waziri Mkuu ya siku tano ikawa humo humo tujadili Wizara nyingine na TAMISEMI, maana tulikuwa tunajadili kwa siku mbili. Mimi niliona kama tulijinyima nafasi ya kuchangia vizuri kwenye hotuba ya TAMISEMI.

Nilikuwa ninaomba basi, katika bajeti inayokuja ya mwezi wa Sita kutengwe siku mbili za ziada katika Ofisi ya Waziri Mkuu, apewe siku tano kwa maswali ya Waziri Mkuu kwa sababu pia ni mengi, huwezi kuzipunguza zile siku pia. Kuwe na siku mbili za ziada, lakini ziwe rasmi kwa ajili ya TAMISEMI tu ili tuweze kupata mwanya wa kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi kwenye TAMISEMI hata sistahili kuyazungumza yote hapa kwa sababu ninayafahamu kabisa kwamba kila mmoja anaelewa ndipo pesa zote za Serikali Kuu zinakwenda kule kusaidia, pesa za Wahisani zipo kule, huduma za jamii zimejaa kule na hasa ndio kiini cha kujadili maendeleo ya wananchi.

Kwa hiyo, tunahitaji tupate nafasi ya kujadili hotuba ya TAMISEMI inayojitegemea kwa siku mbili zilizokamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, ninashukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia taarifa hizi mbili za Kamati zilizoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kutoa mchango wangu, napenda kutoa pole kwa familia ya aliyekuwa Mbunge na Waziri katika Bunge lililopita, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo na tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na nitaanza na suala zima la sheria zilizopitwa na wakati. Ndani ya Bunge lako Tukufu, tuna Chama cha Wabunge Wanawake ambacho kinawahusisha Wanawake wote bila kujali vyama na moja ya madhumuni ya Chama chetu ni kuzisemea zile sheria ambazo tunaona zinamgusa mwanamke na zimepitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kipindi changu cha pili katika Bunge hili, lakini kuna sheria ambazo tumeuliziwa kwa muda mrefu na tukapewa majibu kwamba sheria hizo zinashughulikiwa. Lakini mpaka hivi leo, sheria hizo hazijaweza kufika katika Bunge lako hili ili ziweze kujadiliwa na kuweza kutoa haki hasa kwa akina mama ambao wameteseka sana au wamenyimwa haki kutokana na sheria hizi kupitwa na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya mirathi na sheria ya ndoa ya mwaka 1971, zinawanyima haki akina mama, hasa sheria ya mirathi. Akina mama wengi wanapata matatizo makubwa hasa waume zao wanapofariki, ndugu wa waume hao huingilia na kuwanyang'anya mali na kuwaacha mama na watoto katika matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimeletwa sheria nyingi sana ndani ya Bunge lako Tukufu na tumeweza kuzipitisha, lakini nashindwa kuelewa ni kwa nini sheria hizi haziletwi. Kuna tatizo gani? Katika taarifa ya Kamati, walitembelea Tume ya Kurekebisha Sheria na Tume hiyo ilitoa maelezo mbele ya Kamati kwamba sheria hizo zimeshapitiwa, zimeshafanyiwa kazi na zimepelekwa Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa anayehusika na Wizara hiyo atuambie ni nini kinazuia kuleta sheria hizo mbele ya Bunge lako ili sisi akina mama ambao tumepata nafasi hii kuwawakilisha wanawake ndani ya Bunge hili tuweze kuzitetea na kuzipitisha ili akina mama hao waweze kupata haki katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulizungumzia ni ucheleweshaji wa kesi. Hivi karibuni, nchi yetu imeingia katika mgomo na tuliona wafungwa wakigoma kwenda mahakamani na hii imesababishwa na ucheleweshaji wa kesi na ilibidi wafanye hivyo baada ya kuona kwamba zipo kesi nyingine ambazo zinafanyiwa upelelezi haraka sana na watu wengine kuachiwa au kupata dhamana kutoka nje ya mahakama. Hii ilitokea pale Mkuu wa Mkoa wa Tabora alipoweza kupata dhamana na kutoka. Moja ya sababu ambazo wafungwa wale walisema ni ucheleweshaji wa kesi zao na taarifa juu ya kesi zao zilikuwa hazifiki mahakamani.

Mimi ningependa kujua ni kwa nini kesi za wale wanyonge ambao hawana uwezo wa kuweka mawakili hazifanyiwi kazi. Je, ni wakubwa tu au wenye uwezo ndio watakaoweza kupatiwa haki katika nchi hii? Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Wizara husika ituambie kwa sababu tunataka utawala wa sheria na wa haki katika nchi yetu. Hii inaonyesha kabisa kwamba upo upendeleo kwa baadhi ya washtakiwa katika nchi yetu na sasa sisi Wabunge tusipokuwa wakali na kuyasemea haya nchi yetu itaonekana haisimamii sheria wala utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanyonge nao wana haki, hata wale mahabusu ambao hawana uwezo wa kuweka mawakili nao wanatakiwa wapate haki na kama tatizo ni ucheweshaji wa taarifa zao kuletwa mbele ya mahakama na kuwafanya mahabusu wale waendeleee kukaa ndani, tunaishauri Serikali iweze kuwasomesha mahakimu wengi na kukipanua kile Chuo cha Mahakama kilichopo Lushoto – Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi tunaweza kupunguza tatizo kubwa sana la msongamano ndani ya magereza yetu, mengi yamejaa na imekiuka kabisa taratibu ambazo zinatakiwa wafungwa kuwa ndani ya gereza moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupanua na kuongeza Chuo kile kinachotakiwa kwa mahakimu hawa ni kuwaongezea motisha, mishahara yao iongezwe ili nao waweze kutenda haki kwa zile kesi zinazokuja mbele yao. Tusipoweza kuwaongezea au kuwahamasisha mahakimu hawa, bado tatizo la rushwa litaendelea kuwepo ndani ya nchi yetu na hakutakuwa na haki katika kesi zitakazopelekwa katika mahakama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningetaka kulisemea katika taarifa hii ya Katiba, Sheria na Utawala ni *TACAIDS.* Wiki iliyopita tuliweza kubahatika kupata semina ambayo ilifadhiliwa na Ubalozi wa Marekani. Tuliona fedha nyingi sana zinazokuja ndani ya nchi yetu, lakini Wabunge walishindwa kuelewa mgao unaotokana na fedha zile kuwafikia wale waathirika wa ugonjwa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya semina nyingi sana kuhusu ugonjwa huo, lakini wale walengwa bado wanazidi kuathirika. Wagonjwa wale waathirika wa UKIMWI kuwapa dawa haitoshi bila chakula. Dawa zile zina nguvu sana na kama hatutatumia fedha zile kuwapa lishe bora hatutakuwa tumewasaidia wagonjwa wa UKIMWI. Hivyo tunaiomba Wizara ya Afya kushirikiana na *TACAIDS* waweze kuweka utaratibu mzuri wa kuweza kuzisimamia pesa hizi pindi zinapopelekwa kwenye *NGOs* maana *NGOs* nyingi zipo, lakini tunashindwa kuelewa wanafanya kazi gani na matokeo yake fedha nyingi zinaingia kwenye mifuko ya watu binafsi na wale wagonjwa wanaendelea kupata shida na wengi wanakufa kwa njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliyoyaona katika taarifa hii ya Katiba, Sheria na Utawala ni hayo machache na nikaona ni muhimu niyaseme na kuyasema ndani ya Bunge lako hasa hizo sheria nilizozisema ambazo zinawanyima haki akina mama hasa Vijijini pale waume zao wanapofariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika hoja hizi mbili, Kamati ya Mambo ya Nje na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Niseme toka mwanzo kwamba, kama mjumbe mmojawapo wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naunga mkono hoja moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, naomba nizungumzie mkazo au msisitizo katika mambo machache ambayo nafikiri yatasaidia mjadala wetu. Nitadonoa mambo machache kufuatana na Idara au Wizara zile zinazosimamiwa na Kamati yangu. Kwanza kabisa, ni kuhusu Mpiga Chapa wa Serikali. Ningependa kushauri moja kwa moja kwamba huko nyuma kulikuwa na utaratibu ambao ningependa urudiwe wa kuchapisha *official gazette* kila siku ya Ijumaa na vile vile *government directory*. Hii ingetuwezesha sisi Wabunge na wadau wengine kupata nakala za Miswada na Sheria ambazo zimeidhinishwa kuliko hali ya sasa ambayo mara nyingi tunakuja kushtukizwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria, ningependa kusema mambo mawili au matatu. Kwanza naishukuru sana Wizara ya Katiba na Sheria, wamejenga Mahakama Kuu katika Mkoa wangu wa Iringa, wamebadilisha sana sura ya mji ule na ninashukuru sana kwamba wameweza kufanya hivyo.

Lakini hapo hapo ningependa kuomba Wizara ijenge Mahakama ya Mwanzo pale Kalenga. Kalenga ndio kitovu cha historia, siyo tu ya Mkwawa na Wahehe, lakini ni kitovu cha upiganiaji wa Uhuru katika nchi hii. Kwa hiyo, ni vizuri tuondoe aibu iliyopo sasa ambapo haki inatolewa katika magofu ambayo hayana hadhi yoyote. Tukijenga mahakama mpya, siyo tu tutawezesha haki kutendeka kwa wakati na kwa hadhi inayostahili lakini pia tutaimarisha makumbusho yaliyopo pale ambayo kama nilivyosema ni ya heshima ya Mkwawa na historia ya nchi hii. Mtakumbuka hata Spika wetu wa zamani, Hayati Adam Sappi Mkwawa anatokea pale, lakini leo hii ukienda pale ni aibu tupu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kusemea suala moja kuhusu Mahakama ya Ardhi. Hii ni mahakama mpya. Zipo nyingi kama Mahakama ya Kazi, hii ndio kwanza imeundwa siku za karibuni na ipo katika msingi wa kanda kwa sababu mkoa au kanda moja inapewa hakimu mmoja, anaitwa mwenyekiti na inachukua muda mrefu sana kwa kesi moja kusikilizwa, miezi sita na hata mwaka. Katika kungojeangojea yanazuka matatizo mengi, kero kwa wanaohusika na migogoro. Ningependa Serikali na kwa maana hii siyo Wizara hii ya Sheria, ni Wizara ya Ardhi watazame mfumo mzima waone jinsi gani wanaweza kuharakisha utoaji wa haki katika suala hili zima ili haki isitendeke tu, lakini ionekane kwamba inatendeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo ningependa kuzungumzia ni kuhusu utawala ambayo ipo katika Kamati yetu. Utawala una matatizo mengi sana, lakini yale ambayo yanahitaji TAMISEMI kwa mfano, nadhani itakuwa busara kuyazungumzia wakati wa bajeti na ninakusudia kufanya hivyo nikipata nafasi. Lakini hapa ningependa kusema moja tu kuhusu TAMISEMI. Kuna ucheleweshaji mkubwa sana wa fedha za ruzuku kwenda kwenye Serikali za Mitaa. Kama tunavyofahamu, Mbunge huidhinisha makisio mnamo mwanzoni mwa mwezi wa Nane mpaka fedha zikafike huko zinakotakiwa kwenda imekwishapita miezi miwili, mitatu na hata minne. Juu ya hivyo kuna huu utaratibu unaoitwa *cash budget* ambao unazuia fedha zisipelekwe mpaka mapato yaingie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa hapa niiombe Serikali ifanye kila linalowezekana kuhakikisha kwamba fedha zinapelekwa mara moja zinapoidhinishwa kule kwenye Serikali za Mitaa ili pasitokee ucheleweshaji wa miradi. Nina mfano mmoja mzuri. Kuna shirika lilitoa fedha mnamo mwezi wa Nane mwaka 2006 zikaenda TAMISEMI kwa ajili ya miradi katika Jimbo langu. Ni mwezi Machi tu ndio fedha hiyo imetolewa baada ya kuchelewa miezi sita na bila mjadala wowote. Ni dhahiri kabisa kwamba utekelezaji wa miradi yetu hauwezi kwenda ipasavyo na ninashauri Serikali ifanye kila linalowezekana kuondoa kile ambacho mimi ninakiita urasimu ambao ni wa hatari sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sipendi kuzungumza sana. Mwisho ningependa nimalizie jambo moja ambalo amesema Mwenyekiti wa Mambo ya Nje, nayo ni kuhakikisha au kuomba Serikali itoe fedha ya kutosha au bajeti ya kutosha kwa Ofisi ya Spika ili kuziwezesha Kamati mbalimbali ziweze kufanya kazi zao ipasavyo. Kamati

yangu inaelekea ndio inapata mgao mdogo zaidi kuliko nyingine japo sijua kama ni ya mwisho au vipi.

Kwa hiyo, inashindwa kufanya kazi zake ipasavyo kwa sababu inashughulikia utawala wa nchi hii. Pamoja na hayo, mambo mengine ilipaswa iwe na fedha za kutosha kutembelea miradi mbalimbali katika nchi badala ya kuchagua mradi mmoja hapa na pale, haitoi picha sahihi. Siyo hivyo tu, Kamati nyingi nyingine japo nazo zina mgogoro wa pesa zinaweza kwenda nje na kuona wenzetu wanafanyaje. Kamati hii ni ya nyumbani pamoja na kwamba mambo yake ni *international* kwa *status* yake, sioni ni kwa nini na wao wasipate bajeti ya kutosha wakaweza kwenda kujifunza mambo ambayo yangeweza kuwa na faida kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo machache, naunga mkono hoja zote mbili, ya Kamati ya Katibu, Sheria na Utawala na vile vile Kamati ya Mambo ya Nje. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia. Naomba kwa ruhusa yako nianze kwa kuwapa pole wakazi wa Wilaya ya Kyela kwa mvua kubwa inayoandamana na upepo mkali ambayo inaendelea kunyesha na imesababisha nyumba 60 za Wanachi kubomoka na mali nyingi kuteketea. Kama ilivyo kawaida, nitakuwa Kyela mara tu baada ya Mkutano huu kuahirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe pongezi kwa Kamati zote mbili kwa taarifa nzuri sana na pengine nitoe pongezi za pekee kwa Kamati ya Mambo ya Nje kwa kuendeleza rekodi yake ya pekee Barani Afrika ya kutoa Mawaziri wake kuwa viongozi wanaong'ara Kitaifa na kuwa wanadiplomasia waandamizi wa Kimataifa, Dr. Migiro, Dr. Salim Ahmed Salim ni wengi na tuna Rais wa awamu ya tatu, Rais wa awamu ya nne wote wamepita kwenye mkono wa baraka wa Kamati hii. Pengine niombe kwamba mkono wenu wa baraka uendelee hata kwa Waziri aliyepo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisamehe kwa kuongea kwa sauti ya chini kwa sababu nimegundua sasa hivi nina kikohozi. Naomba nianze na ukurasa wa 11 wa taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, inasema kwamba katika mchakato mzima wa shughuli mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni vyema Tanzania ikawa na mtazamo wa kiuchumi zaidi kuliko kisiasa. Aidha, majirani zetu sasa wanafanya juhudi za kushika hatamu katika nyanja za kiuchumi, hivyo kujiunga kwa nchi hizo katika jumuiya itakuwa na manufaa zaidi kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ujumbe ambao ninaunukuu kutoka kwenye taarifa ya Kamati ni ujumbe mzito sana ambao ninataka niunge mkono kwa vielelezo. Ibara ya 8 (3) ya mkataba ulionzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 1999, inasema: "Kila nchi mwanachama itateuwa Wizara ambayo itakuwa inashughulikia mambo ya jumuiya", lakini vile vile kuna Ibara ya 13 ambayo inazungumza kuhusu wajumbe kwenye Baraza la Mawaziri la Jumuiya na inasema, hao wajumbe wote wawe ni Mawaziri wanashughulikia masuala ya mahusiano ya huu ukanda. Vile vile, Ibara ya 48 inayounda

Bunge la Afrika Mashariki nayo inasema kutakuwepo Mawaziri watatu, mmoja kutoka Kenya, mwingine Uganda na mwingine Tanzania wanaoshughulikia *Regional Cooperation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema hapa, ni jinsi ambavyo wenzetu wa Kenya walivyo makini. Uganda wakamteuwa Mheshimiwa Marehemu Wapakabulo, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje ndio akaingia *Community* kusimamia masuala ya *cooperation* na sisi tukamtoa mwanadiplomasia wetu mashuhuri Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje akawa ndio anashughulikia masuala ya jumuiya. Lakini Kenya wakatushangaza wakamleta Waziri wa Viwanda na Biashara wakati huo alikuwa ni Nicolas. Sasa Watanzania hatukuelewa, Kenya tukawa tunasema hawa namna gani akili zao? Kumbe wenzetu jumuiya hii wanaiangalia kiuchumi kweli kweli. Kwa hiyo, tumekuwa na Mawaziri wa Nchi za Nje kutoka Tanzania na Uganda, Wakenya wakatuletea Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Kamati yetu ya Mambo ya Nje unaendana na sera ya Chama cha Mapinduzi ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambao ni sera ya diplomasia ya uchumi. Mimi nina uhakika sana kwamba kwa uwezo mkubwa wa kiutendaji na uelewa wa Mawaziri wetu wa Afrika Mashariki na Waziri wetu wa Mambo ya Nchi za Nje, matumaini yapo makubwa kwamba Tanzania itapiga hatua kubwa kwenye eneo hili, kinachohitajika ni sisi Wabunge kuwaunga mkono kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema katika hii ripoti kwamba majirani zetu sasa wanafanya juhudi za kushika hatamu, wameanza muda mrefu na sasa hivi kwa taarifa tu ya Bunge ni kwamba Kenya leo hii wanafikiria hata kuibadilisha Wizara yao ya Mambo ya Nje waite *Ministry of International Trade and Foreign Relations*, yaani Wizara ya Biashara ya Nje na Masuala ya Kimataifa kwa sababu kwao sasa hivi diplomasia ni uchumi peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kwa kifupi sana ukurasa wa tano wa Taarifa hii ya Mambo ya Nje aya ya pili ambapo wenzetu wanasema idadi ya Wawakilishi wetu nje ya nchi iendane na ukubwa wa maeneo wanayowakilisha na majukumu yanayowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sisi tunalegelega sana kwenye hili suala. Hivi majuzi mimi nilipata bahati kuwa Geneva kuhudhuria Mkutano wa *WTO* pamoja na Naibu Spika tukapata bahati kutembelea ubalozi wetu Geneva. Ubalozi wenyewe tu ukiungalia katika hali yake unajua hapa bado hiyo diplomasia ya kiuchumi haijashika kasi. Kwanza, jumla ya watendaji wapo watano pamoja na Balozi mwenyewe. Wanaoshughulikia masuala ya *WTO* tu ni maafisa wetu wawili wakati nchi nyingine zina maafisa 30 au 40, maana kila siku kuna mikutano zaidi ya mitano, kumi au kumi na tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala hatujalizingatia sana na ninadhani kuna umuhimu sana sasa hivi kutofautisha umuhimu wa Balozi zetu. Kuna Balozi

ambazo kwa kweli zinahitaji tuziangalie zaidi na Balozi nyingine tusizipe kipaumbele kiasi hicho. *(Makofi)*

Siyo sahihi! Sisemi kwa kudharau nchi yoyote, kwa kweli kumlinganisha Balozi wa *Geneva* na *New York* na Malawi au Burundi, sidharau, lakini ni kwamba hizi nchi zipo makini katika suala zima la uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na hoja iliyopo ukurasa wa saba ambayo ni hoja ya msingi kabisa. Wenzetu wanasema Tanzania iboreshe viwango vya elimu katika nyanja mbalimbali ikiwemo Ufundi, Lugha na Maadili ya Kazi ili kumudu ushindani wa kuwa kuna wasiwasi kuwa soko la ajira la pamoja likianza ajira nchini zitachukuliwa na wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nataka nisahihishe tu kidogo kwamba siyo kwamba kuna wasiwasi, ni kwa uhakika sisi tutakuwa kwenye hali mbaya sana. Tatizo la kwanza, kwa kweli tuna wimbi kubwa kweli Tanzania la vyeti feki ambavyo tusipoviangalia vitatupeleka mahali pabaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tumelewa na sifa ya *titles, titles* ambazo ni *empty* kama *Doctors, Masters* na kadhalika. Lakini kaa na huyo mwenye *Masters* na *Doctors* kwenye eneo lake ndiyo hapo tutakuja kukwama kwa sababu kwenye ushindani wa Afrika Mashariki huingii kijanjajanja. Ni kwa *panel* ya watu wanakaa pale kukusikiliza unajua nini kwenye hilo eneo, cheti hakitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili suala tuliongelee kwa nguvu na *seriously* kwa sababu hivyo vyeti vimepenya mpaka kwenye Vyuo Vikuu. Mimi nimeshtuka kusoma kitabu cha Chuo Kikuu kimoja hapa sitakitaja sasa hivi, lakini ukifika muda itabidi tuanze kukitaja. Wahadhiri Waandamizi ni *Graduates* wa Vyuo feki vinavyojulikana duniani, ni Vyuo vya intaneti. Sasa kweli hii itakuwa ni nchi gani? Kwa sababu Mwalimu kihiyo atazalisha wahitimu vihiyo na tukija kuwa nchi ya vihiyo ushindani utatokea wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana *Tanzania Commission for Universities,* imeanza kutoa matangazo kwamba jamani jiangalieni vyeti vyenu kwa sababu sasa hivi Tanzania nafikiri tumekuwa wa pili kwa Nigeria kwa vyeti vingi vya ajabu ajabu, pengine hilo tutaliongeleza wakati tunaongea kuhusu Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba tujiepushe na tamaduni za kilimbukeni. Utamaduni mmoja ambao umejitokeza hapa sasa hivi ni ule wa watoto wadogo hata wanaomaliza Chekechea kuvishwa yaani majoho ya kisomi. Huko tulikotoka joho la kisomi linavaliwa na mhitimu wa Chuo Kikuu tu wa Shahada ya Kwanza, ya pili au ya tatu na majoho hayo yakawa kichocheo kikubwa kwa watoto wetu wa madarasa ya chini, wanakuwa na hamu kwamba na mimi nije nivae hilo joho kwa kwenda Chuo Kikuu. Leo hii Chekechea joho na sherehe nzito. Sijui na sisi wazazi tukoje siku hizi! Tumekuwa wa ajabu ajabu tu! Darasa la saba joho na sherehe nzito, wengine mpaka na kupeleka kadi za michango, kadhalika darasa la kumi na mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga vichwani mwa watoto wetu fikra na dhana potofu kwamba hata elimu ya chekechea ni tosha, inastahili kupongezwa, hata elimu ya Darasa la Saba ni tosha inastahili kupongezwa. Hili Taifa kwa kweli tunakokwenda ni kugumu kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali tulivalie njuga hili suala, kwa kweli tunakokwenda huko na hizi sifa za vyeti zitatumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kengele haijanigongea kuniondoa, nataka kutoa mfano mmoja mdogo, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo yupo hapa kama shahidi yangu. Tumesimama kwenye *interviews* nyingi sisi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki zilizowahusisha Watanzania wengi, Wakenya na Waganda. Watanzania wanakuja nane na kati ya wale nane, watano wana *PhD* na wengine wote *Masters.* Lakini Wakenya watakuja wengine na digrii moja, *diploma* na kadhalika Waganda.

Sasa ikija kwenye *substance,* masuala yenyewe kuyajua wanashangaza! Wale wenye *diploma* wanajua zaidi kupita wale wenye *PhD.* Sasa hii jamani sijui tutakwenda wapi! Tukianza kuoneana aibu nchi hii tutatawaliwa na Wakenya baada ya siku tano au sita na wenzatu Waganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja zote mbili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe na sisi tunaomba kuungana na wewe kuwapa pole ndugu zetu wa huko Kyela wanaokumbwa na mafuriko na mvua kubwa ambazo zinaendelea.

Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Charles Muguta Kajege na Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah ajiandae.

**MHE. CHARLES MUGUTA KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kuchangia hoja ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje. Hivyo basi, nachukua fursa hii kuishukuru Kamati hiyo kwa kazi nzuri iliyoifanya kwa kutuletea taarifa nzuri iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna mambo ambayo nimeona katika taarifa ya Kamati hiyo ambayo nilitegemea yangeweza kuwa tumeletewa ingekuwa ni vyema zaidi. Suala la kwanza kwa mfano ni Umoja wa Forodha. Umoja wa Forodha umeundwa na ukaanza kufanya kazi tarehe 01 Januari, 2005.

Kwa hiyo, sasa hivi ni mwaka wa tatu na ili kuingia kwenye umoja wa forodha ulio kamili *(full fledged customs union)* tuna miaka ambayo inakuja, yaani kufikia mwaka 2010 ndiyo inakuwa *full fledged customs union.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwamba pamoja na Taarifa ya Kamati hii, tungeelezwa kwamba hii *Customs Union* inaendeleaje au kuna changamoto zipi ambazo tunakutana nazo na kwa upande wa Tanzania tunazikabili vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kuhusiana na ngazi mbalimbali za majadiliano ambayo yanaendelea sasa hivi katika sekta mbalimbali. Nimepata bahati kabla ya kujiunga hapa Bungeni, nilikuwa nikifanya kazi za Mambo ya Nchi za Nje wakati huo ambao ndiyo ilikuwa inaratibu masuala yote ya Afrika Mashariki na nilishiriki sana kwenyebaadhi ya vikao katika ngazi ya maafisa na vilevile nikahudhuria mikutano ambayo ilikuwa ikiendeshwa na Makatibu Wakuu.

Katika majadiliano kuna mambo mengi ambayo yanafanyika na hasa katika ngazi za Maofisa na Makatibu Wakuu, kuna mabishano yanatokea mpaka kuja kufikia muafaka mara nyingi inakuwa ni shida. Sasa nilitegemea kwa mfano Kamati hii ya Bunge angalau ionyeshe jinsi gani majadiliano yamefanyika katika baadhi ya sekta ili sisi Wabunge hapa tuweze kujua ni kitu gani kinaendelea.

Suala lingine ni sakata la Wabunge wa Bunge la Kenya ambao walitakiwa kuingia katika Bunge la Afrika Mashariki. Tumekuwa tukisikia katika Vyombo vya Habari lakini hatuna hatupati taarifa rasmi kutoka kwa wenzetu aidha Wizara ya Uhusiano wa Afrika ya Mashariki, hivyo nilitegemea kwamba Kamati hii na sisi itueleze ni kitu gani kinaendelea na tuweze kujua kwa undani zaidi kuliko kusikia kwenye Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki jukumu lake kubwa kama ilivyoonyeshwa katika Taarifa ya Kamati ni kuratibu na kusimamia mchakato wa muungano *(integration process)* katika Afrika Mashariki. Sasa mimi nilitegemea kwamba tuone kwa mfano ni jinsi gani na ni changamoto gani kama Wizara inapata na ni namna gani imeweza kutatua au ni namna gani Serikali inatakiwa isaidie kuweza kukabiliana na majadiliano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Kamati hii ituletee taarifa ambayo itakuwa inazingatia mambo ambayo yanafanywa na Wizara hii katika kikao kingine kama tutakuwa na wakati wa kujadili Taarifa ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kwamba kama hatuelezwi jinsi mchakato unavyoendelea, itakuwa ni vigumu kwetu sisi Wabunge kwa sababu wiki iliyopita ilikuwa sisi Waheshimiwa Wabunge hapa tujadili kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki, sasa kama hatuna taarifa kama Wabunge majadiliano yanavyokwenda, changamoto zilizopo kule na mwelekeo wenyew,e sisi Waheshimiwa Wabunge tutaegemea katika nini kuweza kutoa mchango madhubuti katika hoja hii nzito ya kujiunga na Shirikisho la Afrika Mashariki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Kamati hii ili iweze kujua kabisa ni kitu gani kinaendelea katika majadiliano ijikite katika kutafuta au kuletewa taarifa za Kamati za Wataalam, yaani Maafisa katika Serikali zote tatu yaani Kenya, Uganda na Tanzania na sasa hivi itaingia Burundi na Rwanda. Majadiliano yale yanaonyesha ni namna gani, kuna

ugumu gani na ni kitu gani kinachotakiwa kufanyika. Sasa inapokuja hapa Kamati inatuonyesha kwa uwazi kwamba hali halisi iko hivi na kwa hiyo, sisi changamoto tulizonazo ni hizi na hivyo namna ya kuzitatua ni lazima tufanye namna hii.

Hivyo, kwa upande wa Taarifa ya Mchakato mzima, hayo ndiyo baadhi ya mambo muhimu ambayo yangekuwepo kwa sababu sasa hivi tunatakiwa tuanze mchakato kuhusiana na soko la pamoja. Soko la pamoja pamoja na mambo mengine litaruhusu wananchi wa nchi zote za Jumuiya kuweza kwenda katika nchi yoyote na kuishi, kufanya kazi katika zile nchi na mambo mengine mengi ambayo ni makubwa. Sasa bila kufahamu maendeleo katika hizi hatua nyingine za mwanzo hasa katika Umoja wa Forodha itakuwa ni vigumu sana sisi kufanya uamuzi ambao ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine sasa nazielekeza katika Wizara yenyewe ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kuna taarifa kuhusiana na Viza za Uingereza. Kwa mtu yeyote ambaye amewahi kwenda kwenye Ubalozi wa Uingereza kuchukua Viza, kwa kweli ni kero kubwa. Katika Taarifa ya Kamati hii, ni kama na wao wanalalamika.

Sasa mimi nilitegemea kwamba, kabla ya kuleta taarifa hapa Bungeni, hii Kamati kwa vile ilikwishakutana na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, ingekuja na mapendekezo ya namna gani Serikali yetu ifanye au Wizara imekwishaipatia taarifa hii utaratibu au hatua ambazo itachukua ili kuweza kuwatendea wananchi wetu haki badala ya kuwasimamisha kwenye mstari kuanzia saa 4.00 usiku mpaka saa 12.00 asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili mimi ningeshauri vilevile Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje iliangalie hili suala kwa mapana, siyo Ubalozi wa Uingereza peke yake, pia kuna Ubalozi wa Marekani. Ni vyema Wizara ikasema waziwazi kwani tunatambua kabisa kwamba Tanzania ni nchi masikini, lakini wanapokuja hapa Tanzania ni lazima watutendee haki na heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ni Kituo cha Diplomasia *(CFR)*. Kituo hiki kama taarifa inavyosema, kiliundwa mwaka 1986. Nafikiri nyuma ya hapo, lakini kuanzia mwaka 1986. Msumbiji ni kama imejitoa na kuanzia mwaka 1986 kila nikisoma ripoti naona kama Serikali yetu inalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sioni kama tupo makini kuhusiana na hili. Kuanzia mwaka 1986 Msumbiji imejitoa, Msumbiji haihusiki na chochote na hiki Chuo na bado tunasema kwamba ni Chuo cha Ushirikiano kati ya Tanzania na Msumbiji.

Sasa nilikuwa nashauri Serikali yetu ifanye uamuzi mkubwa, aidha Chuo tukichukue moja kwa moja tukijua kwamba ni cha Watanzania. Lakini mpaka sasa hivi unagharamiwa na Watanzania. Wanafunzi wote wanaosoma pale nafikiri asilimia 99 ni Watanzania. Fedha wanapata kupitia Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje. Sasa tukisema kwamba bado kiko chini ya Msumbiji, nafikiri tunajidanganya. Kwa hiyo, naomba kwamba labda Wizara ifanye utaratibu wa kuweza kukifanya kiwe Chuo cha Kitanzania badala ya kusema kwamba ni Chuo cha Msumbiji na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hati miliki ya majengo ya Ubalozi wa Tanzania yaliyopo Msumbiji. Majengo haya tulipewa na Hayati Samora Machel wakati ule akiwa ni Rais wa Msumbiji baada ya kupata uhuru. Lakini tangu wakati huo mpaka leo hii kweli majengo hayo hayana hati miliki ya kuonyesha kwamba ni mali ya Tanzania na kwa muda wote hata katika ripoti za kila mwaka za Wizara ya Mambo ya Nje tumekuwa tukilalamika kwamba hatupati na hakuna hatimiliki. Sasa tufanye nini ili tupate hatimiliki?

Mimi nafikiri kwamba kuleta tu ripoti katika Bunge hatuwezi kupata hatimiliki. Nashauri kwamba ni vyema sasa hivi tupeane muda kwamba kutokea sasa hivi mpaka lini tuwe na hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni lazima tuangalie, wakati majengo haya tunapeana, uongozi wa juu wa Msumbiji ulikuwa ni ule wa wapigania uhuru na kizazi hiki karibu kinakwisha.

Sasa hivi kuna Mheshimiwa Gebuze ambaye naye amekaa Tanzania, lakini nina uhakika labda baada ya Gebuze hakutakuwa na kiongozi mwingine wa Msumbiji ambaye amewahi kukaa Tanzania.

Sasa na haya ya kupewa majengo sidhani kama kuna hati ya kupewa haya majengo, labda tulipeana kwa maneno, sasa itakapokuja kufika wakati huo, wakati kiongozi Msumbiji ni wa kizazi cha sasa hivi ambaye hakupigania uhuru wala hakuwahi kukaa Tanzania, itakuwa ni vigumu sisi kupata hatimiliki ya haya majengo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali yetu kwa wakati huu ambao bado kiongozi wa Msumbiji anafahamu suala zima la haya majengo akiwa bado madarakani ni vyema tufuatilie kwa ukaribu zaidi ili tuweze kupata hatimiliki za majengo ambayo tumepewa na Msumbiji.

Lakini vilevile nakumbuka kwamba nilipokuwa Msumbiji Serikali ya Msumbiji vilevile imewahi kulalamika kwamba kuna majengo ambayo Serikali ya Tanzania iliwapatia na bado hayana hati miliki. Kwa hiyo, hii yote ni lazima iwe *two way traffic,* hatuwezi tukalalamikia hatimiliki ambazo hatukupewa na Msumbiji wakati sisi wenyewe hatujatoa hatimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yetu ifuatilie kwa karibu kabla hatujachelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naona nilikuwa nimesahau ni kuhusiana na Wizara ya Afrika Mashariki. Hii ni kuhusiana na Kamati inayokusanya maoni ya wananchi. Mara kadhaa kupitia Vyombo vya Habari, wananchi wamelalamika kwamba imekuwa inawashawishi wananchi kutoa maoni yanayopendelea kuwepo kwa shirikisho. Mimi naona hiyo sio haki kwani kazi ya Kamati hii ni kukusanya maoni na wala siyo kushabikia matokeo ya hayo maoni. Kama Profesa Samuel Mwita Wangwe na Kamati yake wameshindwa, basi mimi naomba Serikali iwabadilishe hawa watu kwani wanatupeleka pabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba wafanye kazi kulingana na hadidu za rejea ambazo wamepewa na Serikali yetu na wala sio ambazo wanatoa kwenye *briefcase* zao na kuzi-*pursue*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo machache na mimi naomba kuunga mkono hoja zote mbili, yaani ya Katiba na hii ya Mambo ya Nchi za Nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Charles Muguta Kajege. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah na kama muda wetu utakuwa umekaa sawasawa, msemaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo kwa kuwa tutatakiwa tuwasikilize watoa hoja na baadaye huenda tukawa na hoja binafsi. Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah karibu!

**MHE. JUMA HASSAN KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Lakini awali ya yote nami niungane na wachangiaji waliopita kutoa rambirambi kwa kifo cha aliyekuwa Waziri wa Afya wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Mzee wetu Dr. Aaron Chiduo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi. Nawapa pole wafiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda labda nilijulishe Bunge hili Tukufu kwamba, mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje. Katika hili, nitatumia nafasi fupi sana kuchangia mchango wa Kamati ya Mambo ya Nje iliyoletwa mbele yako kwa sababu tu naamini yote yaliyowasilishwa kupitia Mwenyekiti wangu naamini yote yapo sawasawa na yamewasilishwa kama tulivyojadili katika Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie kwa kifupi sana suala la diplomasia ya kiuchumi. Hili suala la diplomasia ya uchumi ni nyenzo muhimu sana kwa nchi yetu Tanzania kwa sababu tunaamini kwamba tunapokuwa na Balozi nje ya nchi, moja ya majukumu makubwa ya Balozi zetu ni kutuwakilisha juu ya mambo mbalimbali ili kuweza kuiharakisha nchi yetu iwe katika maendeleo na kuwaondolea wananchi wetu umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, moja ya kazi tulizozifanya sisi kama Kamati na tuliyoyaona ni juu ya vipaumbele na namna ya Balozi zetu zinavyochukuliwa. Bado inaonyesha wazi kabisa kwamba Balozi zetu pengine zinawakilisha kwa masuala ya kisiasa zaidi na sio masuala ya kiuchumi. Wakati Mwenyekiti wa Kamati anawasilisha taarifa, ameeleza Kamati yetu moja ya kazi ilizozifanya na imetembelea sehemu mbalimbali. Katika kutembelea sehemu hizo, Kamati imejionea mambo mbalimbali ambayo pengine kwa namna moja ama nyingine pengine hayapewi kipaumbele pengine tu kuangalia namna ya Balozi wetu wanavyofanya kazi kiumaskini wanapokuwa kule nje ya nchi na wanavyoiwakilisha nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni katika nchi za *Scandinavia*. Pale tuna Balozi mmoja ambaye anawakilisha zaidi ya nchi nne, naye ni Balozi Ben Moses. Yeye

yupo *Stockholm*, *Sweden*. Sasa ukiangalia, Balozi Ben Moses anavyoweza kufanya kazi na idadi ya wafanyakazi aliotuambia ana wafanyakazi wasiozidi kumi na mbili, sasa uwezo wa kuziwakilisha nchi zile na ukubwa ulivyo kwa kweli inamuwia vigumu sana na hata Mabalozi wetu kwa kweli wanashindwa kuweza kuitangaza nchi yetu kwa hali na mali ili tuweze kuhakikisha kwamba pengine katika hali ya kutuondolea umaskini, pengine angeweza kuitangaza na tukaweza kupata misaada zaidi. Kwa hiyo, kile kidogo tunachokipata ni uwezo wake ule anaoweza kuufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati kwamba upo umuhimu kutilia mkazo katika kuhakikisha kwamba tunaziimarisha Balozi zetu.

Sambamba na hii, tunao ubalozi mwingine wa Japan. Tuna Balozi wa Japan anayewakilisha nchi za New Zealand na pia anawakilisha nchi ya Australia, kote nako kunahitaji nguvu ya kutosha ili tuhakikishe kwamba Balozi wetu anafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Kadhalika Balozi wa Ujerumani ambaye ana jukumu la nchi za *Belgium* pamoja na *Holland* napo vilevile kwa dhati kabisa bado panahitajika nguvu za kutosha kwa sababu naamini kabisa kwa kutumia nchi hizi za wenzetu ambazo zimeendelea, basi tunaweza kujipatia mambo mbalimbali kama wawekezaji na misaada mbalimbali. Kwa hiyo, ipo haja Balozi hizi zikaongezwa nguvu ili ziweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie tu kwamba moja ya jukumu kwa Kamati yetu, kubwa zaidi ni kujua masuala mbalimbali ya nje, lakini tumekuwa tukihoji au Wajumbe wa Kamati wamekuwa wapo nyuma sana na masuala ya nje pengine kwa kutokueleweshwa vizuri. Sasa ni wajibu na tulisema kwamba lazima tukaweka mkazo, tukasema kwamba Kamati hii ipewe kipaumbele na iheshimiwe ili ihakikishe kwamba kila kinachotendeka nje basi ni lazima tupewe taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo labda nasema kwamba Kamati hii inaweza ikawajibika na masuala ya Bunge la Afrika Mashariki, lakini tuna Mabunge mengine ambayo yanatokana na Bunge letu hili Tukufu, Bunge kama la *SADC* lakini haliripoti katika Kamati yetu, Bunge la Afrika haliripoti katika Kamati yetu na hata Wawakilishi wa *CPA* nao vilevile hawaripoti katika Kamati yatu na hata *PAN AFRICA* na kadhalika. Kwa hiyo, ipo haja sasa kwamba Kamati kwa sababu inashughulika na mambo ya nje ikapewa jukumu la moja kwa moja na ikapata uelewa wa kutosha juu ya masuala ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni kwamba, tulikutana na wafanyakazi wa Wizara na moja ya mambo wakatuambia kwamba Rais wetu toka amekuwa akisafiri hizi safari amekuwa akisafiri safari ambazo zinaitwa *Official Visits* siyo safari za *State Visits* ambazo zinatokana na mwaliko wa nchi nyingine. Lakini ili kuokoa raslimali ya nchi yetu na kwa sababu nchi yetu ni maskini sana, bado tunaona misafara mikubwa sana kwa safari za nje.

Kwa hiyo, tunachoomba, tulisema tu kwa nia njema na kwa kuweza kuhakikisha kwamba ili tuzitumie raslimali zetu kwa mahali ambapo pengine kuna watu wengine wanakwenda nje, pengine wanaweza kuwa wamejumuishwa kwenye msafara wakiwa kazi ni kuandika vocha tu lakini mlipaji ni mtu mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulisema kabisa kwa nia njema katika Kamati kwamba tunaomba sasa safari za namna hii kama za Rais zipunguziwe misafara mizito mizito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja zote mbili na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah kwa ushirikiano. Naomba nimwite Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ili na yeye aweze kutoa mchango wake.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Natambua muda umekwenda, kwa hiyo, nitaongea kwa haraka na kwa kifupi sana.

Awali ya yote, kwa niaba ya familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo, akiwa ni Mjomba wangu, naomba niwashukuru wote kuanzia Spika na Wabunge wote kwa msaada wenu wa hali na mali, kwa kweli mmejitokeza kwa wingi kwenye mazishi jana. Ninawashukuru sana na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na mengi, lakini kwa sababu najua sina zaidi ya dakika kumi, basi labda niseme yale ambayo naweza kuyasema. Katika taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, zaidi nitajielekeza kwenye taarifa hiyo kwa sababu ndiyo Kamati yangu na mengi yalikuwa yanahitaji kuongezewa ingawa yote yameelezwa, lakini naona niweke mkazo .

Suala kubwa la uteuzi wa mabalozi, sisi kama Kamati tunasema kwamba wazingatiwe wenye taaluma na uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, sijaota ndoto ambayo Mheshimiwa Chrisant M. Mzindakaya alizungumza. Kwa hiyo, itabidi tu mnisikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuta kwamba kwenye Balozi zetu Mabalozi wanaoteuliwa kwanza unakuta mtu amefikia umri wa kustaafu anapelekwa Ubalozi, au mtu amefanyafanya mambo hapa ambayo kwa akili za kawaida unaona kwamba huyu mtu amevurunda, anapelekwa Ubalozini, mtu anapelekwa ili akapumzike. Lakini kuna watu ambao wanastahili kweli.

Sasa mimi nilikuwa nasema na mara nyingi nilishawahi kulisema hata kwenye Kamati kwamba ninaomba basi, kama itawezekana kama nchi nyingine wanavyofanya uteuzi wa wale watu muhimu kama hawa Mabalozi uletwe hapa Bungeni ili tuuthibitishe. Siyo kazima iwe Bunge, kama inaonekana Bunge pengine itakuwa mlolongo mkubwa, basi hata kwenye Kamati ya Mambo ya Nje kwa niaba ya Bunge. Lakini hili nimeliona ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba unakuta kuna Mabalozi ambao wamebobea kwenye Balozi hizi miaka 17, Balozi anahama hapa, anakwenda hapa anaunganisha tu, jamani! Mimi nilikuwa nafikiria kama ilivyo kawaida ambavyo miaka minne wanarudi nchini, basi warudi, wakae wazoee na shida za hapa na raha za hapa halafu tena uende ukiwa na akili mpya. *(Makofi)*

Lakini vilevile ninaomba kuwe na umri wa kustaafu Ubalozi hasa kwa wale Mabalozi wanaoteuliwa kisiasa, pawe na umri wa kustaafu, maana yake unaambiwa yupo tu, yupo tu! Vijana wanakaa mpaka wanakuwa *frustrated.* Wengine wanapewa vyeo vya Ubalozi lakini utashangaa wako kwenye *corridor* za Mambo ya Nje miaka nenda rudi mpaka wanastaafu.

Kwa hiyo, kwa kweli nilikuwa nasema, Waheshimiwa Wabunge wenzangu kama tutakubaliana angalau tutoe hoja kwamba majina ya watu hawa yakishapendekezwa huko, basi yaletwe kwetu na sisi tuweze kutoa maoni yetu kama tutakuwa hatuingilii kazi ya mtu.

La pili, ni suala la bajeti ya Bunge. Kwa kweli nimefurahi sana kwa sababu wametoa mfano mzuri wa Kenya. Mimi binafsi na Kamati tulikuwa tunasema kwamba ikishaidhinishwa na sisi tufanye kama wenzetu. Mbona mambo mengi ya Jumiya ya Afrika Mashariki tunayapeleka mbio, tunakwenda sawa na wenzetu! Mbona mengi kama haya nyeti tunayaacha ambayo ni muhimu! Kwa sababu kama hili, mimi naona kabisa kuna haja na sisi bajeti yetu tuibadilishe, maana yake mtashangaa kama mmewahi kusafiri safari za nje ya nchi za Bunge, utakuta ule Waraka unaotumika umeandikwa Waraka wa Watumishi wa Umma, wakati sisi siyo watumishi wa Umma.

Kwa mfano, nilikwenda Uingereza kwenye Kikao cha *CPA, simply* kwa sababu walikuwa wanalipa malazi na chakula, tulipewa kitu kama *dollar* 200. Unafika pale unashindwa hata kuwapa wenzako *offer.* Waheshimiwa Wabunge wengine wanashangaa, lakini yote haya yanatokana na kwamba sisi tunatumia Waraka ambao siyo wa kwetu. Kwa hiyo, kwa kweli mimi nadhani hata mwaka huu wa fedha unaokuja tungeanza hivyo ingekuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia, hususan Mheshimiwa Charles Kajege amesema kuna taarifa nyingi ambazo walitegemea zitoke kwetu. Ndugu zangu, hata sisi wenyewe tunapata shida kupata hizo taarifa. Wakati mwingine inabidi tufuatilie, tuombe na tuombe ili tuweze kupata hizo taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona imefika wakati kuona kwamba ni muhimu taarifa ziletwe hapa Bungeni. Kwa mfano, sasa hivi ukiuliza suala la Maziwa Makuu, tuanze tu na Waheshimiwa Mawaziri, kuacha Waheshimiwa Wabunge, ni nani anajua suala la Maziwa Makuu ni nini na wameazimia nini? Sisi wenyewe tukiulizwa masuala ya Umoja wa Afrika*,* nani anayejua ni nini? Kwa hiyo, suala hili limekuwa kama ni siri, kama ilivyo kwenye Mikataba kwamba kinachoamuliwa ni siri, basi na hili nalo limekuwa ni siri kwa muda mrefu. Labda ni kwa makusudi au kwa uzembe. Lakini mimi

ninashauri ni vyema kabisa masuala haya, sisi Waheshimiwa Wabunge tukawa tunaweza kuyazungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda haraka haraka, kwa hiyo, mengine ninayaruka. Lakini nije kwenye suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jumuiya ya Afrika Mashariki inasemekana kwamba ni ya watu. Lakini tatizo kubwa ambalo limekuwepo, hao watu wenyewe hawajui ni kitu gani. Sasa utashangaa kila unapouliza unaambiwa hakuna fedha za uhamasishaji. Nadhani moja ambalo lilitufanya mimi na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe kuondoka huko ni hilo, tuliona kwa sababu tumeishajua upungufu wake tuje huku tusaidiane na ninyi tuweze kuweka changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini utashangaa hili zoezi la shirikisho ndugu zangu, tunaomba tunyamaze tu hivi hivi kama Kamati. Mkijua gharama ambazo wanatumia Kamati ya Kukusanya maoni, ahaa, itakuwa habari nyingine. Sasa ikiwa tuna fedha za shirikisho, hao watu wanakwenda kuhojiwa ni akina nani. Mimi kwa mfano, leo nimepata barua naambiwa tarehe 21 mpaka 23 watakuwa Kilindi, mtu mmoja akanipigia simu akaniuliza hivi mama tunaandaa viongozi wa Chama au tunawaandaa nani? Hawajui ni kitu gani!

Tunatumia mabilioni ya fedha kwenda kuhamasisha watu kwa kitu ambacho hawakijui. Hizo fedha tungezichukua zikasaidia katika uhamasishaji tukampa hata Mheshimiwa Mbunge hili fungu la mafuta aende akahamasishe kuhusu masuala ya Afrika Mashariki ingekuwa jambo jema zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashauri sana bajeti ya Afrika Mashariki inayokuja ndugu zangu hata hapa ilipo sasa hivi tulivyoona *ceiling* ni kidogo mno. Naomba tushirikiane wapewe fedha za kutosha kuendesha shughuli zao, siyo tu uhamasishaji, nenda kwenye Ofisi ya Afrika Mashariki, ni ile tu kwamba amewekwa Waziri na watu wachache, lakini ni kitu kingine. Kwa hiyo, mimi naomba sana ushirikiano wenu kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ambalo nataka kusemea ni kuhusu Ofisi za Balozi zetu. Kwenye hizo Ofisi, Balozi tunazokwenda ndugu zangu kwa kweli hali inasikitisha kama ambavyo wenzangu wamekwishakulisemea, sitaki kulirudia. Lakini utashangaa hapo hapo tunajaribu kufungua Ofisi za Balozi nyingine.

Kwa mfano, tuko kwenye *AU* sasa hivi, unakuta nchi 13 za Afrika Magharibi zinahudumiwa na Ubalozi mmoja wa Nigeria. Kwa sababu *AU* inahimiza mashirikiano yetu. Tufungue hata Balozi nyingine mbili! Tunakwenda kufungua ofisi ya Ubalozi *Brazil*, tunakwenda kufungua ofisi ya Ubalozi sijui wapi. Mimi kwa kweli nilikuwa nasema, kuna haja pia kuweka *priorities* zetu na ili ziwe *priorities* sawa, nilikuwa naomba dhidi ya haya maamuzi mengine tuje tushirikishwe Bungeni hata kama siyo ndani ya Bunge kama Mkutano pale kwenye ukumbi wa Msekwa ili tuweze kutoa mawazo yetu kama Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilikuwa na mengi, lakini niseme kwa sasa yanatosha hayo. Ninaunga mkono hoja zote mbili. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Beatrice nakushukuru sana msemaji wetu wa mwisho. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaanza kuwaita watoa hoja ili waweze kuendelea kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizozungumziwa na Waheshimiwa Wabunge, nitawaomba tutumie utaratibu wa kuiomba Serikali ijibu maneno yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, ni maneno mazito na labda Serikali ingeweza kusema neno fulani au kuweka ahadi katika hayo yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, nitawaomba Waheshimiwa Mawaziri kwa utaratibu ufuatao, nitamwomba kwanza Mheshimiwa Balozi Iddi Seif - Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa nimpe angalau dakika kama tano azungumze. Halafu nitamwomba Mheshimiwa Mathias Chikawe - Naibu Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria, halafu nitamwita Dr. Diodorus Kamala - Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, lakini kabla sijawapa nafasi Wenyeviti wetu wakahitimisha hoja zao, nitamwomba pia *Chief Whip* kwa kuwa kuna maneno mazito yaliyozungumza yanayohusu Ofisi ya Waziri Mkuu yakihusisha masuala ya Bunge, naye nitampa muda mfupi aweze kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge maneno yaliyoyasemwa hapa ndani.

Waheshimiwa Wabunge, lakini naomba niseme mambo mawili. Ni haya yafuatayo: Katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, yamejitokeza mambo mawili mazito sana.

La kwanza, Mheshimiwa Stephen Galinoma amelalamika kwamba Waheshimiwa Wabunge hawapewi gazeti la Serikali ili kujua mambo yanayoendelea na kuweza kujiandaa na kufahamu vitu vingi vinavyotakiwa. Naomba tu niendelee kuwapa taarifa kwamba Bunge limekuwa likishughulika kutafuta nakala hizo za gazeti la Serikali na mara zote tumekuwa tukigawiwa na kuwekewa katika maeneo yenu mnayotunzia barua zenu. Kwa hiyo, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge mwendelee kupitia yale maeneo yetu na kuchukua.

Waheshimiwa Wabunge, la pili, ninaomba niwape taarifa kwamba suala la Shirikisho la Afrika Mashariki ni nyeti sana na ninaomba niwatangazie kwamba Mheshimiwa Spika, amewasiliana na Wizara husika na hivyo tarehe 21 Aprili, 2007 tutakuwa na kazi moja tu Waheshimiwa Wabunge kupatiwa semina maalum ya kufahamu kwa undani suala hilo la Shirikisho la Afrika Mashariki. Kwa hiyo, nitawaomba wote tuwe tayari na ili tuweze kupata uelewa wa kutosha kuhusiana na suala hilo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba nimwite Mheshimiwa Balozi Iddi Seif aanze kujibu hoja. Halafu na Mheshimiwa Mathias Chikawe ajiandae.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa taarifa yake iliyojieleza vizuri na kueleweka. Kutokana na taarifa hii napenda kutoa mchango wangu mdogo katika yafuatayo:-

Kwanza kuhusu soko la pamoja la ajira iwapo Shirikisho la Afrika Mashariki, je, ili kulinda ajira za raia wa kila nchi kwa kiwango fulani (asilimia fulani, mathalani asilimia 40), hakuna uwezekano ikapendekezwa na kukubaliana kwa nchi zote za shirikisho kwamba soko la ajira lisizidi asilimia 60 raia wa kutoka nje ya nchi nyingine? Je, upo uwezekano wa kuzishawishi nchi nyingine kukubaliana katika jambo hili, ili kuepusha nchi mojawapo iliyo nyuma katika kiwango cha elimu cha wananchi wake wasipokonywe nafasi zote za ajira? Kamati ina maoni gani kuhusu suala hili. Suala hili likiachwa holela Tanzania ni nchi mojawapo itakayoathirika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya maji ya Ziwa Victoria, napenda kufahamu kama kuna *self regulating mechanism* ya kuzuia nchi mojawapo kujiamulia kutumia maji ya Ziwa Victoria juu ya kiwango kilichokubalika na kukiuka makubaliano ya kiwango kinachokubalika kwa nchi kutumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kuwa nchi fulani imefunga mtambo wa umeme ambao unatumia maji ya Ziwa Victoria kwa kiwango kikubwa, kiasi kwamba kimeathiri hata *level* ya maji ya Ziwa hili na kuziathiri nchi jirani. Je, Kamati iliweza kubaini sababu zipi zilizoiwezesha nchi hiyo kuanza mradi huo uliochukua muda mrefu kuutekeleza hadi mwisho, bila nchi nyingine kufahamu mapema na kuweza kuwazuia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inapata mafundisho mawili katika suala hili:-

(a) Inaonyesha hakuna utaratibu madhubuti wa ncho moja (ku-*monitor*) kuratibu mwenendo na ufuatiliaji wa vitendo vya kila nchi katika masuala yaliyokubalika chini ya dhana ya ushirikiano. Hili halina budi liwekewe mkakati maalumu.

(b) Pamoja na nchi shirikisho kukubaliana mambo mbalimbali chini ya mkataba wa makubaliano, zipo nchi ambazo zitaweza kwa makusudi mazima na ujasiri, kukiuka makubaliano kwa maslahi binafsi ya nchi hiyo. Ni dalili za aina hii ndizo zinazowapa wananchi wengi wasiwasi wa kukubali kuharakisha uundwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki. Je, ni njia zipi zitatumika kuzuia uvunjaji wa uaminifu wa aina hii jinsi Shirikisho likishaundwa lisije likalazimika kuvunjika tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Kamati iwasilishe hoja zetu Wabunge kwa umakini mkubwa kwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ili kuhakikisha kuwa ustaarabu,

uvumilivu na urahimu wa Watanzania kwa watu wa nchi zote jirani, wasiutumie vibaya kwa kutupiku kijanja kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuamini Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, itatuwakilisha ipasavyo, naunga mkono hoja.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati hizi mbili kwa kazi nzuri na taarifa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ningependa kuchangia kuhusu *TASAF.* Nafarijika kwamba miradi ya *TASAF* inasaidia sana wananchi kutekeleza miradi yao mingi ya jamii.

Hata hivyo, urasimu mkali na ucheleweshaji mkubwa wa kufikisha fedha ni kero kubwa na hali hizo zinakatisaha tamaa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, ningependa kuchangia yafuatayo:-

Kwanza, Diplomasia ya Uchumi, nia njema ya Tanzania kuwekea mkazo Diplomasia ya Uchumi haina budi kuambatana na utekelezaji thabiti. Hapana budi Balozi zetu zikiwa na wataalamu wa kutosha wenye kiwango cha elimu na uzoefu wa kutosha katika fani za biashara na uchumi.

Aidha, wataalamu hao wapewe vitendea kazi na malengo thabiti pamoja na motisha za kuwawezesha kuzikabili ipasavyo changamoto za kukuza biashara na uwekezaji wenye ushindani mkali wa utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi na ubora wa wataalamu ni muhimu katika Balozi zetu hasa zile zinazoshughulikia *Multilateral Diplomacy* kama vile *Geneva, Brussels, UN New York* na *London* kuwa na wataalamu waliobobea na wenye upeo mkubwa ili kumudu kwa ufanisi unaostahili mambo mengi na mazito yanayojadiliwa katika Balozi hizo. Zaidi ya kuwa na wataalamu wengi kutosheleza mahitaji makubwa yaliyopo, kuna umuhimu wa kuwaacha wataalamu wetu wanaokuwa katika Balozi hizi wawe na vipindi virefu zaidi ili uzoefu wao endelevu uweze kuleta tija na mafanikia makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kuwa na mtazamo thabiti na maandalizi ya kutosha kwa Tanzania kwa ujumla na hasa kuwaandaa wananchi wetu kufaidika ipasavyo katika kushiriki kwetu katika Jumuiya hiyo iweze kuwa na manufaa yanayotarajiwa. Vile vile utata kuhusu Tanzania kuwemo *SADC* na Kenya kuwemo *COMESA* hauna budi upatiwe utatuzi ufaao mapema iwezekanavyo, vinginevyo tutakwama baada ya muda si mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bajeti, naunga mkono umuhimu wa Kamati za Bunge na Bunge lenyewe kuwa na Bajeti za kutosha na uhakika ili ziweze kufanya kazi zao kwa uhakika na kwa ufanisi unaotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote mbili na kuishauri Serikali yetu iyakubali na kujitahidi kuyatekeleza kadri inavyowezekana.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa mchakato unaoendelea kuhusu hoja ya kuunda Shirikisho la Afrika Mashariki Watanzania walio wengi wamekata tamaa hata kabla shirikisho hilo kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanaogopa nini? Walio wengi wanaogopa ajira nyingi zitaenda Kenya na Uganda na wao kukosa. Dhana ya kujiamini kwamba na wao wanayo elimu ya kutosha kukidhi ushindani na wenzetu wa Kenya na Uganda, napendekeza Watanzania wasikate tamaa, bali na wao wajielimishe ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walio wengi wana hofu pia kuwa ardhi yetu itaporwa na wananchi wa Kenya na Uganda. Hii inatokana na tabia yetu ya kutojali uzalendo. Nikisema uzalendo sina maana ya ubaguzi kwa misingi ya uzawa bali nina maana ya *nationalist.* Watanzania wana hofu kuwa ingawa sheria inasema wazi kuhusu umilikishwaji wa ardhi kwa wazalendo bado tumeendelea kuwapa wageni ardhi bila kujali sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Diplomasia ya Kiuchumi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, imejikita katika utekelezaji wa Diplomasia ya Kiuchumi. Hapa Serikali ina nafasi nzuri sana katika kuitangaza nchi yetu kiuchumi kupitia Balozi zetu. Suala la kupata wawekezaji wa mashamba makubwa, viwanda kupitia *EPZ,* nchi kadhaa za Afrika zimeanza siku nyingi mipango ambayo sisi tunaanza leo. Kwa mfano, nchi ya Mauritius ambacho ni Kisiwa, kina uwezo wa kuzalisha sukari mara sita ya Tanzania ingawa hawana ardhi kubwa kama sisi. Mipango ya *EPZ* kule imeanza mwaka 1988.

Katika Ilani ya Uchaguzi tumeahidi kuwa Serikali itatilia mkazo kuwavutia wawekezaji katika kuwekeza kwenye mashamba makubwa, katika miaka mitano hii. Ofisi za Balozi zetu, zinaweza kuwa kitovu cha kuwashawishi wawekezaji kuja kuwekeza hapa nchini.

Kuhusu utendaji kazi wa Bunge, Wabunge wa Tanzania wanafanya kazi chini ya maridhiano ya mfumo wa Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola. Karibu nchi zote za Jumuiya ya Madola wana mfumo wa kufanya kazi ya Ubunge kwa kutambua kuwa Wabunge au Bunge ni mhimili kama ilivyo Serikali na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Constituency Development Allowance (CDF) or Fund,* karibu kila Bunge la nchi za Jumuiya ya Madola inawalipa Wabunge wake mfuko huu wa maendeleo ya Jimbo. Bunge la Tanzania nalo linapaswa kulipwa posho hii kwa manufaa ya maendeleo ya jimbo la Mbunge husika. Namna gani *fund* inaweza kulipwa, Serikali inaweza kutembelea nchi ya Kenya au Uganda.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni nzuri na imechambua mambo muhimu. Hata hivyo, katika kusisitiza lugha ya Kiswahili, kwa mfano, hapa Bungeni kuwepo vifaa vya ukalimani ili viweze kutumika hasa tunapopata wageni wa nje, kwani kuna wakati sisi tunaongea kiswahili wakati wenzetu hawaelewi, matokeo yake kukosa mantiki ya ujumbe wetu au sisi kutokupata taarifa kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinazopatikana baada ya kwenda safari za nje au Mabunge ya nje zipate nafasi ya kutolewa taarifa Bungeni ili kubadilishana uzoefu. Kwa mfano, baada ya kuhudhuria chaguzi mbalimbali au mikutano mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa safari za kujadili mikataba ya nje kama vile *WTO, EPA* na kadhalika, Wabunge, wawakilishi wa wananchi pia washirikishwe ili Bunge lijue kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bajeti ya Kamati na Wizara yake iongezwe na ipewe kipaumbele. Pia Wabunge wanapoenda kusimamia chaguzi nchi za nje, wakatiwe Bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwakilishi ndani ya *SADC* kwa taarifa kuna mtindo wa kulipa posho tofauti kati ya wanaobaki mjini na vijijini na hivyo kufanya Wabunge wa vijijini kuwa na maisha magumu wakati wapo ugenini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, mimi naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya *TASAF* inasaidia japo baadhi ya maeneo yamebahatika kupata miradi mingi kuliko maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kuridhia uwakilishi wa wanawake katika ngazi za maamuzi kufikia 50%, mchakato ndani ya Bunge wa wadau wengine utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha utawala bora, Wilaya zenye maeneo makubwa na watu wengi kama ilivyo Mbinga na Tunduru, pia Majimbo yake yasaidiwe kugawanywa ili kuwafikishia wananchi wa maeneo hayo huduma kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na miji salama, mji kama Dar es Salaam na miji midogo hamna madampo ya uhakika na maeneo yanayopimwa yatengewe maeneo maalumu kwa ajili ya ukusanyaji wa taka.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipa ya

kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa ushindi mkubwa alioupata katika Jimbo lake la Tunduru.

Aidha, napenda kutoa pole zangu nyingi kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo kwa msiba walioupata. Naiombea roho ya Marehemu ilale mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Kamati ya Mambo ya nje ya Bunge kwa taarifa yake nzuri ambayo imeipa Wizara yangu faraja kubwa. Taarifa hiyo, pamoja na mapendekezo yake imekuwa na nia ya kutoa mwongozo kwa Wizara yangu ili itekeleze kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeyapokea mapendekezo hayo kwa mikono miwili na ninaahidi kwamba mapendekezo hayo tutayafuatilia na kuyatekeleza ipasavyo. Hivi sasa tayari baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa hapa yameanza kutekelezwa na tunajitahidi yale yote ambayo yamependekezwa tuyafanyie kazi kwa nguvu zetu zote. Kuhusu hatimiliki, tayari tunafuatilia za majengo yetu kule Msumbiji na baadhi zimeanza kupatikana. Kwa hiyo, tunajitahidi kufuatilia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo kuhusu Chuo cha Diplomasia yanaendelea kati ya Tanzania na Msumbiji na hivi karibuni tunaweza takapata jibu kutoka kwa wenzetu wa Msumbiji. Isipokuwa siyo rahisi kwa hivi sasa Chuo cha Diplomasia kikaitwa Chuo cha Diplomasia cha Tanzania kwa sababu Mkataba uliosainiwa unasema *Mozambique and Tanzania Centre for Foreign Relations*. Kwa hiyo, siyo rahisi kwa sasa kusema kwamba Chuo hiki kitakuwa cha Tanzania mpaka taratibu zilizopo ziweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajitahidi kuziwezesha Balozi zetu ili ziweze kufanya kazi zake vizuri, lakini hali yetu ya fedha ndiyo inaturudisha nyuma, lakini hali yetu ya bajeti ikituruhusu tutajaribu kuzisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliotoa michango yao, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe tumesikia, lakini tutajitahidi Ubalozi wetu wa Geneva na Balozi nyingine kama hizo ambazo zinafanya kazi za *multilateral* kuziwekea Maafisa wa kutosha. Lakini hilo nalo tatizo lake ni fedha na tutashukuru kama Bunge hili litatusaidia ili tuweze kupata fedha za kutosha za kukidhi haja kuwa na Maafisa wengi katika Balozi zetu. Ni kweli dira yetu sasa hivi ni Diplomasia ya Kiuchumi na lazima tuwe na wataalam kama nilivyojibu swali hapa kwamba lazima tuwe na wataalam wa kutosha, wenye uwezo na uzoefu katika mambo ya uchumi na biashara. Kwa hiyo, tunajitahidi kutafuta wafanyakazi wa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu litusaidie kupata fedha kwa ajili ya kufanyia shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajitahidi kufuatilia suala la Visa kwa ajili ya Ubalozi wa Uingezera, lakini kama tunavyojua, wale ni wagumu kama ilivyosemwa ni

nchi kubwa. Lakini tunajitahidi na wao wenyewe wanasema kwamba hakuna haja ya Watanzania kwenda pale kupanga foleni kwa sababu wamefungua tovuti, kila kitu kinatoka katika tovuti. Lakini mimi nimeshafanya mazungumzo na Balozi wa Uingereza mara mbili kwa ajili ya kutatua tatizo hili na nimemwambia siyo wote wanaoweza kutumia tovuti kwa ajili ya kujaza fomu hizo kuomba Viza. Kwa hiyo, tunajitahidi kuongea na Ubalozi wa Uingereza na vilevile Ubalozi wa Marekani kuona namna gani wanaweza kutusaidia wananchi wetu waweze kupata Viza hizo kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Killimbah amezungumzia habari ya wafanyakazi katika Ubalozi wetu wa Japan, Ubalozi wa Ujerumani na kadhalika, lakini nimeshajibu hilo kwamba tatizo ni fedha kupeleka watu wetu kule waweze kufanya kazi vizuri na kwa wingi. Siku hizi Wizarani kwetu kupata ajira mpaka tupate kibali cha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndiyo uweze kuajiri. Kwa hiyo, tunapata ugumu kidogo. Tunaweza kuhitaji Maofisa tuseme 20, lakini tunaambiwa tuajiri Maafisa 10. Kwa hiyo, hatuwezi kukidhi haja kuweza kupeleka Maafisa wa kutosha katika Balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma Killimbah, safari za Rais, tutajitahidi kama Wizara kumshauri Rais ili tuweze kumworodheshea watu wale wa safari hasa wanaohusika na siyo wale wa Ikulu peke yao.

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Ninafahamu Waheshimiwa Mawaziri kwamba muda ni mfupi, lakini tunaamini kwamba hoja hizi za Waheshimiwa Wabunge itakuwa vizuri sana kama mtazijibu vizuri ikiwezekana hata mkatuletea kwa maandishi na hasa kwenye Kamati husika zikajibiwa vizuri na kuona katika mipango yenu ijayo mnaweza kuendelea kuzifanyia kazi. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mathias Chikawe. Ninaomba kuendelea kusisitiza kwamba azingatie muda na niendelee kusisitiza kwamba kujibu kwa maandishi ni muhimu sana kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge kadri ya hoja zao walivyozieleza mbele ya Bunge leo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa dakika tano na mimi niweze kutoa ufafanuzi kwa hoja chache ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, pia na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala.

Lakini kabla sijafanya hivyo, nami nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Nachingwea nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Dr. Aaron Chiduo na pia kwa wananchi waliofariki katika ajali ya basi la Buffallo kule Kisangara. Naziombea roho za Marehemu zilazwe mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mwenyekiti na Kamati kwa kazi nzuri waliyofanya, wametoa ripoti ambayo inaelezea shughuli zao kwa mwaka 2006. Baada ya kutoa shukrani hizo sasa na mimi nitoe mchango wangu katika sehemu mbili au tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imependekeza kwamba Wizara ya Katiba na Sheria ama Serikali ilete kitu kinaitwa *Legislative Progamme,* yaani Ratiba ya Miswada ambayo italetwa Bungeni katika kipindi cha mwaka mzima unaokuja. Sisi tunaliona jambo hilo ni zuri na tumelipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu tayari imekwishaziandikia Wizara zote ili zituletee orodha ya Miswada inayokusudiwa kuletwa katika Bunge katika kipindi cha mwaka 2007/2008. Nia ni kuandaa ratiba ambayo Waheshimiwa Wabunge wote watapewa ili wajiandae ni Miswada gani wanakuja kuijadili katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitoa mapendekezo kuhusu Tume ya Haki za Binadamu kwamba tungefungua ofisi Zanzibar na katika Mikoa mingine. Nafikiri hili sasa limepitwa na wakati maana kama Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu wanavyokumbuka wamepitisha mabadiliko ya Sheria kuruhusu Ofisi za Tume ya Haki za Binadamu kufunguliwa huko Zanzibar. Kuhusu kufungua ofisi Mikoani, hilo pia tutalizingatia, kinachotukwaza ni bajeti tu. Lakini tunakusudia kufungua ofisi mbili katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha huko Mwanza na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imezungumzia kuhusu uchakavu wa jengo la Kabidhi Wasii Mkuu. Ni kweli jengo hilo limechakaa na sisi tumeliona hilo na tunakusudia kujenga Ofisi ya kisasa kabisa katika sehemu ile ambayo itajumuisha Makao Makuu ya Wizara ya Katiba na Sheria. Hivi ninavyoongea, Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu tayari imekwishahama kutoka pale ili kupisha utaratibu wa ujenzi wa jengo hilo. Kwa hiyo, jengo la Kabidhi Wasii Mkuu litabadilika litakuwa zuri na litakuwa na vifaa vyote vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetoa pendekezo kwamba taarifa zinazotolewa na Tume ya Kurekebisha Sheria, zinapofanyiwa kazi, basi Tume hiyo iarifiwe kwamba taarifa yenu kadhaa tumeifanyia kazi. Hilo labda niseme tu kwamba Serikali huleta Miswada hapa Bungeni na Bunge huipitisha ikawa Sheria, halafu zinarudishwa kwa Serikali kutekeleza sheria hizo.

Sasa Serikali imekuwa ikitekeleza na baada ya muda ikaona kwamba haina njia ya kujua kwamba: Je, sheria hizi bado zina umuhimu ama zinapokelewa vipi na jamii? Ndiyo maana ikaundwa Idara moja ya Serikali ikaitwa Tume ya Kurekebisha Sheria ikapewa jukumu la kuzipitia sheria hizo na kuishauri Serikali kama Sheria hizo bado ni muhimu au hazifai zibadilishwe.

Kwa hiyo, ni Idara moja inaishauri Serikali na Serikali mara nyingi sana imekuwa ikichukua mapendekezo ya Tume na kuyafanyia kazi. Sioni sasa kama umuhimu tena wa

kurudi kuiambia Idara ile kwamba Idara hii imenipa mapendekezo haya nimeyafanyia kazi. Sijui kama kuna ulazima huo, lakini nafahamu tu kwamba mapendekezo ya Tume ya Kurekebisha Sheria yanafanyiwa kazi sana. Ni juzi tu tumepitisha Sheria ya Rushwa hapa.

Kipindi kilichopita tulipitisha Sheria ya Mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria ambayo sasa tunatumia ushahidi wa elektroniki *(Electronic Evidence)* Mahakamani. Hayo yalikuwa ni mapendekezo yaliyotoka kwenye Tume na kila mara Tume inaleta mambo mazuri ambayo tunayafanyia kazi. Lakini Serikali haioni kwamba sasa inalazimika kuiambia Idara yake moja kwamba wewe Idara ya Maji, basi kwa sababu umetufanyia hivi, tunakutangaza umetufanyia hivi wakati ni hiyo hiyo Serikali moja. Kwa hiyo, nafikiri Kamati iridhike kwamba Tume inafanya kazi nzuri na Waheshimiwa Wabunge waridhike kwamba Tume inafanya kazi nzuri na Serikali inatumia taarifa za Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Stephen Galinoma walizungumza kuhusu uchakavu wa Mahakama za mwanzo na mimi ninakubali. Ni kweli Mahakama za Mwanzo ni chakavu na Serikali inakusudi katika mpango wa Mpango wa Mageuzi katika Sekta ya Sheria *(Legal Sector Reform Programme)* kurekebisha Mahakama nyingi na kujenga mpya nyingi pia. Natumaini basi, tutazingatia maoni yao wakati tunapotekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ruth Msafiri alizungumzia pia kuhusu watoto wadogo kufungwa na mama zao. Hili linatokea kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi leo asubuhi kwamba mtoto akiwa mdogo, basi akimaliza kunyonya kama inawezekana arudishwe kwa jamii. Lakini inaposhindikana, basi inabidi akae mle ndani na mama yake. Lakini Serikali haikusudii kuwafunga hao watoto kwa kosa kama hilo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi kama ulivyosema, tutawajibu Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi tutayaleta. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Dr. Aaron Chiduo. Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Mbunge mwenzetu aliyepata nafasi ya kuingia katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimetolewa hoja mbalimbali ambazo naomba niseme ni zile zinazogusa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, tutazifanyia kazi na kuleta majibu kwa maandishi kwa ajili ya kumbukumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu kwa haraka haraka kwamba alivyosema Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe kwamba ni vizuri tukajikita zaidi

kwenye uchumi, tusishabikie siasa tu kwenye masuala ya Afrika Mashariki. Ni kweli kwa sababu hata Mkataba wenyewe unaohusu Afrika Mashariki ukitazama zile hatua, hatua ya kwanza ambayo ni Umoja wa Forodha, ya pili Soko la Pamoja na ya tatu, sarafu moja na hayo yote ni uchumi. Kwa hiyo, hakuna la kuchagua hapa. Tutake tusikate lazima tujikite zaidi katika masuala ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile wapo waliouliza kwamba ushuru wa forodha unaendelea vipi? Unaendelea japokuwa matatizo ya hapa na pale yanapojitokeza tunakaa, tunayazungumza, tunapata muafaka. Lakini muda sio mrefu tutafanya tathmini ya kuangalia ni mambo yapi yanajitokeza na nini tufanye ili kuyakosoa hayo. Nitoe wito kwa Watanzania, basi pale ambapo wafanyabiashara au watu wengine wanaoshiriki katika masuala ya kufanya biashara, ushuru wa forodha wanapokutana na jambo ambalo sio la kawaida wasisitize kutujulisha haraka pale Wizarani ili tuweze kuchukua hatua za haraka badala ya kusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la pamoja ni kwamba, hivi sasa tupo katika maandalizi ya kuanza mazungumzo na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, tayari imeziandikia Sekta zote ili zifanye maandalizi ya awali ya kuangalia ni mambo yapi ya msingi tutayazingatia katika mazungumzo ya soko la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile na hoja mbalimbali zimekuwa zikitolewa na wananchi kuhusu masuala ya ardhi, kuhusu masuala ya ajira na mambo mengine yote hayo tutayazingatia katika mazungumzo ya kuweka Itifaki ya soko la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya kukusanya maoni inaendelea kufanya kazi. Tunatambua kwamba, wapo Watanzania ambao wamekuwa na wasiwasi kwamba labda inapigia debe badala ya kukusanya maoni. Lakini tunakiri ugumu wa kazi waliyonayo, maana walipewa kazi mbili. Kazi mojawapo ni kuelimisha na kazi nyingine ni kukusanya maoni. Sasa wanapokuwa wanaelimisha, wakati mwingine wanateleza. Sasa pale wanapoteleza tuwasamehe, lakini kazi kubwa waliyonayo ni kuhakikisha wanakusanya maoni ambayo yatatuongoza twende vipi katika Shirikisho ama twende taratibu ama twende haraka, hayo yote yatategemea Watanzania watasema nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kupigiwa kengele. Niseme tu kwamba naunga mkono hoja zote mbili mia kwa mia na ninaahidi kwamba tutaleta maelezo ya kina kwa maandishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nafikiri Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala tuna nafasi nzuri sana tarehe 21 Aprili, 2007 kuweza kupata mjadala mwingine mkubwa na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tutakuwa na semina ya kuelekea kwenye Shirikisho. Kwa hiyo, tutakuwa na nafasi ya kutosha.

Kwa hiyo, tunaomba mjiandae pia na hayo yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nimpe dakika chache *Chief Whip* azungumze masuala ya Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Bunge na kadhalika yamezungumzwa kwa nguvu sana kwenye mchango huu. Naomba atumie dakika chache kuhusu hilo, tuwape watoa hoja wahitimishie hoja zao.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile nina dakika chache, naomba tu niseme kwamba kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba niwapongeze Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote mbili ambazo zimewasilisha taarifa zao leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali, nasema kwamba kazi hiyo wameifanya ni kubwa na ni nzuri sana na sisi tunazichukua taarifa hizo kama ni nyenzo muhimu za kuweza kutuwezesha kujiimarisha zaidi na kuendelea kutekeleza wajibu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mbalimbali yamewasilishwa katika taarifa hizo, yamegusa katika Sekta na Wizara mbalimbali na masuala mengi yameelezewa kuhusu Sekta ya Utawala Bora, Utumishi wa Umma na Wizara ya Tawala za Mitaa na Serikali za Mitaa. Naomba niliahidi Bunge hili kwamba Wizara zote zinazohusika ambazo zimetajwa hapa tutazipelekea taarifa hii ili waweze kuleta taarifa na kuweza kuona majibu ya mambo mliyoyahoji yanapatiwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu, masuala mbalimbali yameulizwa ambayo mimi ninahusika nayo moja kwa moja. Suala la Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu, tumelipokea na sisi tupo katika mpango wa kuimarisha ofisi ile. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie kwamba suala hili tutalichukua kwa uzito wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lililouliziwa hapa ni kuimarisha *TACAIDS*, Tume ya Kudhibiti masuala ya UKIMWI. Leo hii katika moja ya Programu aliyokuwa nayo Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kukutana na Tume ya *TACAIDS*. Kwa hiyo, katika moja ya malengo ni kuhakikishia kwamba wanatekeleza wajibu wao na kuimarika katika utendaji wao hasa baada ya semina ile tuliyofanya siku ya Jumamosi. *(Makofi)*

La mwisho ambalo limegusiwa na wengi na mimi mwenyewe ninahusika ni suala zima la hoja ya masuala ya Bunge. Tumelichukua suala hilo, tutalijadili katika ngazi mbalimbali na tutalifanyia kazi. Kuna hoja zilizokamilika na kuna nyingine ambazo zinafanyiwa kazi. Naomba niwaahidi kwamba tutayashughulikia kwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja zote mbili. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Naomba sasa nimwite Mtoa hoja Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili na yeye aweze kutumia dakika tano kuzungumzia hoja yake. Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali!

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda

nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuhimitisha hoja ambayo imetolewa katika Bunge lako Tukufu. Kwanza, naomba niwatambue Wabunge wote ambao wamechangia hoja yangu na wote wameunga mkono hoja hii, ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Stephen Galinoma, Mheshimiwa Mathias Chikawe, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Dr. Batilda Burian - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Aliyechangia kwa maandishi ni Mheshimiwa *Eng*. Stella Manyanya. *(Makofi)*

Niwashukuru wote ambao wamechangia na hoja nyingi zimeelekezwa Serikalini, nawashukuru Mawaziri wamejitahidi kuzijibu. Lakini labda tu naomba kusisitiza mambo yafuatayo: Kwanza, Mheshimiwa Ruth Msafiri alizungumzia suala la *TASAF*, naomba niipongeze *TASAF* wanafanya kazi nzuri sana. Kamati ilipata nafasi ya kukagua Miradi ya *TASAF* Tanga, Pemba, Unguja na katika baadhi ya Mikoa. *(Makofi)*

Kuna matatizo ambayo yamejitokeza. *TASAF* awamu ya kwanza ilihusisha Wilaya 40 na ule mchakato wa kuibua miradi ulikuwa ni mwepesi. Kwa sababu miradi ilikuwa inaibuliwa na wananchi, baadaye wananchi wanapeleka taarifa kwenye Halmashauri za Wilaya na Halmashauri za Wilaya zinapeleka taarifa Makao Makuu ya *TASAF* na wanapewa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo. *TASAF* ya awamu ya pili ilihusisha Wilaya zote Tanzania Bara pamoja na Pemba na Unguja. Lakini mchakato wa kuibua miradi ni mrefu.

Kwanza, wananchi wanaibua mradi wanapeleka taarifa kwenye Halmashauri ya Wilaya, Halmashauri ya Wilaya inapeleka *TASAF* Makao Makuu na *TASAF* Makao Makuu wanapeleka kwenye Wizara inayohusika. Sasa Wizara zina miradi mingi. Kwa hiyo, tunashauri kwamba mchakato huo ungeangaliwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Grace Kiwelu, amezungumzia sheria zilizopitwa na wakati. Ni kweli Kamati yangu ilipotembelea Tume ya Kurekebisha Sheria tulipewa taarifa na tayari sheria hizo ambazo zimefanyiwa utafiti na Tume ya Kurekebisha Sheria zimekwishapelekwa Wizara ya Katiba na Sheria.

Kwa hiyo, ushauri wa Kamati ni kwamba, sheria hizo hasa Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi zifanyiwe marekebisho kwa sababu wananchi wanapata kero kubwa sana na usumbufu hasa katika malipo ya mirathi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Stephen Galinoma alizungumzia suala la Mahakama ya Kalenga. Bahati nzuri mwaka huu tulitembelea Mahakama ya Kalenga. Lile jengo la Mahakama halifai kabisa. Kwa hiyo basi, tunaishauri Serikali kujenga jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo Kalenga ili wananchi waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ucheleweshwaji wa fedha za ruzuku. Hili nakubaliana nalo, lakini vilevile wananchi kwa mfano Halmashauri kunyimwa fedha eti kwa sababu kuna ubadhirifu, Mtendaji amefanya kosa Halmshauri inanyimwa fedha. Kwa kweli hatuwatendei haki wananchi. Kwa hiyo, aadhibiwe yule aliyefanya kosa la ubadhirifu lakini sio wananchi. Kwa hoja hii, tunamshukuru sana Mheshimiwa Galinoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, sasa ikubaliwe na Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipitishwa na Bunge)*

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashukuru sana watu waliopata nafasi ya kuchangia taarifa hii. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Waheshimiwa Wabunge sita waliochangia kwa kuzungumza na wengine wanne wamechangia kwa maandishi. Wa kwanza alikuwa ni Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe - Mbunge wa Kyela, Mheshimiwa Charles Kajege - Mbunge wa Mwibara, Mheshimiwa Juma Killimbah - Mbunge wa Ilamba Magharibi, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo - Mbunge wa Kilindi, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idi - Mbunge wa Kitope, Mheshimiwa Diodorus Kamala -Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mbunge wa Nkenge, Naibu Waziri Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro na Mheshimiwa Castor Ligalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge ni ya kutilia mkazo yale yaliyopo katika taarifa na mimi nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa sababu wamefafanua baadhi ya mambo vizuri zaidi na yameeleweka vizuri zaidi kuliko kama yalivyo kwenye taarifa ambayo ni fupi. Nawashukuru wote kwa michango yao mizuri.

Labda niseme jambo moja ambalo alilizungumzia Mheshimiwa Kajege na ambalo namshukuru sana Mheshimiwa Diodorus Kamala - Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa maelezo yake kwamba kwa bahati sijui niseme mbaya ama ndivyo hali ilivyo hata hizo sekta katika mambo yote yanayojadiliwa katika Afrika Mashariki yako kisekta, wa Afya wanakwenda kwa sekta yao, wa biashara na sekta yao, kila watu na sekta yao. Kwa hiyo, sio rahisi Kamati hii kupata kila kitu kutoka kwenye hizo Kamati za kitaalam.

Mimi ninatumaini kwamba, Wizara husika ndiyo ambayo ingefanya uratibu, vinginevyo Kamati italazimika kwenda kwa kila Wizara ya sekta inayohusika, jambo ambalo kidogo linaweza likaleta ugumu. Kwa hiyo, ninachoomba, Wizara husika yenyewe ndiyo ingechukua kila kitu halafu sisi tutawauliza watatueleza yale ambayo tumeshauriwa tuyafahamu. Lakini utakuta kwamba yanaingia pia katika sekta ya Kamati nyingine na mimi nina hakika kabisa tutapata hapo baadaye maelezo mazuri.

Tumesikia mambo mazuri tu, marafiki tuliokuwa nao huko nyuma na habari za Msumbiji na kila kitu kama hivi ilivyoelezwa, haya yote yanachukuliwa hatua. Sasa kwa maandishi, yapo mambo mengi mazuri ambayo kwa bahati mbaya kwa kuwa hawakusema Mawaziri, hawakuyajua wala kuyasikia.

Lakini hata yale yaliyosemwa mimi nilikuwa nafikiri kwa utaratibu mzuri sisi Kamati tutayachukua haya yaliyoandikwa na yale yaliolezwa tukae pamoja na Wizara husika moja hadi nyingine tupate majibu ili yatakapojibiwa yawe yanatosheleza. *(Makofi)*

Vinginevyo pia, itakuwa ni nusu nusu. Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, napenda kuwashukuru sana wale waliochangia, ni matumaini yangu kwamba huu ulikuwa mwanzo na ninahakika huko tunakokwenda taarifa hizi zitatengewa muda wa kutosha kujadiliwa na maoni haya yanaweza kupata nafasi nzuri sana ya kupata majibu yake. Ahsate sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea taarifa hii ya Kamati ya Mambo ya Nje kwa mwaka 2006.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa kuafiki na kuzipitisha taarifa zote mbili. Naomba niwapongeze sana Wenyeviti wetu hawa wawili kwa taarifa zao, lakini naomba niwapongeze Wajumbe wa Kamati zote mbili, kwa kweli kazi waliyoifanya, wameweza kutuwakilisha kwa namna ya pekee sana katika Kamati zao.

Ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu na ninaomba niendelee kusisitiza mtusaidie kupata maandishi.

Waheshimiwa Wabunge, kazi zilizopo katika meza yangu zinakaribia kwisha. Kwa mujibu wa Kanuni Na. 21 (6) ambayo inazungumzia hoja ama maelezo binafsi inasema kwamba endapo Spika atakuwa amepokea taarifa ya Mbunge yeyote anayetaka kutoa maelezo yake chini ya fasili ya (9) ya Kanuni hii, basi Bunge litatakiwa liahirishwe mapema kabla ya muda wake ili Mbunge huyo aweze kufanya anachotaka kufanya.

Kwa maana hiyo, ninaomba kuwapa taarifa kwamba Mheshimiwa Dr. Slaa amepeleka hoja yake binafsi kwa Mheshimiwa Spika, ameona inafaa kuletwa Bungeni na Serikali imepatiwa taarifa ya hoja hiyo, nayo ipo tayari kumsikiliza Dr. Slaa. Kwa hali hiyo, ninaomba nimwite Waziri wa Nchi ili kwa mujibu wa Kanuni za Bunge aweze kuahirisha Bunge hili mapema na tumpe nafasi Mheshimiwa Dr. Slaa atoe hoja yake na hivyo tutaendelea na taratibu zetu kadiri Kanuni zinavyotuongoza. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, karibu!

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwa mujibu wa Kanuni ya 21(6), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa kabla ya muda wake, na kwa sasa ni saa 1.40 usiku hadi tutakapokutana kesho saa tatu Asubuhi, ili kutoa nafasi kwa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa Mbunge wa Jimbo la Karatu aweze kutoa maelezo yake binafsi chini ya fasili ya (9) ya Kanuni ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki.

*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Dr. Slaa aweze kuleta maelezo yake mbele ya Bunge.

## MAELEZO KUHUSU MATUMIZI YA ZIADA YA SERIKALI 2003/2004

**MHE. WILBROD P. SLAA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshimiwa na taadhima, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi kwa kuweza kutoa maelezo yangu binafsi kuhusu matumizi ya ziada ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 chini ya Kanuni 21 (6), (9).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maelezo yangu, ninaomba kwa sekunde moja niwapongeze sana wenzangu pamoja na Wenyeviti wa Vitongoji kadhaa walioshinda uchaguzi leo pale Katesh, Makao Makuu ya Wilaya ya Hanang na kuwa Wenyeviti wa Vitongoji. Nawapongeza sana wananchi wa Hanang kwa kuwa na imani na CHADEMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 12/4/2006, wakati Bunge lilipokaa kama Kamati ya Bunge Zima kupitisha Muswada wa Matumizi ya ziada ya Serikali, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto alihoji juu ya ukiukwaji wa Kifungu 19 (1) na 19(2) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sheria Na. 6 ya mwaka 2001*(Public Finance Act, Act No.6 of 2001)* kuhusiana na Hoja ya Matumizi ya Ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Kabwe, kama alivyonukuliwa na *Hansard* ya tarehe husika ilikuwa ni kuhoji uhalali wa Serikali kuleta Muswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Serikali, kabla ya kuleta taarifa ya matumizi ya ziada *( Statement of Excess)* ambayo kwa mujibu wa Sheria yanatakiwa yaletwe mbele ya Bunge na kukubaliwa kwa hoja ambako kungepelekea kuletwa kwa Muswada wa Matumizi ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa hoja ya Mheshimiwa Kabwe ni Kifungu 19(1) na 19 (2) cha Sheria tajwa hapo juu, naomba kunukuu: *Section 19 (1) "If at the close of account for any financial year it is found that moneys have been expended:*

(a) *On any expenditure vote in excess of the amount appropriated for it by an appropriation Act .*

(b) *For a purpose for which no money have been voted and appropriated; or*

(c) *On any sub- headed of an expenditure vote in excess of the sum assigned thereto the estimates of expenditure for the financial year and to which no further sum has been applied under any provision of this Act or any subsidiary legislation issued under it, the amount of the excess expended or not appropriated as the case may be shall be included in a statement of expenditure in excess which shall be laid before the National Assembly.*

*Section.19(2) "Where the National Assembly shall, by means of a motion allow* (Mkazo upo kwenye *allow*) *any excess or any amount expended or not appropriated to stand charged to Public Funds, the sum required to meet such excess or such amount shall be allowed, shall be included in a supplementary appropriation Bill for Appropriation."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri sahihi ya kipengele husika ni kwamba, taarifa ya matumizi ya ziada inatakiwa iletwe Bungeni ambapo Bunge kwa hoja likubaliane na matumizi husika ya ziada, kutakapopelekea matumizi hayo ya ziada kujumuishwa kwenye Muswada wa Matumizi ya Ziada, kama ilivyowekwa wazi na kifungu cha 19(2) cha Sheria iliyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akijibu hoja ya Mheshimiwa Kabwe na akiungana na angalizo lililotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Zima siku hiyo, Waziri wa Miundombinu alisema yafuatayo, naomba kunukuu:

"Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa mchango wa Mheshimiwa Kabwe Zitto lakini unaposema *by motion, motion* ni hoja, inatolewa hoja ya kuwasilisha *Statement* ya *Excess*. Ukisema kwamba Serikali haikufuata hata utaratibu wa *motion* kidogo naanza kushangaa kwani wewe ni Mwanasheria na ni vizuri tunapoyatumia maneno haya '*motion'* nadhani nimempa *title* ambayo si yake niwie radhi. Lakini *motion* maana yake ni kwamba una hoja rasmi mbele ya Bunge na maana ya hoja ni kwamba naomba kutoa hoja kwamba niwasilishe *Statement* ya Excess kwa mwaka 2003/2004, hoja hiyo inaungwa mkono na tayari imeiva. Ndiyo maana yake. Uzito nimeweka mimi.

Unakuja kwa hatua ya pili kwa sababu tunaomba sasa zile pesa ziingizwe kwa utaratibu sasa wa *appropriation* ndiyo Muswada unawasilishwa kama ilivyofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ulipoanza kusema kwamba: "Asubuhi *Order Paper* ilikuwa na mtiririko huo na kilichofanyika ni sahihi kabisa wala hakuna Sheria ambayo imekiukwa". Mwisho wa Kunukuu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika tarehe 12/4/2007 ni kwa Waziri wa Fedha kuwasilisha Hati ya Matumizi ya Ziada kwa mwaka 2003/2004 *(The Statement of Excess for the Year 2003/2004)* kwa mujibu wa kifungu 31(1)(a). Rejea orodha ya shughuli za Bunge, Mkutano wa Saba, Kikao cha Tatu -Tarehe 12/4/2007 katika utaratibu wa kawaida wa kuwasilisha hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna hoja yoyote iliyotolewa kuhusiana na matumizi ya ziada iliyotolewa na Waziri husika ikaungwa mkono na Bunge kwa mujibu wa Kifungu cha 19(2), ambayo inataka Bunge "liruhusu" *(allow)* matumizi hayo ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi la kujiuliza, Bunge litapitishaje matumizi ya ziada pasipo lenyewe kufahamu kiasi sahihi cha matumizi ya ziada? Hii inatokana na ukweli kwamba Waziri alipowasilisha Hati Bungeni zaidi ya kusoma kichwa cha habari *(Heading)* cha hati husika, hakutoa taarifa Bungeni kwa undani jinsi matumizi hayo ya ziada yalivyofanyika na kisha kutoa hoja kwa Wabunge. Hoja ambayo kama ingetolewa, kujadiliwa na kuungwa mkono na Wabunge kipengele cha 19(2) cha Sheria husika kingekuwa kimezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lilipata ufahamu wa matumizi ya ziada pale Naibu Waziri wa Fedha alipokuwa akiwasilisha Bungeni hotuba ya Muswada wa Matumizi ya Ziada kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa, katika hatua hata muswada ulikuwa haujagawiwa kwa Wabunge, kwani ni baada ya kuwasilishwa ndio uliwekwa kwenye visanduku vya Wabunge. Huu ni uvunjwaji dhahiri wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kwamba Waziri wa Miundombinu alilipotosha Bunge na kwa kuzingatia kwamba Serikali haikufuata Sheria katika kuleta Muswada wa Matumizi ya Ziada, tunataka Serikali ifafanue kauli yake ambayo kwa dhahiri kabisa ni kinyume na utaratibu uliowekwa na Sheria iliyotajwa hapo juu kifungu cha 19(2) na iwapo inakubali kuwa utaratibu huo haukufuatwa, basi tunaiomba ifute kauli yake kwamba kitendo cha Hati kuwasilishwa Mezani, maana yake ni 'hoja imetolewa mbele ya Bunge na kuungwa mkono' kama alivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuliachia suala hili lilivyo ni kupotosha sheria, utaratibu sahihi na kumbukumbu sahihi za Bunge. Bunge ni lazima lifanye kazi kwa mujibu wa Sheria na liwe mfano wa kutekeleza Sheria iliyotunga lenyewe ili liweze kuzisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema tutafakari kwamba kukubali kukosea ni uungwana na kusahihisha jambo ni utaratibu wa kawaida katika jamii yoyote. Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Slaa, kwa kutumia utaratibu wa Kanuni zinazompa ruhusa Mbunge yeyote kuwasilisha maelezo yake binafsi anapoona kwamba inafaa kufanya hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wetu unasema kwamba, Serikali baada ya kusikia maelezo hayo ama inaweza ikajibu wakati huo huo ama akapangiwa nafasi nyingine muafaka katika ratiba zilizopo ndani ya ratiba za Bunge katika kipindi kicho na ikatoa majibu ya maelezo ya hoja hiyo iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge. Sasa kulingana na muda, nitaomba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu atoe maelezo ya Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, kutoa maelezo ya Serikali kuhusu maelezo ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kuhusu maelezo ya Serikali wakati wa Bunge kupitisha Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 12 Aprili, 2007 wakati Bunge lilipokaa kama Kamati ya Bunge Zima kupitisha Muswada wa Matumizi ya Ziada ya Serikali, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto alihoji juu ya ukiukwaji wa Kifungu cha 19(1) na (2) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Bunge likiwa katika hatua ya Kamati ya Bunge Zima, Mheshimiwa Kabwe Zitto - Mbunge wa Kigoma Kaskazini, alisimama na kuhoji uhalali wa Serikali kuwasilisha Muswada wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Serikali, kabla ya kuleta taarifa ya matumizi ya ziada, ambayo alisema, yanatakiwa yaletwe mbele ya Bunge na kukubaliwa kwa hoja ambapo ingepelekea kuletwa kwa Muswada wa Matumizi ya Ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine yaliyotokea, Waziri wa Miundombinu - Mheshimiwa Andrew Chenge alitoa maelezo kwamba, nanukuu: "Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa mchango wa Mheshimiwa Kabwe Zitto, lakini unaposema *by motion*, *motion* ni hoja. Inatolewa hoja ya kuwasilisha *Statement* ya *Excess*. Ukisema kwamba Serikali haikufuata hata utaratibu wa *motion,* kidogo naanza kushangaa, kwani wewe ni Mwanasheria na ni vizuri tunapoyatumia maneno haya '*motion*' nadhani nimempa *title* ambayo sio yake, niwie radhi.

Lakini *motion* maana yake ni kwamba, una hoja rasmi mbele ya Bunge na maana ya hoja ni kwamba, naomba kutoa hoja kwamba niwasilishe *Statement* ya *Excess* kwa mwaka 2003/2004. Hoja hiyo inaungwa mkono na tayari imeiva. Ndiyo maana yake, uzito naweka mimi. Unakuja kwa hatua ya pili, kwa sababu tunaomba sasa zile pesa ziingizwe kwa utaratibu sasa wa *appropriation* ndiyo Muswada unawasilishwa kama ilivyofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ulipoanza kusema asubuhi kwamba *Order Paper* ilikuwa na mtiririko huo na kilichofanyika ni sahihi kabisa wala hakuna sheria ambayo imekiukwa." Mwisho wa Kunukuu. Baada ya maelezo ya ufafanuzi wa utaratibu uliowekwa katika kifungu cha 19(2), Bunge lilipitisha Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, ametoa maelezo binafsi chini ya Kanuni ya 21(6) na (9) akitaka Serikali itoe ufafanuzi kuhusu kauli au maelezo yaliyotolewa na Serikali. Kwa maoni yake, maelezo ya Serikali hayakuwa sahihi na kwamba Serikali kwa dhahiri kabisa ilifanya kinyume cha utaratibu uliowekwa na Sheria chini ya kifungu cha 19(2) na iwapo Serikali inakubali kuwa utaratibu huo haukufuatwa, basi ifute kauli yake kwamba kitendo cha Hati kuwasilishwa Mezani, maana yake ni hoja imetolewa mbele ya Bunge na kuungwa mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kueleza kwamba haikuwa sahihi alivyosema Mheshimiwa Dr. Slaa kwamba Serikali ilivunja au kukiuka utaratibu uliowekwa na Sheria. Rekodi sahihi ni kwamba, Muswada wa Matumizi ya Ziada ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 uligawiwa kwa Wabunge mwezi Februari, 2007, wakati wa Kikao cha Sita cha Bunge na *"Hansard"* inaonyesha kuwa Muswada huo Ulisomwa Mara ya Kwanza tarehe 10 Aprili, 2007. Ipo kumbukumbu pia kwamba ni Wabunge wachache tu ambao hawakuwa na nakala ya Muswada ama kwa kuchelewa kupata kutoka Ofisi ya Katibu wa Bunge au kwa kusahau Jimboni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19(1) kinaelekeza kuhusu Matumizi ya Ziada ya Serikali kwamba kiasi cha fedha za ziada kilichotumika au ambacho hakikuidhinishwa na Bunge kitaingizwa katika Maelezo ya Matumizi ya Ziada ambayo yatawasilishwa Bungeni. Hii ndiyo hatua ya kwanza ambayo Naibu Waziri wa Fedha alitekeleza tarehe 12 Aprili, 2007 asubuhi kwa kuwasilisha Mezani Hati kuhusu Matumizi hayo ya ziada.

Hatua ya pili ni ile inayoelekezwa katika kifungu cha 19(2). Kutokana na umuhimu wake, nanukuu kifungu hicho kama ifuatavyo:-

*"(2) Where the National Assembly shall, by means of a motion allows any excess or any amount expended but not appropriated to stand charged to public funds, the sum required to meet such excess or such amount as shall be allowed, shall be included in a Supplementary Appropriation Bill for appropriation."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hatua ya pili inayoendana na maneno: *"Where the National Assembly shall, by means of motion allows any excess or any amount expended but not appropriated to stand charged to public funds..."* Yaliyomo katika kifungu cha 19(2), Serikali kupitia Naibu Waziri wa Fedha ilitoa Hoja wakati wa kuwasilisha Muswada kwamba Bunge sasa lijadili na kupitisha Muswada huo na mwisho alitamka maneno "Naomba Kutoa Hoja". Hoja iliungwa mkono na Wabunge wa upande wa Serikali.

Baada ya Hoja hiyo kuungwa mkono, Mheshimiwa Naibu Spika, , alilitaka Bunge lijadili Hoja hiyo. Ikumbukwe kwamba wakati Naibu Waziri wa Fedha anawasilisha Hoja ya Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza, alieleza kwa kina sababu zilizosababisha Matumizi hayo ya ziada kufanyika, hivyo kuwapa Waheshimiwa Wabunge uwanja mpana wa kujadili hoja hiyo. Ili hoja ya Mheshimiwa Kabwe Zitto na

sasa Mheshimiwa Dr. Slaa, iweze kutekelezwa kwa tafsiri yao, basi Mbunge yeyote angeweza kusimama na kuanza kujadili Hoja iliyotolewa kabla mjadala mahsusi wa Muswada haujaanza. Hilo halikutokea na hakuna yeyote aliyetaka mjadala huo uwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata kama yeyote angedai kufanya hivyo, hakuna Kanuni katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2004 ambayo imeweka utaratibu huo. Zipo sheria nyingi zinazoweka masharti ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali, lakini utaratibu huo hauwezi kuwa mbadala wa Kanuni za Kudumu za Bunge, ambazo kimsingi, zinasomwa pamoja na Ibara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hakuna Kanuni mahsusi, Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2004 zinampatia Spika mamlaka ya kutoa mwongozo na katika suala hili, Spika alikubaliana na utaratibu ambao Serikali iliona unafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza hatua ya tatu inayohusu maneno: *"The sum required to meet such excess or such amount as shall be allowed, shall be included in a Supplementary Appropriation Bill for appropriation."*

Hatua hii ilifikiwa pale Bunge lilipoanza kujadili Muswada husika na baadaye kuhitimishwa na Waziri wakati akitoa majumuisho. Katika kukamilisha majumuisho, Waziri alitamka maneno: "Naomba Kutoa Hoja" na Hoja hiyo iliungwa mkono. Hatua hii ndiyo ilitoa fursa kwa Bunge kuidhinisha au kutokuidhinisha Matumizi ya Nyongeza yaliyoombwa na Serikali kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19(2) cha Sheria ya Fedha za Umma, kinatamka kwamba *"The National Assembly shall, by means of a 'motion' allow any excess or any amount expended."* Neno "*motion*" chini ya Sheria hii halijatafsiriwa na hivyo, kwa Kanuni za Tafsiri ya Sheria, unalipa maana ya kawaida. Tafsiri ya neno *"motion"* ni hoja.

Kwa hiyo basi, maana ya kifungu hiki ni kwamba, kutatolewa hoja na Serikali kulitaka Bunge likubali Matumizi ya Ziada. Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, haiweki mfumo maalum *(format)* wa jinsi hoja ya Matumizi ya Nyongeza itakavyoletwa Bungeni.

Vile vile, kama nilivyoeleza hapo awali, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2004, haziainishi utaratibu wa kuwasilisha hoja hiyo. Kwa hiyo, Serikali ilitumia utaratibu ulioainishwa ndani ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuhusu uwasilishaji wa muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili kutoa ufafanuzi kuhusu maelezo ya Serikali na kufafanua maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Waziri wa Miundombinu wakati Bunge lilipokuwa linapitisha Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Ziada ya Serikali wa Mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimshukuru Mwanasheria Mkuu kwa kujibu maelezo binafsi yaliyoletwa na Mheshimiwa Dr. Slaa. Huo ndio utaratibu wa Bunge, kama Mbunge ana maelezo yake binafsi anayaleta na Serikali inapata muda wa kutafakari maelezo haya na kutoa majibu na ikiwezekana papo kwa papo kama ilivyokuwa leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujamaliza shughuli zetu zilizopangwa katika siku hii ya leo, nafikiri wote mmegawiwa tangazo la uchaguzi wa Wajumbe wawili wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ama Katibu wa Bunge, anapenda kuwaarifu kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005, kifungu cha saba (7), Bunge linatakiwa kuchagua Wabunge wawili tena kwa usawa wa jinsia, Mwanaume mmoja na Mwanamke mmoja watakaoingia katika Baraza la Chuo Kikuu. Uchaguzi huo tulishaufanya, lakini Sheria hiyo ambayo ilitungwa mwaka 1970 imefutwa na hivyo basi, inatupasa kuanza kwa kulingana na Sheria ambayo imeshapitishwa tena na Bunge.

Kwa hiyo, wale wote wanaofikiria wangependa kutuwakilisha katika Chuo hicho Kikuu, basi wakachukue fomu kwa Katibu wa Bunge na uchaguzi tutaufanya siku ya Ijumaa saa kumi jioni. Kwa hiyo, naomba niwaalike Waheshimiwa Wabunge wale wote wanaoona kwamba watafaa kutuwakilisha huko, basi wakachukue hizo fomu na waweze kupigiwa hizo kura tuwachague wakatuwakilishe huko kwa kadri ya utaratibu wetu kama ulivyo.

Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa ushirikiano kwa shughuli zetu zilizopangwa jioni hii ya leo. Sasa kwa mujibu wa utaratibu, kwa kuwa kazi zetu zote tumezimaliza, basi ninaomba niwatangazie kwamba tunaahirishwa Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 02.00 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 18 Aprili, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*